# Mafunzo ya Imani ya Kweli

## Tumia Pamoja na Biblia




# Knessiah Print Media

© Knessiah Church of Elohim

## Toleo la Kwanza

# UTANGULIZI

Kitabu hiki kimeandikwa ili kikusaidie katika kuchunguza mafundisho ya kina yanayopatikana katika Maandiko Matakatifu. Katika kurasa hizi, utagundua mkusanyiko wa masomo ya kibiblia ulioandaliwa kwa umakini, yakichukua mifano mbalimbali kutoka kwa vifungu vya Maandiko ili kutoa uelewa wa kina na mpana kuhusu mapenzi ya Elohim kwa mwanadamu.

Biblia, kwa hekima yake Elohim, inatupa mwongozo wa kudumu, ikitufundisha jinsi ya kuishi kulingana na makusudi ya Muumba wetu. Kwa kuzingatia ushauri kamili wa Maandiko, ukichanganya mafunzo ya Agano la Kale na yale ya Agano Jipya, tunapata mtazamo wa kina wa mapenzi ya Elohim kwa watu wake. Masomo yaliyomo katika kitabu hiki yanakusudiwa kukusaidia kukabiliana na changamoto za maisha, kukubali mwito wako, na kuoanisha moyo wako na mpango wa milele wa Elohim.

Ni matumaini yetu ya dhati kwamba utakichukulia kitabu hiki kwa heshima, na kukitumia kama mwongozo wa kibinafsi katika safari yako ya imani. Unapojifunza Maandiko Matakatifu, chukua muda kutafakari juu ya hekima yake na uyatumie katika maisha yako. Biblia si tu mkusanyiko wa hadithi au mafundisho, bali ni Neno lililo hai la Elohim, lililokusudiwa kubadilisha na kuhamasisha wale wanaotafuta kuelewa na kulitii.

Tunatumaini kitabu hiki kitakusaidia katika safari yako ya kiroho ili upate kuimarisha uhusiano wako na Elohim, kikikuelekeza kuelewa mapenzi yake na maisha ya ukamilifu anayoyataka kwako. Tunakutakia baraka katika safari yako ya kuhekimika na imani.

# KUHUSU MAJINA

Lugha tofauti huwa na majina tofauti ya Muumba wa mbingu na nchi. Jambo hili linatia mioyo yetu hofu kwa sababu Muumba wa mbingu na nchi pamoja na mwanawe, Mwokozi wa ulimwengu wana majina yao ya kipekee, ila sio mchanganyiko wa majina mengi. Kama jinsi Suleimani anauliza katika Methali 30:4, majina haya yapo katika maandiko na ni ya kiebrania. Yalibadilishwa wakati biblia ilipotafsiriwa ili kuweka miungu ya mataifa yote duniani.Tutapata kujifunza zaidi katika mafunzo ya Amri ya kwanza na ya pili, na pia katika sehemu ya pili (Unabii) tutapata ni nani alibadilisha majina haya, na ni kwa nini aliyabadilisha.

Jina lililotumika katika kitabu hiki ni Elohim katika Kiebrania, kumaanisha (Mwenye uwezo). Marko 15:34 Jina la mwokozi ni Yahshuah Masihi (Kwa kiebrania ni Yahshuah Hamashiach – Mwana wa Elohim, Mwokozi aliyetiwa mafuta).

Majina haya tumefundishwa na wayahudi, ambao ndio warithi wa maagano ya kweli. Warumi 9:4-5; Zaburi 147:19-20

Ni ombi letu kwamba utachunguza kuhusu majina haya kwa bidii kama ilivyo ahadi ya kwamba nyakati za mwisho mataifa watamjua Elohim. Isaya 52:6-9; Zaburi 69:35,36; Zaburi 91:14; Yohana 17:6; Yohana 5:43

# Yaliyomo

UTANGULIZI ....................................................... iv
KUHUSU MAJINA ....................................................... v
JINSI YA KUSOMA BIBLIA ....................................................... viii
SEHEMU YA KWANZA ....................................................... 11
AMRI KUMI ....................................................... 11
UTANGULIZI WA AMRI KUMI ....................................................... 12
AMRI YA KWANZA ....................................................... 12
AMRI YA PILI ....................................................... 15
AMRI YA TATU ....................................................... 18
AMRI YA NNE ....................................................... 20
AMRI YA TANO ....................................................... 22
AMRI YA SITA ....................................................... 24
AMRI YA SABA ....................................................... 27
AMRI YA NANE ....................................................... 28
AMRI YA TISA ....................................................... 31
AMRI YA KUMI ....................................................... 34
SEHEMU YA PILI ....................................................... 37
MANABII NA IMANI YA YAHSHUAH ....................................................... 37
UTANGULIZI WA SEHEMU YA PILI ....................................................... 38
CHEMICHEMI ....................................................... 38
UBATIZO ....................................................... 41
TUMAINI LA WATAKATIFU ....................................................... 43
MLIMA WA MORIA ....................................................... 45
KUFA NA KUFUFUKA KWA YAHSHUA ....................................................... 48
SIKUKUU YA 'GOOD FRIDAY NA EASTER SUNDAY' ....................................................... 50
WATU WA MATAIFA HUPANDIKIZWA VIPI ....................................................... 52
BINTI ZAYUNI ....................................................... 55
FALME NNE; MWANAUME WA CHUMA ....................................................... 58
MAONO YA DANIELI SURA YA SABA ....................................................... 61
MNYAMA WA PILI - 538 BC ....................................................... 65

MNYAMA WA TATU 333BC ........ 68
MNYAMA WA NNE ........ 69
PEMBE NDOGO ........ 72
JERAHA LA MAUTI LILILOPONA ........ 76
SEHEMU YA TATU ........ 82
MWONGOZO WA BIBLIA KATIKA MAISHA........ 82
UTANGULIZI WA SEHEMU YA TATU ........ 83
MAOMBI ........ 83
CHAKULA........ 85
ULEVI........ 90
MAVAZI ........ 93
JUKUMU LA MZAZI........ 95

# JINSI YA KUSOMA BIBLIA

Utangulizi: Leo hii kuna imani nyingi sana duniani zinazotokana na kusoma na kutafsiri Biblia. Kila anayesoma hutafsiri kwa mtazamo wake. Biblia yenyewe imeandikwa jinsi inavyopaswa kusomwa na kutafsiriwa.

1. **Biblia inasema watu hupotea kwa nini?**

Mithali 2:3-6 - Naam, ukiita busara, Na kupaza sauti yako upate ufahamu; Ukiutafuta kama fedha, Na kuutafutia kama hazina iliyositirika; Ndipo utakapofahamu kumcha BWANA, Na kupata kumjua Elohim. Kwa kuwa BWANA huwapa watu hekima; Kinywani mwake hutoka maarifa na ufahamu.

2. **Ukweli kamilifu wa mada yoyote hupatikana vipi katika maandiko?**

Isaya 28:10 - Kwa maana ni amri juu ya amri, amri juu ya amri; kanuni juu ya kanuni, kanuni juu ya kanuni; huku kidogo na huku kidogo.

Isaya 28:13 - Kwa sababu hiyo neno la BWANA kwao litakuwa hivi, amri juu ya amri, amri juu ya amri; kanuni juu ya kanuni, kanuni juu ya kanuni; huku kidogo na huku kidogo; ili waende na kuanguka nyuma, na kuvunjwa, na kunaswa, na kuchukuliwa.

Maelezo - Kulingana na andiko hili, hakuna mada yoyote inayoweza kupatikana kwa kusoma Biblia kama riwaya au vitabu vingine vya historia. Ni andiko moja hapa na lingine pale ili upate ufahamu kamili.

3. **Mwokozi wetu alisema tutajua kumhusu tukifanya nini?**

Yohana 5:39 - Mwayachunguza maandiko, kwa sababu mnadhani kwamba ninyi mna uzima wa milele ndani yake; na hayo ndiyo yanayonishuhudia.

Maelezo - Wakati Mwokozi alisema haya, Agano Jipya halikuwa limeandikwa.

4. **Je, Mwokozi alisema kuwa Musa aliandika kumhusu?**

Yohana 5:46 - Kwa maana kama mngalimwamini Musa, mngeniamini mimi; kwa sababu yeye aliandika habari zangu.

5. **Kuna mfano wa manabii wengine walioandika kuhusu Mwokozi?**

Nehemia 8:8 - Nao wakasoma katika kitabu, katika torati ya Elohim, kwa sauti ya kusikilika; wakaeleza maana yake, hata wakayafahamu yaliyosomwa.

Zaburi 2:6-7 - Nami nimemweka mfalme wangu Juu ya Sayuni, mlima wangu mtakatifu. Nitaihubiri amri; ELOHIM aliniambia, Ndiwe mwanangu, Mimi leo nimekuzaa.

6. **Mtume Paulo anatuagiza vipi kuhusu kusoma neno?**

2 Timotheo 2:15, na tutaisoma vipi? (Msomaji anashauriwa kutumia Biblia ya King James ili aweze kupata maana kamili ya andiko hili).

2 Timotheo 2:15 - Jitahidi kujionyesha kuwa umekubaliwa na Elohim, mtenda kazi asiye na sababu ya kutahayari, ukitumia kwa halali neno la kweli.

*Study to shew thyself approved unto Elohim, a workman that needeth not to be ashamed, rightly dividing the word of truth.*

Maelezo - Paulo alituhimiza tujifunze kwa bidii na kwa usahihi ili kuhakikisha kwamba tunaelewa maandiko vizuri na kwa usahihi.

7. **Kutakuwa na faida gani kwetu tukisoma Biblia inavyostahili kulingana na Mwokozi?**

Yohana 8:32 - Tena mtaifahamu kweli, nayo hiyo kweli itawaweka huru.

8. **Mtu anaweza kuwa na tafsiri yake mwenyewe?**

2 Petro 1:21 - Maana unabii haukuletwa po pote kwa mapenzi ya mwanadamu; bali wanadamu walinena yaliyotoka kwa Elohim, wakiongozwa na Roho Mtakatifu.

2 Petro 1:20 - Mkijua neno hili kwanza, ya kwamba hakuna unabii katika maandiko upatao kufasiriwa kama apendavyo mtu fulani tu.

2 Timotheo 3:16 - Kila andiko, lenye pumzi ya Elohim, lafaa kwa mafundisho, na kwa kuwaonya watu makosa yao, na kwa kuwaongoza, na kwa kuwaadibisha katika haki.

9. **Mwongozo huu wa kusoma Biblia hupatikana wapi?**

Yakobo 1:5 - Lakini mtu wa kwenu akipungukiwa na hekima, na aombe dua kwa Elohim, awapaye wote, kwa ukarimu, wala hakemei; naye atapewa.

10. **Ni kielelezo kipi kizuri cha kuyachunguza maandiko? Matendo ya Mitume 17:10-12, Warumi 4:3 (sehemu ya kwanza)**

Matendo ya Mitume 17:10-12 - Mara hao ndugu wakawapeleka Paulo na Sila usiku hata Beroya. Nao walipofika huko wakaingia katika sinagogi la Wayahudi.

Watu hawa walikuwa waungwana kuliko wale wa Thesalonike, kwa kuwa walilipokea lile neno kwa uelekevu wa moyo, wakayachunguza maandiko kila siku, waone kwamba mambo hayo ndivyo yalivyo. Basi watu wengi miongoni mwao wakaamini, na wanawake wa Kiyunani wenye cheo, na wanaume si wachache.

Warumi 4:3 - (Sehemu ya kwanza) Maana maandiko yasemaje?

Luka 10:25-26 - Na tazama, mwana-sheria mmoja alisimama amjaribu; akisema, Mwalimu, nifanye nini ili niurithi uzima wa milele? Akamwambia, Imeandikwa nini katika torati? Wasomaje?

Hitimisho - Katika kusoma mada fulani, mtu anapaswa kufafanuliwa zaidi kuihusu katika Biblia kama jinsi hiyo mada imenakiliwa na waandishi tofauti tofauti. (2 Wakorintho 13:1 - Hii ndiyo mara ya tatu ya mimi kuja kwenu. Kwa vinywa vya mashahidi wawili au watatu kila neno litathibitishwa.)

# SEHEMU YA KWANZA

# AMRI KUMI



# UTANGULIZI WA AMRI KUMI

Amri Kumi ni miongoni mwa sehemu za Biblia zinazoheshimika na kutambuliwa sana. Zinapatikana katika Kutoka 20:1-17 na Kumbukumbu la Torati 5:6-21, na zinaunda msingi wa agano la Elohim na mwanadamu, zikiweka kanuni za mwenendo wa maadili na kujitolea kiroho. Amri hizi ni kanuni zisizopitwa na wakati, za kudumu milele, na zinaunda mfumo wa kimaadili sio tu kwa Israeli ya kale bali pia kwa wale wote wanaotafuta na kufuata mapenzi ya Elohim.

Katika kijitabu hiki, tutachunguza kila moja ya Amri Kumi katika muktadha wa Kutoka na Kumbukumbu la Torati, huku pia tukizingatia maana zake za ndani zaidi kama zilivyochunguzwa katika Maandiko mengine. Agano la Kale linatoa maarifa mazuri juu ya asili ya sheria ya Elohim, wakati Agano Jipya linaonyesha jinsi Yahshua Masihi alivyotimiza na kupanua amri hizi katika mafundisho yake.

Kwa mfano, Yahshua alifafanua sheria katika amri kuu mbili: kumpenda Elohim na kumpenda jirani yako (Mathayo 22:37-40), akionyesha kwamba Amri Kumi si kanuni za kutiiwa tu bali ni kanuni za upendo na kujitolea. Kupitia kujifunza kwa makini Biblia, tutaona jinsi kila amri inavyofafanua moyo wa Elohim na jinsi, katika Yahshua, waamini wanaitwa kuzishika kanuni hizi katika uwezo wa Roho Mtakatifu.

Unaposoma somo hili, twaomba upate kuthamini zaidi Amri Kumi na kuelewa nguvu zake za kubadilisha na kuongoza maisha ya kila mwamini leo.

## AMRI YA KWANZA

1. **Amri ya kwanza inatuonya vipi?**

Kutoka 20:1-3

Elohim akanena maneno haya yote akisema, Mimi ni BWANA, Elohim wako, niliyekutoa katika nchi ya Misri, katika nyumba ya utumwa. Usiwe na miungu mingine ila mimi.

Yoshua 24:23

Akasema, Basi sasa, iondoeni miungu migeni iliyo kati yenu, mkaielekeze mioyo yenu kwa BWANA, Elohim wa Israeli.

2. **Je, miungu ni wengi wanaoabudiwa na mataifa?**

Yoshua 24:2

Yoshua akawaambia watu wote, BWANA, Elohim wa Israeli, asema hivi, Baba zenu hapo zamani walikaa ng'ambo ya Mto, maana Tera, baba yake Ibrahimu, naye ni baba yake Nahori; wakaitumikia miungu mingine.

1 Wakorintho 8:5

Kwa maana ijapokuwa wako waitwao miungu, ama mbinguni ama duniani, kama vile walivyoko miungu mingi na mabwana wengi.

Yeremia 2:10-11

Maana, vukeni mpaka visiwa vya Kitimu, mkaone; tumeni watu waende Kedari, mkafikiri sana; mkaone kwamba jambo kama hili limekuwa wakati wo wote. Je, taifa wamebadili miungu yao, ingawa siyo miungu? Lakini watu wangu wameubadili utukufu wao kwa ajili ya kitu kisichofaidia.

3. **Je, Elohim ni wengi au ni mmoja?**

Kumbukumbu la Torati 4:4-5

Bali ninyi mlioambatana na BWANA, Elohim wenu, mnaishi kila mmoja wenu, hata leo. Angalieni nimewafundisha amri na hukumu, vile vile kama BWANA, Elohim wangu, alivyoniamuru, ili mzitende katika nchi mwingiayo ili kuimiliki.

Kumbukumbu la Torati 32:39

Fahamu sasa ya kuwa Mimi, naam, Mimi ndiye, Wala hapana Elohim mwingine ila Mimi; Naua Mimi, nahuisha Mimi, Nimejeruhi, tena naponya; Wala hapana awezaye kuokoa katika mkono wangu.

4. **Wana wa Israeli walionywa vipi kuhusu miungu ya watu mataifa?**

Zaburi 81:8-9

Enyi watu wangu, sikieni, nami nitawaonya, Ee Israeli, kama ukitaka kunisikiliza; Usiwe na Elohim mgeni ndani yako; Wala usimsujudie Elohim mwingine.

Kumbukumbu la Torati 12:30

Ujiangalie, usije ukanaswa ukawafuata, wakiisha kuangamizwa mbele yako; wala usije ukauliza habari za miungu yao, ukisema, Mataifa haya waitumikiaje miungu yao? Nami nifanye vivyo.

5. **Maandiko yametuonya vipi kuhusu kuitegemea miungu mingine ijapokuwa iko na uwezo?**

Kumbukumbu la Torati 13:1-4

Kukizuka katikati yako nabii, au mwotaji wa ndoto, akikutolea ishara au ajabu, ikatukia hiyo ishara au hiyo ajabu aliyokuambia akisema, Na tuifuate miungu mingine usiyoijua, tuitumikie hiyo; wewe usiyasikize maneno ya nabii yule, au yule mwotaji wa ndoto, kwa kuwa BWANA, Elohim wenu, yuawajaribu, apate kujua kwamba mwampenda BWANA, Elohim wenu, kwa mioyo yenu yote na roho zenu zote. Tembeeni kwa kumfuata BWANA, Elohim wenu; mcheni na kushika maagizo yake na kuisikia sauti yake, nanyi mtumikieni na kushikamana naye.

Kumbukumbu la Torati 13:6

Atakapokushawishi kwa siri ndugu yako, mwana wa mama yako, au mwana wako, au binti yako, au mke wa kifuani mwako, au rafiki yako aliye kama moyo wako, akikuambia, Twende tukaabudu miungu mingine usiyoijua wewe wala baba zako.

6. **Watu wa mataifa siku hizi wanaabudu hata mizimu (WAFU). Je, jambo hilo ni chukizo machoni pa Elohim?**

Isaya 28:15

Kwa sababu mmesema, Tumefanya agano na mauti, tumepatana na kuzimu; pigo lifurikalo litakapopita, halitatufikia sisi; kwa maana tumefanya maneno ya uongo kuwa kimbilio letu, tumejificha chini ya maneno yasiyo kweli.

Zaburi 106:28-29

Wakajiambatiza na Baal-Peori, Wakazila dhabihu za wafu. Wakamkasirisha kwa matendo yao; Tauni ikawashambulia.

7. **Je, wafu kuna jambo ambalo wanaweza kutenda; kulaani au kubariki?**

Mhubiri 9:5-6

Kwa sababu walio hai wanajua ya kwamba watakufa; lakini wafu hawajui neno lo lote, wala hawana ijara tena; maana kumbukumbu lao limesahauliwa. Mapenzi yao na machukio yao, na husuda yao, imepotea yote pamoja; wala hawana sehemu tena katika jambo lo lote lililofanyika chini ya jua.

8. **Je, Elohim ni Elohim wa walio hai au wafu?**

Ayubu 14:11-12

Kama vile maji kupwa katika bahari, Na mto kupunguka na kukatika; Ni vivyo mwanadamu hulala chini, asiinuke; Hata wakati wa mbingu kutokuwako tena, hawataamka, Wala kuamshwa usingizini.

Marko 12:27

Yeye si Elohim wa wafu, bali wa walio hai. Hivyo mwapotea sana.

9. **Ni juhudi gani ambayo mtu anapaswa kufanya kwa bidii ili amjue Elohim?**

Yeremia 12:16

Kisha itakuwa, ikiwa watajifunza kwa bidii njia za watu wangu, kuapa kwa jina langu, Kama BWANA aishivyo, vile vile kama walivyowafundisha watu wangu kuapa kwa Baali, ndipo watakapojengwa kati ya watu wangu.

Maelezo - Amri ya Kwanza inatufundisha kumpa Elohim mmoja wa kweli utukufu wote, tukimpenda na kumtegemea kwa moyo, akili, na roho, huku tukikwepa miungu mingine, mizimu, na desturi zinazotutenganisha naye.

## AMRI YA PILI

1. **Amri ya pili inatuonya dhidi ya nini?**

Kutoka 20:4-6

Usijifanyie sanamu ya kuchonga, wala mfano wa kitu chochote kilicho juu mbinguni, wala kilicho chini duniani, wala kilicho majini chini ya dunia. Usivisujudie wala kuvitumikia; kwa kuwa mimi, BWANA, Elohim wako, ni Elohim mwenye wivu; nawapatiliza wana maovu ya baba zao, hata kizazi cha tatu na cha nne cha wanichukiao, nami nawarehemu maelfu elfu wanipendao, na kuzishika amri zangu.

2. **Kwa nini tunaambiwa tusifanye sanamu wala kuwa na mfano wa kitu chochote?**

Kumbukumbu la Torati 4:15

Jihadharini nafsi zenu basi; maana hamkuona umbo la namna yoyote siku ile BWANA aliyosema nanyi kutoka kati ya moto.

3. **Je! Elohim mtamsawazisha na nani?**

Isaya 46:5

Mtanifananisha na nani, na kunisawazisha naye, na kunilinganisha naye, ili tuwe sawasawa?

4. **Ni kwa nini hatuwezi kumlinganisha Elohim na chochote?**

2 Wakorintho 3:17 - Basi Bwana ndiye Roho; walakini alipo Roho wa Bwana, hapo ndipo penye uhuru.

Isaya 42:8 - Mimi ni BWANA; ndilo jina langu; na utukufu wangu sitampa mwingine, wala sitawapa sanamu sifa zangu.

5. **Ikiwa ni hivyo kwamba Elohim ni roho, wale wanaomwabudu wanafaa kumwabudu vipi?**

Yohana 4:24 - Elohim ni Roho, nao wamwabuduo yeye imewapasa kumwabudu katika roho na kweli.

Maelezo - Biblia inatufundisha kwamba Elohim ni roho, hivyo tunapomwabudu tunafaa kujua na kuamini kuwa yupo na huwapa thawabu wale wamtafutao. (Waebrania 11:1, Basi imani ni kuwa na hakika ya mambo yatarajiwayo, ni bayana ya mambo yasiyoonekana.)

6. **Je! Watu wa nyakati zetu wanajifanyia sanamu na kuziabudu?**

Isaya 46:6 - Watu wamwagao dhahabu kutoka mfukoni, na kupima fedha katika mizani, huajiri mfua dhahabu, akaifanya Elohim; huanguka, naam, huabudu.

7. **Je! Sanamu hutengenezwa kutumia nini?**

Isaya 44:13-20

Seremala hunyosha uzi; huiandika kwa kalamu ya mate; huitengeneza kwa randa, huiandika kwa bikari, huifanza kwa mfano wa mwanadamu, sawasawa na uzuri wa mwanadamu, ili ikae nyumbani. Yeye hujikatia mierezi, hutwaa mtiriza, na mwaloni, hujichagulia mti mmoja katika miti ya msituni; hupanda mvinje, mvua ikausitawisha. Kisha utamfaa mwanadamu kwa kuni; hutwaa kipande, akaota moto; naam, huuwasha moto, akaoka mkate; naam, huufanya Elohim, akauabudu;

huifanya sanamu ya kuchonga, akaisujudia. Sehemu moja huiteketeza; kwa sehemu nyingine hula nyama; huoka chakula kiokwacho, akashiba; naam, huota moto, akasema, Aha, nimeota moto, nimeona moto; na kwa sehemu iliyobakia hufanya Elohim, yaani, sanamu yake ya kuchonga; husujudu mbele yake akaiabudu, akaiomba, akasema, Uniokoe; maana wewe u Elohim wangu. Hawajui wala hawafikiri; maana amewafumba macho, wasione, na mioyo yao, wasiweze kufahamu. Wala hapana atiaye moyoni, wala hapana maarifa, wala fahamu kusema, Nimeteketeza sehemu motoni, naam, pia nimeoka mkate juu ya makaa yake; nimeoka nyama nikaila; nami, je! Kilichobaki nikifanye kuwa chukizo? Je! Nisujudie shina la mti? Hula majivu; moyo uliodanganyika umempotosha, asiweze kuiokoa nafsi yake, wala kusema, Je! Sio uongo mkononi mwangu?

8. **Je! Sanamu zina faida yoyote na je zinaweza kumsaidia anayeabudu kwa njia yoyote?**

Zaburi 115:4-8

Sanamu zao ni fedha na dhahabu, Kazi ya mikono ya wanadamu. Zina vinywa lakini hazisemi, Zina macho lakini hazioni, Zina masikio lakini hazisikii, Zina pua lakini hazisikii harufu, Mikono lakini hazishiki, miguu lakini haziendi, Wala hazitoi sauti kwa koo zake. Wazifanyao watafanana nazo, Kila mmoja anayezitumainia.

Habakuki 2:18-19 - Sanamu ya kuchora yafaa nini, hata yeye aliyeifanya ameichora? Sanamu ya kuyeyuka, nayo ni mwalimu wa uongo, yafaa nini, hata yeye aliyeifanya aiwekee tumaini lake, na kufanya sanamu zisizoweza kusema? Ole wake yeye auambiaye mti, Amka; aliambiaye jiwe lisiloweza kusema, Ondoka! Je! Kitu hicho kitafundisha? Tazama, kimefunikwa kwa dhahabu na fedha, wala hamna pumzi ndani yake kabisa.12:14

9. **Uchungu wa Paulo ulikuwa upi alipopata mji wa Athene umejaa sanamu?**

Matendo ya Mitume 17:16 - Paulo alipokuwa akiwangojea huko Athene na kuona jinsi mji ule ulivyojaa sanamu, roho yake ilichukizwa sana ndani yake.

10. **Je! Paulo alijitahidi vipi kuzigeuza nia zao?**

Matendo ya Mitume 19:26-27

Tena mnaona na kusikia ya kwamba si katika Efeso tu, bali katika Asia yote pia Paulo huyo ameshawishi watu wengi na kuwageuza nia zao, akisema ya kwamba hiyo inayofanywa kwa mikono siyo miungu. Si kwamba kazi hii yetu ina hatari ya kudharauliwa tu; bali na hekalu la Elohim mke aliye mkuu, Artemi, kuhesabiwa si kitu, na kuondolewa utukufu wake, ambaye Asia yote pia na walimwengu wote humwabudu.

**11.Je! Kuna Elohim mwingine?**

Isaya 45:5-6

Mimi ni BWANA, wala hapana mwingine; zaidi yangu mimi hapana Elohim; nitakufunga mshipi ijapokuwa hukunijua; ili wapate kujua toka maawio ya jua, na toka magharibi, ya kuwa hapana mwingine zaidi ya mimi; Mimi ni BWANA, wala hapana mwingine.

**12.Maandiko Matakatifu yatushauri vipi kwa kujiepusha na sanamu?**

1 Yohana 5:21

Watoto wadogo, jilindeni nafsi zenu na sanamu.

Maelezo - Elohim ni Roho na kweli na ni wa kipekee, hivyo tunapaswa kumwabudu kwa roho na kweli, tukijiepusha na sanamu ambazo hazina uhai wala faida.

## AMRI YA TATU

**1. Amri ya tatu inaonya dhidi ya nini?**

Kutoka 20:7

Usilitaje bure jina la BWANA, Elohim wako, maana BWANA hatamhesabia kuwa hana hatia mtu alitajaye jina lake bure.

**2. Kwa nini maandiko yanatuonya tusilitaje jina la Baba yetu bure?**

Zaburi 111:9 - Amewapelekea watu wake ukombozi, Ameamuru agano lake liwe la milele, Jina lake ni takatifu la kuogopwa.

**3. Je, Yahshua alidhihirisha ukweli huu?**

Mathayo 6:9 - Basi ninyi salini hivi; Baba yetu uliye mbinguni, Jina lako litukuzwe, Ufalme wako uje.

**4. Je, watu wa kale walikuwa wameonywa vipi dhidi ya kutolitumia jina la Elohim bure?**

Mambo ya Walawi 19:12 - Msiape uongo kwa jina langu, hata ukalinajisi jina la Elohim wako; Mimi ndimi BWANA.

**5. Kulijua jina la Elohim na kulitunza kwa kutolitaja bure kunawaletea wanadamu faida gani kuu?**

Zaburi 91:14 - Kwa kuwa amekaza kunipenda, Nitamwokoa; na kumweka palipo juu, Kwa kuwa amenijua Jina langu.

**6. Na je, uzima wa milele unapatikana kwa njia ipi?**

Yohana 17:3 - Na uzima wa milele ndio huu, Wakujue wewe, Elohim wa pekee wa kweli, na Yahshua Masihi uliyemtuma.

**7. Biblia inatuuliza swali gani nzito kuhusiana na jina la Baba yetu na la Mwanawe?**

Mithali 30:4 - Ni nani aliyepanda mbinguni na kushuka chini? Ni nani aliyekamata upepo kwa makonzi yake? Ni nani aliyeyafunga maji ndani ya nguo yake? Ni nani aliyefanya imara ncha zote za nchi? Jina lake ni nani? Na ni nani jina la mwanawe, kama wajua?

**8. Je, Biblia inajibu swali hili?**

Zaburi 68:4 - Mwimbieni Elohim, lisifuni jina lake, Mtengenezeeni njia ya barabara, Apitaye majangwani kama mpanda farasi; Jina lake ni ....; shangilieni mbele zake.

**9. Kwa ajili ya kuliheshimu jina lililotukufu la Baba yetu wa mbinguni, Mwanawe alitumia jina gani mbadala alipokuwa alimwita Baba yake Elohim, na ana swali gani kwa makuhani na kwa wote wanaolidhalau jina lake?**

Malaki 1:6 - Mwana humheshimu baba yake, na mtumishi humcha bwana wake; basi, kama mimi ni baba yenu, heshima yangu iko wapi? Na kama mimi ni bwana wenu, kicho changu ki wapi? BWANA wa majeshi awauliza ninyi, enyi makuhani, mnaolidharau jina langu. Nanyi mwasema, Tumelidharau jina lako kwa jinsi gani?

Yohana 5:43 - Mimi nimekuja kwa jina la Baba yangu, wala ninyi hamnipokei; mwingine akija kwa jina lake mwenyewe, mtampokea huyo.

**10.Nabii Sefania alisema ni nini kitakachotukia kwa wote wanaolitaja jina la Elohim huku wakimwabudu pamoja na miungu na jeshi la mbinguni?**

Sefania 1:1-5 - Neno la BWANA lililomjia Sefania, mwana wa Kushi, mwana wa Gedalia, mwana wa Amaria, mwana wa Hezekia; katika siku za Yosia, mwana wa Amoni, mfalme wa Yuda. Nitavikomesha kabisa vitu vyote, visionekane juu ya uso wa nchi, asema BWANA. Nitavikomesha mwanadamu na mnyama; nitakomesha ndege wa angani, na samaki wa baharini, na hayo makwazo pamoja na wabaya; nami nitamkatilia mbali mwanadamu, asionekane juu ya uso wa nchi, asema BWANA. Nami nitaunyosha mkono wangu juu ya Yuda, na juu ya watu wote wakaao Yerusalemu; nami nitayakatilia mbali mabaki ya Baali, yasionekane mahali hapa, na hilo jina la Wakemari pamoja na makuhani; na wale walisujudiao jeshi la mbinguni juu ya dari za nyumba; na hao waabuduo, waapao kwa BWANA na kuapa pia kwa Malkamu.

Maelezo - Amri ya Tatu inahimiza heshima, ibada ya kweli, na utakatifu wa jina la Elohim, kwani ni msingi wa mahusiano ya dhati na Elohim na njia ya uzima wa milele. Wale wanaozingatia maonyo haya wanaahidiwa wokovu na baraka, lakini wanaokosa kutii wanakabiliwa na hukumu.

## AMRI YA NNE

1. **Amri hii inatuagiza aje?**

Kutoka 20:8 - Ikumbuke siku ya Sabato uitakase.

2. **Nani hufaidika na pumziko hili?**

Mariko 2:27 - Akawaambia, Sabato ilifanyika kwa ajili ya mwanadamu, si mwanadamu kwa ajili ya sabato.

3. **Ni faida gani iko kwa hii siku?**

Mwanzo 2:3 - Elohim akaibarikia siku ya saba, akaitakasa kwa sababu katika siku hiyo Elohim alistarehe, akaacha kufanya kazi yake yote aliyoiumba na kuifanya.

Isaya 58:13-14 - Kama ukigeuza mguu wako usihalifu sabato, usifanye anasa yako siku ya utakatifu wangu; ukiita sabato siku ya furaha, na siku takatifu ya Bwana yenye heshima; ukiitukuza, kwa kutokuzifanya njia zako mwenyewe, wala kuyatafuta yakupendezayo, wala kusema maneno yako mwenyewe; ndipo

utakapojifurahisha katika Bwana; nami nitakupandisha mahali pa nchi palipoinuka; nitakulisha urithi wa Yakobo baba yako; kwa maana kinywa cha Bwana kimenena hayo.

4. **Sabato ni siku gani katika mpangilio wa juma na ni ya nani?**

Kutoka 20:10 - lakini siku ya saba ni Sabato ya Bwana, Elohim wako, siku hiyo usifanye kazi yo yote, wewe, wala mwana wako, wala binti yako, wala mtumwa wako, wala mjakazi wako, wala mnyama wako wa kufuga, wala mgeni aliye ndani ya malango yako.

Mathayo 28:1 - Hata sabato ilipokwisha, ikipambazuka siku ya kwanza ya juma, Mariamu Magdalene, na Mariamu yule wa pili, walikwenda kulitazama kaburi.

5. **Siku hii huanza saa gapi?**

Mambo ya Walawi 23:32 (sehemu ya mwisho) - tangu jioni hata jioni, mtaishika hiyo Sabato yenu.

Nehemia 13:19 - Ikawa malango ya Yerusalemu yalipoanza kuwa na giza kabla ya sabato, naliamuru milango ifungwe, nikaamuru isifunguliwe hata sabato iishe; na baadhi ya watumishi wangu nikawaweka juu ya malango, ili usiingizwe mzigo wo wote siku ya sabato.

6. **Sabato ilikuwa itunzwe kwa muda upi?**

Kutoka 31:16 - Kwa ajili ya hayo wana wa Israeli wataishika Sabato, kuiangalia sana hiyo Sabato katika vizazi vyao vyote, ni agano la milele.

Mathayo 5:18 - Kwa maana, amin, nawaambia, Mpaka mbingu na nchi zitakapoondoka, yodi moja wala nukta moja ya torati haitaoondoka, hata yote yatimie.

7. **Watu wa Mataifa wanastahili pia kutunza sabato?**

Isaya 56:6-7 - Na wageni, walioandamana na Bwana ili wamhudumu, na kulipenda jina la Bwana, kuwa watumishi wake; kila aishikaye sabato asiivunje, na kulishika sana agano langu; Nitawaleta hao nao hata mlima wangu mtakatifu, na kuwafurahisha katika nyumba yangu ya sala; makafara yao na dhabihu zao zitakubaliwa juu ya madhabahu zangu; kwa maana nyumba yangu itaitwa nyumba ya sala kwa mataifa yote.

8. **Masihi alitumia siku ya sabato aje? Je, na Paulo?**

Luka 4:16 - Akaenda Nazareti, hapo alipolelewa; na siku ya sabato akaingia katika sinagogi kama ilivyokuwa desturi yake, akasimama ili asome.

Matendo ya Mitume 17:2 - Na Paulo, kama ilivyokuwa desturi yake, akaingia mle walimo, akahojiana nao kwa maneno ya maandiko sabato tatu.

9. **Watu wa Elohim wamebakishiwa siku ya kustarehe?**

Waebrania 4:9 - Basi, imesalia raha ya sabato kwa watu wa Elohim.

Maelezo - Amri hii ya Sabato ni agizo takatifu lililowekwa na Elohim tangu uumbaji, likilenga kutoa pumziko, baraka, na nafasi ya ushirika wa kiroho na Muumba. Siku ya saba, ambayo ni Sabato, imebarikiwa na kutakaswa, na inapaswa kutunzwa na watu wote kama agano la milele. Heshima ya Sabato inahusisha kuepuka shughuli za kawaida, kuitumia kumtukuza Elohim, na kufurahia uwepo wake. Yahshua na mitume waliithamini siku hii, wakitumia kwa ibada na mafundisho. Kwa mujibu wa maandiko, Sabato huanza jioni na hudumu hadi jioni ya siku inayofuata, ikiwa ni ishara ya utii na uhusiano wa karibu kati ya mwanadamu na Muumba.

## AMRI YA TANO

1. **Amri hii ilitolewa na nani na inasemaje?**

Kutoka 20:1-2,12 - Elohim akanena maneno haya yote akasema, Mimi ni BWANA, Elohim wako, niliyekutoa katika nchi ya Misri, katika nyumba ya utumwa. Waheshimu baba yako na mama yako; siku zako zipate kuwa nyingi katika nchi upewayo na BWANA, Elohim wako.

2. **Wakati watoto wanaheshimu wazazi, Bwana wetu hufurahia. Je, amewaahidi hao watoto nini?**

Wakolosai 3:20 - Ninyi watoto, watiini wazazi wenu katika mambo yote; maana jambo hili lapendeza katika Bwana.

Waefeso 6:1-3 - Enyi watoto, watiini wazazi wenu katika Bwana, maana hii ndiyo haki. Waheshimu baba yako na mama yako; amri hii ndiyo amri ya kwanza yenye ahadi, Upate heri, ukae siku nyingi katika dunia.

Maelezo - Ikiwa kuheshimu wazazi kunapelekea mtu kuwa na heri na siku nyingi, basi ni bayana kutotii kutafanya siku za mtu za kuishi kuwa chache.

3. **Mtoto mtiifu huonekana vipi machoni mwa Elohim?**

Mhubiri 4:13 - Heri kijana maskini mwenye hekima Kuliko mfalme mzee mpumbavu,ambaye hajui tena kupokea maonyo.

Mithali 12:1 - Kila apendaye mafundisho hupenda maarifa; Bali yeye achukiaye kulaumiwa ni kama mnyama.

4. **Mzazi anastahili kuheshimiwa mpaka lini?**

Mithali 23:22 - Msikilize baba yako aliyekuzaa, Wala usimdharau mama yako akiwa mzee.

5. **Kwa mujibu wa Mithali 30:11 (Kuna kizazi cha watu wamlaanio baba yao; Wala hawambariki mama yao), adhabu ya kutotii mzazi ni ipi?**

Mithali 30:17 - Jicho la mtu amdhihakiye babaye, Na kudharau kumtii mamaye; Kunguru wa bondeni wataling'oa, Na vifaranga vya tai watalila.

6. **Wana wa Israeli waliamriwaje kuhusu mtoto asiyetii wazazi wake?**

Kumbukumbu la Torati 21:18-21 - Mtu akiwa na mwana mkaidi, mshupavu, asiyetii sauti ya baba yake, wala sauti ya mama yake, nao wajapomwadhibu hawasikizi, ndipo babaye na mamaye wamkamate, na kumpeleka kwa wazee wa mji wake, katika lango la mahali pake; wawaambie wazee wa mji wake, Huyu mwana wetu ni mkaidi, mshupavu, hasikizi sauti yetu; ni mwasherati, tena ni mlevi. Waume wote wa mji wake na wamtupie mawe, afe; ndivyo utakavyoondoa uovu katikati yako; na Israeli wote watasikia na kuogopa.

Mithali 20:20 - Amlaaniye babaye au mamaye, Taa yake itazimika katika giza kuu.

Maelezo - Wakati mwingi watoto wakiwa watu wazima wanakosa kuwaheshimu wazazi lakini kulingana na hayo maandiko, mzazi anastahili kuheshimiwa na mtoto siku zote mpaka kufa.

7. **Je, mtoto ameonywa dhidi ya kumpiga au kumtusi mzazi?**

Kutoka 21:15,17 - Ampigaye baba yake au mama yake, sharti atauawa. Yeye amwapizaye baba yake au mama yake, sharti atauawa.

8. **Walio wa rika moja na wazazi wako wanastahili kuheshimiwa. Je, kuna mfano wa maafa kwa kutotii hayo maagizo?**

2 Wafalme 2:23-24 - Akakwea kutoka huko mpaka Betheli; naye alipokuwa akienda njiani, wakatoka vijana katika mji, wakamfanyizia mzaha, wakamwambia, Paa wewe mwenye upaa! Paa wewe mwenye upaa! Akatazama nyuma akawaona, akawalaani kwa jina la BWANA. Wakatoka dubu wawili wa kike mwituni, wakawararua vijana arobaini na wawili miongoni mwao.

1 Timotheo 5:1 - Mzee usimkemee, bali umwonye kama baba; na vijana kama ndugu.

9. **Tunapoambiwa siku za mwisho ni za hatari, je watoto wengi wataendelea kutii ama kutotii wazazi?**

2 Timotheo 3:1-2 - Lakini ufahamu neno hili, ya kuwa siku za mwisho kutakuwako nyakati za hatari. Maana watu watakuwa wenye kujipenda wenyewe, wenye kupenda fedha, wenye kujisifu, wenye kiburi, wenye kutukana, wasiotii wazazi wao, wasio na shukrani, wasio safi.

10. **Ikiwa kuna mtoto amekosea mzazi wake, moyo wake unastahili kuwa vipi ili waweze kurudiana na mzazi, na je, jambo hilo huleta furaha?**

Luka 15:17-18 - Alipozingatia moyoni mwake, alisema, Ni watumishi wangapi wa baba yangu wanaokula chakula na kusaza, na mimi hapa ninakufa kwa njaa. Nitaondoka, nitakwenda kwa baba yangu na kumwambia, Baba, nimekosa juu ya mbingu na mbele yako.

Maelezo - Amri ya tano ni msingi wa uhusiano wa familia na jamii. Utiifu na heshima kwa wazazi ni agizo la moja kwa moja kutoka kwa Elohim, linaloleta baraka na maisha marefu. Kutotii wazazi kunavunja utaratibu wa Elohim na huleta hukumu kali. Elohim anataka mahusiano ya familia yanayozingatia heshima, upendo, na toba ili kudumisha amani na furaha ya kweli.

## AMRI YA SITA

1. **Je, ni nani alitoa amri hii?**

Kutoka 20:1-2 - Elohim akanena maneno haya yote akisema, Mimi ni BWANA, Elohim wako, niliyekutoa katika nchi ya Misri, katika nyumba ya utumwa.

2. **Mtu atahesabiwa kuwa muuaji wakati gani?**

Hesabu 35:16-18 - Lakini kama alimpiga kwa chombo cha chuma, akafa, ni muuaji huyo; muuaji hakika yake atauawa. Na kama alimpiga kwa jiwe lililokuwa mkononi mwake, ambalo kwa hilo humkini mtu kufa, naye akafa, yeye ni muuaji; huyo muuaji lazima atauawa. Au kama alimpiga kwa chombo cha mti kilichokuwa mkononi mwake ambacho kwa hicho humkini mtu kufa, naye akafa, ni muuaji huyo, muuaji lazima atauawa.

3. **Kuna sababu yoyote ya mtu kumuua mwingine hata kama ni adui yake?**

Hesabu 35:20-21 - Tena kwamba alimsukuma kwa kumchukia, au kwamba alimtupia kitu kwa kumvizia, hata akafa; au akampiga kwa mkono wake kwa kuwa ni adui, naye akafa; yeye aliyempiga lazima atauawa; yeye ni muuaji; mwenye kutwaa kisasi cha damu atamwua muuaji, hapo atakapokutana naye.

4. **Na je! Mtu angemuua mwenzake pasipo kukusudia, adhabu yake ilikuwa ipi?**

Hesabu 35:22-28 - Lakini ikiwa alimsukuma ghafula pasipo kumchukia; au akamtupia kitu cho chote pasipo kumvizia, au kwa jiwe liwalo lote, ambalo kwa kupigwa kwalo humkini mtu kufa, asipomwona, akamtupia hata akafa, naye hakuwa adui yake, wala hakumtakia madhara; ndipo mkutano utaamua kati ya huyo aliyempiga mtu na huyo atakayetwaa kisasi cha damu, kama hukumu hizi zilivyo; nao mkutano utamwokoa yule aliyemwua mtu na mkono wa mwenye kutwaa kisasi cha damu; tena mkutano utamrejeza katika mji wake wa makimbilio, aliokuwa anaukimbilia; naye atakaa humo hata kifo chake kuhani mkuu, aliyepakwa mafuta kwa mafuta matakatifu. Lakini kama mwenye kumwua mtu akienda wakati wo wote kupita mpaka wa huo mji wa makimbilio, alioukimbilia; na mwenye kutwaa kisasi cha damu akamwona, naye yu nje ya mpaka wa mji wake wa makimbilio, na mwenye kutwaa kisasi cha damu akamwua huyo muuaji, hatakuwa na hatia ya damu; kwa sababu ilimpasa kukaa ndani ya mji wake wa makimbilio hata kifo chake kuhani mkuu lakini kuhani mkuu atakapokwisha kufa huyo muuaji atarudi aende nchi ya urithi wake.

5. **Na kama amemuua kwa kukusudia, adhabu ilikuwa ipi?**

Hesabu 35:30 - Mtu awaye yote atakayemwua mtu, huyo muuaji atauawa kwa vinywa vya mashahidi; lakini shahidi mmoja hatashuhudia juu ya mtu hata akafa.

6. **Katika nyakati za zamani, Elohim aliitaka damu iliyo mwagwa kwa mkono wa mwanadamu au kwa mnyama?**

Mwanzo 9:5 - Hakika damu yenu ya uhai wenu nitaitaka; na kwa mkono wa kila mnyama nitaitaka; na kwa mkono wa mwanadamu, kwa mkono wa ndugu ya mtu nitataka uhai wa mwanadamu.

7. **Kwa nini Elohim aliitaka damu iliyo mwagwa?**

Mwanzo 9:6 - Atakayemwaga damu ya mwanadamu, damu yake huyo itamwagwa na mwanadamu, maana kwa mfano wake Elohim alimfanya mwanadamu.

8. **Ni nani alikuwa wa kwanza kuivuja amri hii?**

Mwanzo 4:8 - Kaini akamwambia Habili nduguye, [Twende uwandani]. Ikawa walipokuwapo uwandani, Kaini akamwinukia Habili nduguye, akamwua.

9. **Ni madhara gani yanayotokana na uvunjaji wa amri hii?**

Mwanzo 4:11-12 - Basi sasa, umelaaniwa wewe katika ardhi, iliyofumbua kinywa chake ipokee damu ya ndugu yako kwa mkono wako; utakapoilima ardhi haitakupa mazao yake; utakuwa mtoro na mtu asiye na kikao duniani.

Maelezo: Kutoa uhai ni jambo lililokatazwa katika maandiko. Hata kama utapanga njama ili mtu auawe kama inavyofanyika siku hizi, hakika yake adhabu ya Elohim inakukalia usipotubu. Uhai wa mwanadamu una dhamana kubwa machoni pa Elohim hata kama ni wa mtoto ambaye hajazaliwa. Hivyo basi tujihadhari na dhambi hii hata kama ni kwa njia ya kuavya mimba - **Abortion**.

10. **Adhabu ya wauaji wote ni gani?**

Ufunuo wa Yohana 22:15 - Huko nje wako mbwa, na wachawi, na wazinzi, na wauaji, na hao waabuduo sanamu, na kila mtu apendaye uongo na kuufanya.

Maelezo - Kutoa uhai wa mwanadamu ni dhambi kubwa mbele za Elohim, kwa kuwa maisha yana thamani kuu. Mauaji ya kukusudia yanaadhibiwa vikali, na hata yasiyokusudiwa yana masharti maalum. Hata utoaji mimba unahesabiwa kuwa dhambi, kwani maisha ya kila mtu, hata mtoto hajazaliwa, ni ya thamani. Mwisho wa wauaji ni hukumu ya milele, hivyo kila mmoja anapaswa kuheshimu maisha, kutubu, na kujiepusha na dhambi hii.

## AMRI YA SABA

Maelezo - Talaka, kuoa na kuolewa tena ni mojawapo ya dhambi zinazoongezeka sana na kukiuka mipaka nyakati hizi kama Masihi alivyonena. Hata kama sheria za nchi zinaruhusu jambo hili, bado ni dhambi na itabaki hivyo mbele ya Muumba wetu. Tunapaswa kuwa waangalifu na kufundisha ukweli juu ya somo hili, si tu juu ya somo hili muhimu, lakini kama Paulo alisema, Sikujiepusha na kuwatangazia ninyi kusudi lolote la Elohim (Matendo ya Mitume 20:17 - Toka Mileto Paulo akatuma watu kwenda Efeso, akawaita wazee wa kanisa).

1. **Baba yetu wa mbinguni amekataza vipi katika amri hii ya saba?**

Kutoka 20:14 - Usizini.

2. Ndoa itaendelea kwa muda gani? Ni wakati gani mmoja kati ya wawili hao anaweza kufunga ndoa tena?

1 Wakorintho 7:10-11,39 - Lakini wale waliokwisha kuoana nawaagiza; wala hapo si mimi, ila Bwana; mke asiachane na mumewe; lakini, ikiwa ameachana naye, na akae asiolewe, au apatane na mumewe; tena mume asimwache mkewe. Mwanamke hufungwa maadamu mumewe yu hai, lakini ikiwa mumewe amefariki, yu huru kuolewa na mtu yeyote amtakaye; katika Bwana tu.

Warumi 7:2 - Kwa maana mwanamke aliye na mume amefungwa na sheria kwa yule mume wakati anapokuwa yu hai; bali akifa yule mume, amefunguliwa ile sheria ya mume.

3. **Masihi alifundisha kwamba mtu anapoachana na mkewe au mumewe na kuoa au kuolewa tena afanya nini?**

Marko 10:11 - Akawaambia, Kila mtu atakayemwacha mkewe na kuoa mwingine azini juu yake.

Luka 16:18 - Kila amwachaye mkewe na kumwoa mke mwingine azini; naye amwoaye yeye aliyeachwa na mumewe azini.

4. **Paulo alithibitisha mafundisho haya ya Masihi? Mtu akioa au kuolewa tena mkewe au mumewe akiwa hai anaitwa nani?**

Warumi 7:3 - Basi wakati awapo hai mumewe, kama akiwa na mume mwingine huitwa mzinzi. Ila mumewe akifa, amekuwa huru, hafungwi na sheria hiyo, hata yeye si mzinzi, ajapoolewa na mume mwingine.

5. **Mtu akiwa muhusika katika dhambi atauritthi ufalme wa mbinguni?**

1 Wakorintho 6:9-10 - Au hamjui ya kuwa wadhalimu hawataurithi ufalme wa Elohim? Msidanganyike; waasherati hawataurithi ufalme wa Elohim, wala waabudu sanamu, wala wazinzi, wala wafiraji, wala walawiti, wala wevi, wala watamanio, wala walevi, wala watukanaji, wala wanyang'anyi.

6. **Ikiwa ni hivyo basi, sehemu yao itakuwa wapi? Ni nani atawadhibu?**

Ufunuo wa Yohana 21:8 - Bali waoga, na wasioamini, na wachukizao, na wauaji, na wazinzi, na wachawi, na hao waabuduo sanamu, na waongo wote, sehemu yao ni katika lile ziwa liwakalo moto na kiberiti. Hii ndiyo mauti ya pili.

Waebrania 13:4 - Ndoa na iheshimiwe na watu wote, na malazi yawe safi; kwa maana waasherati na wazinzi Elohim atawahukumia adhabu.

7. **Je, ni hatua zipi tunaweza kuchukua ili kuhakikisha ya kwamba tunajiepusha kikamilifu na ukiukaji wa amri hii?**

1 Wakorintho 6:18-20 - Ikimbieni zinaa. Kila dhambi aitendayo mwanadamu ni nje ya mwili wake; ila yeye afanyaye zinaa hutenda dhambi juu ya mwili wake mwenyewe. Au hamjui ya kuwa mwili wenu ni hekalu la Roho Mtakatifu aliye ndani yenu, mliyepewa na Elohim? Wala ninyi si mali yenu wenyewe; maana mlinunuliwa kwa thamani. Sasa basi, mtukuzeni Elohim katika miili yenu.

Maelezo - Amri ya saba inasisitiza Usizini kama agizo muhimu kutoka kwa Elohim, likilenga kuheshimu ndoa na kudumisha utakatifu wa mahusiano ya ndoa. Ingawa jamii za sasa mara nyingi zinahalalisha talaka na ndoa mpya, maandiko yanaweka wazi kuwa vitendo hivi, vinapokiuka agano la ndoa, vinabaki kuwa dhambi mbele za Elohim. Masihi alifundisha wazi kuwa talaka isiyo halali na kuoa au kuolewa tena katika hali hiyo ni uzinzi, jambo linalothibitishwa pia na mafundisho ya Paulo.

## AMRI YA NANE

1. **Je, kuna amri imewekwa ili kuzuia wizi?**

Kutoka 20:15 - Usiibe.

2. **Ni vitu gani ambavyo mtu amekatazwa kuiba?**

Kutoka 21:16 - Yeye amwibaye mtu, na kumwuza, au akipatikana mkononi mwake, sharti atauawa huyo.

Kutoka 22:1 - Mtu akiiba ng'ombe au kondoo, na kumchinja, au kumwuza; atalipa ng'ombe watano badala ya ng'ombe mmoja, na kondoo wanne badala ya kondoo mmoja.

3. **Ni dhambi gani nyingine zimetajwa pamoja na wizi?**

Mambo ya Walawi 19:11 - Msiibe, wala msidanganye, wala msiambiane uongo.

4. **Nabii Yeremia anasemaje kuhusu wizi?**

Yeremia 7:9 - Je! Mtaiba, na kuua, na kuzini, na kuapa kwa uongo, na kumfukizia Baali uvumba, na kuifuata miungu mingine ambayo hamkuijua.

5. **Kwa nini Waisraeli walishindwa vitani?**

Yoshua 7:12-21 - Ndiposa wana wa Israeli hawawezi kusimama mbele ya adui zao; wakawapa visogo adui zao, kwa sababu wamelaaniwa; mimi sitakuwa pamoja nanyi tena, msipokiharibu kitu kile mlicho nacho kilichowekwa wakfu. Haya! Inuka, uwatakase watu, ukaseme, Jitakaseni, mwe tayari kesho; maana BWANA, Elohim wa Israeli, asema hivi; Kitu kilichowekwa wakfu kiko katikati yako, Ee Israeli; huwezi kusimama mbele ya adui zako, hata mtakapokiondoa kile mlicho nacho kilichowekwa wakfu. Basi asubuhi mtaletwa karibu nami kabila kwa kabila; kisha itakuwa ya kwamba kabila ile atakayoitwaa BWANA itakaribia jamaa kwa jamaa; na jamaa ile atakayoitwaa BWANA itakaribia nyumba kwa nyumba; na nyumba ile atakayoitwaa BWANA itakaribia mtu kwa mtu. Tena itakuwa ya kwamba yeye atakayetwaliwa, naye anacho kitu kile kilichowekwa wakfu, atateketezwa kwa moto, yeye na vitu vyote alivyo navyo; kwa sababu amelivunja agano la BWANA, na kwa sababu ametenda upumbavu katika Israeli. Basi Yoshua akaondoka asubuhi na mapema, akawasogeza Israeli kabila kwa kabila; kabila ya Yuda ikatwaliwa. Akazisogeza jamaa za Yuda, akaitwaa jamaa ya Wazera; akaisogeza jamaa ya Wazera mtu kwa mtu; Zabdi akatwaliwa. Akawasogeza watu wa nyumba yake mmoja mmoja; na Akani, mwana wa Karmi, mwana wa Zabdi, mwana wa Zera, wa kabila ya Yuda akatwaliwa. Yoshua akamwambia Akani, Mwanangu, nakusihi, umtukuze BWANA, Elohim wa Israeli, ukaungame kwake; uniambie sasa ulilolitenda; usinifiche. Akani akamjibu Yoshua, akasema, Kweli nimefanya dhambi juu ya BWANA, Elohim wa Israeli, nami nimefanya mambo haya na haya.
Nilipoona katika nyara joho nzuri ya Babeli, na shekeli mia mbili za fedha, na

kabari ya dhahabu, uzani wake shekeli hamsini, basi nalivitamani nikavitwaa; tazama, vimefichwa mchangani katikati ya hema yangu, na ile fedha chini yake.

6. **Mwokozi alisisitiza kuepuka wizi; je, hii ni njia ya kupata uzima wa milele?**

Mathayo 19:16-19 - Na tazama, mtu mmoja akamwendea akamwambia, Mwalimu, nitende jambo gani jema, ili nipate uzima wa milele? Akamwambia Kwani kuniuliza habari ya wema? Aliye mwema ni mmoja. Lakini ukitaka kuingia katika uzima, zishike amri. Akamwambia, Zipi? Yahshua akasema, Ni hizi, Usiue, Usizini, Usiibe, Usishuhudie uongo, Waheshimu baba yako na mama yako, na, Mpende jirani yako kama nafsi yako.

7. **Maandiko yanasema mwizi awe na tabia gani?**

Waefeso 4:28 - Mwibaji asiibe tena; bali afadhali afanye juhudi, akitenda kazi iliyo nzuri kwa mikono yake mwenyewe, apate kuwa na kitu cha kumgawia mhitaji.

8. **Ombi la Sulemani lilikuwa nini?**

Mithali 30:7-9 - Mambo haya mawili nimekuomba; Usininyime [matatu] kabla sijafa. Uniondolee ubatili na uongo; Usinipe umaskini wala utajiri; Unilishe chakula kilicho kadiri yangu. Nisije nikashiba nikakukana, Nikasema, BWANA ni nani? Wala nisiwe maskini sana nikaiba, Na kulitaja bure jina la Elohim wangu.

9. **Je, kuna wizi katika biashara?**

Hosea 12:7 - Ni mchuuzi, mizani ya udanganyifu i mkononi mwake; anapenda kudhulumu.

Amosi 8:5 - mkisema, Mwezi mpya utaondoka lini, tupate kuuza nafaka? Na sabato nayo, tupate kuandika ngano? Mkiipunguza efa na kuiongeza shekeli, mkidanganya watu kwa mizani ya udanganyifu.

Mika 6:9-12 - Sauti ya BWANA inaulilia mji, na mtu mwenye akili ataliona jina lako; isikieni hiyo fimbo na yeye aliyeiagiza. Je! Hata sasa hazina za uovu zingalimo nyumbani mwa wabaya, na kipimo kilichopunguka, ambacho ni chukizo? Je! Naweza kuwa safi nami nina mizani ya udhalimu, na mfuko wa mawe ya kupimia ya udanganyifu? Kwa maana matajiri wake wamejaa jeuri, na wenyeji wake wamesema uongo, na ulimi wao una udanganyifu kichwani mwao.

10. **Tumepewa ushauri gani kuhusu vipimo katika biashara zetu?**

Ezekieli 45:9-10 - Bwana Elohim asema hivi; Na iwatoshe ninyi, enyi wakuu wa Israeli; ondoeni dhuluma na unyang'anyi; fanyeni hukumu na haki; ondoeni kutoza kwa nguvu kwenu katika watu wangu, asema Bwana Elohim. Mtakuwa na mizani ya haki, na efa ya haki, na bathi ya haki.

**11. Je, wezi watairithi ufalme wa mbinguni?**

1 Wakorintho 6:9-10 - Au hamjui ya kuwa wadhalimu hawatairithi ufalme wa Elohim? Msidanganyike; waasherati hawatairithi ufalme wa Elohim, wala waabudu sanamu, wala wazinzi, wala wafiraji, wala walawiti, wala wevi, wala watamanio, wala walevi, wala watukanaji, wala wanyang'anyi.

Maelezo - Biblia inaonyesha kwa uwazi kwamba wizi ni dhambi inayochukiza mbele za Elohim na inayoleta athari mbaya kwa mtu binafsi, jamii, na uhusiano wa kiroho kati ya mwanadamu na Muumba wake. Wizi ni dhambi inayopingana na haki, upendo, na heshima kwa Elohim na wanadamu. Kila mmoja anaitwa kuishi maisha ya uadilifu, uaminifu, na huruma, akiepuka wizi kwa namna zote. Kwa kushika amri ya nane, watu wanapokea baraka za Elohim, kuepuka hukumu, na kujenga jamii yenye mshikamano na haki.

## AMRI YA TISA

1. **Amri ya tisa inatuzuia kufanya nini?**

Kutoka 20:16 - Usimshuhudie jirani yako uongo.

Kumbukumbu la Torati 5:20 - Wala usimshuhudie jirani yako uongo.

2. **Elohim ametukanya dhidi ya kuvumisha Habari za uongo? Na kuwa shahidi wa udhalimu?**

Kutoka 23:1 - Usivumishe habari za uongo; usitie mkono wako pamoja na mwovu, kuwa shahidi wa udhalimu.

3. **Kwa nini tunafaa kujiepusha na ushuhuda wa uongo dhidi ya majirani wetu?**

Kutoka 23:2 - Usiandamane na mkutano kutenda uovu; wala usitie ushahidi wako katika neno lo lote kwa kugeukia kando na kuandamana na mkutano ili kupotoa hukumu.

Waefeso 4:25 - Basi uvueni uongo, mkaseme kweli kila mtu na jirani yake; kwa maana tu viungo, kila mmoja kiungo cha wenzake.

Maelezo: Ushuhuda wa uongo unaweza kupotoa hukumu.

4. **Je, Elohim huchukia ulimi usemao uongo?**

Mithali 6:16-17,19 - Kuna vitu sita anavyovichukia BWANA; Naam, viko saba vilivyo chukizo kwake. Macho ya kiburi, ulimi wa uongo, Na mikono imwagayo damu isiyo na hatia. Shahidi wa uongo asemaye uongo; Naye apandaye mbegu za fitina kati ya ndugu.

5. **Je, kusema uongo kunaweza kusababisha uharibifu?**

Mithali 26:28 - Ulimi unenao uongo huwachukia wale uliowajeruhi; Na kinywa cha kujipendekeza hutenda uharibifu.

Yakobo 3:6 - Nao ulimi ni moto; ule ulimwengu wa uovu, ule ulimi, umewekwa katika viungo vyetu, nao ndio uutiao mwili wote unajisi, huuwasha moto mfulizo wa maumbile, nao huwashwa moto na jehanum.

6. **Tuna mfano mwafaka wa maafa makubwa yaliyosababishwa na ushuhuda wa uongo?**

1 Wafalme 21:8-10,13 - Basi, akaandika nyaraka kwa jina la Ahabu, akazitia muhuri yake, akazipeleka zile nyaraka kwa wazee, na kwa watu wenye nguvu waliokuwa katika mji wake, waliokaa pamoja na Nabothi. Akaandika katika zile nyaraka, akasema, Pigeni mbiu ya watu kufunga, mkamweke Nabothi juu mbele ya watu, mkainue watu wawili, watu wasiofaa, ili wamshitaki, na kumshuhudia, kunena, Umemtukana Elohim na mfalme. Kisha mchukueni nje, mkampige kwa mawe, ili afe. Na hao watu wawili, watu wasiofaa, wakaingia, wakaketi mbele yake; wale watu wasiofaa wakamshuhudia Nabothi mbele ya watu, wakasema, Nabothi amemtukana Elohim na mfalme. Ndipo wakamchukua nje ya mji, wakampiga kwa mawe hata akafa.

Maelezo - Kushiriki katika uongo kunaweza kuonekana kama ni dhambi ndogo. Lakini husababisha dhambi kubwa hata ya mauaji.

7. **Mtu aweza kuwa shahidi wa uongo dhidi ya Elohim?**

1 Yohana 2:4 - Yeye asemaye, Nimemjua, wala hazishiki amri zake, ni mwongo, wala kweli haimo ndani yake.

**8. Tunaweza kuepuka kuvunja amri hii kwa njia gani?**

1 Yohana 2:6 - Yeye asemaye ya kuwa anakaa ndani yake, imempasa kuenenda mwenyewe vile vile kama yeye alivyoenenda.

Warumi 13:8-9 - Msiwiwe na mtu cho chote, isipokuwa kupendana; kwa maana ampendaye mwenzake ameitimiza sheria. Maana kule kusema, Usizini, Usiue, Usiibe, Usitamani; na ikiwapo amri nyingine yo yote, inajumlishwa katika neno hili, ya kwamba, Mpende jirani yako kama nafsi yako.

**9. Tunafaa kuiga mtazamo upi mwafaka katika maisha yetu hapa duniani?**

Ayubu 27:4-6 - Hakika midomo yangu haitanena yasiyo haki, Wala ulimi wangu hautatamka udanganyifu. Hasha! Nisiwahesabie ninyi kuwa na haki; Hata nitakapokufa sitajiondolea uelekevu wangu. Haki yangu naishika sana, wala sitaiacha; Moyo wangu hautanisuta wakati nikiwapo hai.

**10.Je, twawezaje kuzuia miili yetu kutenda maovu, na kuwa wakamilifu?**

Yakobo 3:2 - Maana twajikwaa sisi sote pia katika mambo mengi. Mtu asiyejikwaa katika kunena, huyo ni mtu mkamilifu, awezaye kuuzuia na mwili wake wote kama kwa lijamu.

1 Petro 3:10 - Kwa maana, Atakaye kupenda maisha, Na kuona siku njema, Auzuie ulimi wake usinene mabaya, Na midomo yake isiseme hila.

**11.Je, ni nani atakayekaa katika hema ya Elohim?**

Zaburi 15:2-3 - Ni mtu aendaye kwa ukamilifu, Na kutenda haki. Asemaye kweli kwa moyo wake, Asiyesingizia kwa ulimi wake. Wala hakumtenda mwenziwe mabaya, Wala hakumsengenya jirani yake.

Maelezo - Amri ya Tisa inatufundisha kuwa ukweli ni msingi wa maisha ya haki na amani. Ushuhuda wa uongo sio tu kwamba unavunja uaminifu kati ya watu, bali pia unamchukiza Elohim. Tunaonywa dhidi ya kushirikiana na uongo, hata kwa hila ndogo, kwa sababu matokeo yake yanaweza kuwa mabaya na ya kudumu. Tunaweza kuepuka kuvunja amri hii kwa kuenenda kwa kweli, kuonyesha upendo kwa jirani zetu, na kuiga mfano wa Masihi. Kila mmoja anapaswa kudhibiti ulimi wake na kuwa kielelezo cha uaminifu katika jamii.

## AMRI YA KUMI

1. **Je! Amri ya kumi inatuonya aje?**

Kutoka 20:17 - Usiitamani nyumba ya jirani yako, usimtamani mke wa jirani yako; wala mtumwa wake, wala mjakazi wake, wala ng'ombe wake, wala punda wake, wala cho chote alicho nacho jirani yako.

Warumi 7:7 - Tusemeje, basi? Torati ni dhambi? Hasha! Walakini singalitambua dhambi ila kwa sheria; kwa kuwa singalijua kutamani, kama torati isingalisema, Usitamani.

2. **Je! Tamaa mbaya, na kila aina ya uwovu hutoka wapi?**

Marko 7:21-23 - Kwa maana ndani ya mioyo ya watu hutoka mawazo mabaya, uasherati, wivi, uuaji, uzinzi, tamaa mbaya, ukorofi, hila, ufisadi, kijicho, matukano, kiburi, upumbavu.Haya yote yaliyo maovu yatoka ndani, nayo yamtia mtu unajisi.

Yakobo 1:14-15 - Lakini kila mmoja hujaribiwa na tamaa yake mwenyewe huku akivutwa na kudanganywa. Halafu ile tamaa ikiisha kuchukua mimba huzaa dhambi, na ile dhambi ikiisha kukomaa huzaa mauti.

3. **Dhambi ya tamaa mbaya imeorodheshwa pamoja na dhambi gani nyingine?**

1 Wakorintho 5:11 - Lakini, mambo yalivyo, naliwaandikia kwamba msichangamane na mtu aitwaye ndugu, akiwa ni mzinzi au mwenye kutamani au mwenye kuabudu sanamu au mtukanaji au mlevi au mnyang'anyi; mtu wa namna hii msikubali hata kula naye.

4. **Ni nini ya huzuni husababishwa na tamaa?**

1 Timotheo 6:10 - Maana shina moja la mabaya ya kila namna ni kupenda fedha; ambayo wengine hali wakiitamani hiyo wamefarakana na Imani, na kujichoma kwa maumivu mengi.

5. **Je! Tumeamurishwa kuikimbia tamaa?**

1 Timotheo 6:11 - Bali wewe, mtu wa Elohim, uyakimbie mambo hayo; ukafuate haki, utauwa, imani, upendo, saburi, upole.Maelezo.

Maelezo - Amri ya kumi yatusaidia kuwa na kiasi cha kudhibiti maisha yetu katika hali zote ili kuzingatia yaliyo muhimu.

**6. Je! Hali ya kutamani itaongezeka siku za mwisho?**

2 Timotheo 3:1-2 -Lakini ufahamu neno hili, ya kuwa siku za mwisho kutakuwako nyakati za hatari.Maana watu watakuwa wenye kujipenda wenyewe, wenye kupenda fedha, wenye kujisifu, wenye kiburi, wenye kutukana, wasiotii wazazi wao, wasio na shukrani, wasio safi.

**7. Yahshua alisema nini kuhusu tamaa mbaya?**

Luka 12:15 - Akawaambia, Angalieni, jilindeni na choyo, maana uzima wa mtu haumo katika wingi wa vitu vyake alivyo navyo.

**8. Tunapaswa kufanya nini ili kuishinda tamaa ya mwili?**

Wakolosai 3:5-6 - Basi, vifisheni viungo vyenu vilivyo katika nchi, uasherati, uchafu, tamaa mbaya, mawazo mabaya, na kutamani, ndiyo ibada ya sanamu; kwa ajili ya mambo hayo huja ghadhabu ya Elohim.

**9. Watu wa Elohim wameruhusiwa kuwa na tamaa ipi?**

1 Wakorintho 12:31 - Takeni sana karama zilizo kuu. Hata hivyo nawaonyesha njia iliyo bora.

1 Wakorintho 14:39 - Kwa ajili ya hayo, ndugu, takeni sana kuhutubu, wala msizuie kunena kwa lugha.

**10.Je! Wenye tamaa mbaya wataridhi ufalme wa milele?**

1 Wakorintho 6:9-10 - Au hamjui ya kuwa wadhalimu hawataurithi ufalme wa Elohim? Msidanganyike; waasherati hawataurithi ufalme wa Elohim, wala waabudu sanamu, wala wazinzi, wala wafiraji, wala walawiti, wala wevi, wala watamanio, wala walevi, wala watukanaji, wala wanyang'anyi.

Waefeso 5:5 - Maana neno hili mnalijua hakika, ya kwamba hakuna mwasherati wala mchafu wala mwenye tamaa, ndiye mwabudu sanamu, aliye na urithi katika ufalme wa Messiah na Elohim.

Maelezo - Amri ya Kumi inatufundisha kuishi kwa kujidhibiti, kupinga tamaa za mwili, na kuzingatia mambo ya kiroho. Tamaa mbaya, ingawa ni ya ndani, ina uwezo wa kuharibu maisha ya kiroho na ya kijamii. Kwa kufuata mafundisho ya maandiko, tunaweza kuishi maisha ya haki, kujizuia kutokana na maovu, na

kuzingatia yaliyo muhimu kwa ajili ya urithi wa milele. Amri hii inatufundisha kuridhika, kupenda yaliyo mema, na kuacha kushindana kwa vitu vya dunia.

# SEHEMU YA PILI

# MANABII NA IMANI YA YAHSHUAH

## UTANGULIZI WA SEHEMU YA PILI

Baada ya kuchunguza Amri kumi katika maandiko. Ni vyema tuangalie baadhi ya mambo yanayohusu imani ya Yahshuah ambayo inahitajika ili kuuridhi Ufalme wa Elohim. Katika sehemu hii ya pili tutajifunza kwa kina kuhusu chemichemi ya wokovu wa kweli. Tutapata kujua jinsi watu wote - wayahudi na wayunani wanaweza kupata wokovu huu. Katika Ufunuo, Yohana alionyeshwa wateule wenye Subira ni wale wanaoshika Amri za Elohim tulizojifunza katika sehemu ya kwanza na kuwa na Imani ya Yahshuah. Ufunuo 14:12 - **Hapa ndipo penye subira ya watakatifu, hao wazishikao amri za Elohim, na imani ya Yahshuah.**

Sehemu hii ya pili pia itaangazia yale yaliyotabiriwa na manabii kuhusu yatakayotokea katika siku za baazaye. Baadhi yake ni ndoto na njozi ambazo Elohim aliwapa watumishi wake Danieli, mfalme wa Babeli aliyejulikana kama Nebukadneza na yakafunuliwa Mtume Yohana. Mambo hay ani muhimu katika imani kwa sababu yanatujulisha yatakayotokea huku yakitoa tahadhari ya hukumu kwa wote wasiotii amri na Imani ya Yahshuah. Maandiko yanatuagiza na kutuhimiza tusome, tusikilize na tuyashike mambo ya unabii. Ufunuo 1:3.- **Heri asomaye na wao wayasikiao maneno ya unabii huu, na kuyashika yaliyoandikwa humo; kwa maana wakati u karibu.**

Umuhimu wa sehemu hii ni kukamilisha imani yetu ambayo imejengwa juu ya msingi wa manabii na mitume, naye Masihi ndiye jiwe kuu la pembeni. Waefeso 2:20 – 21 - **Mmejengwa juu ya msingi wa mitume na manabii, naye Kristo Yahshuah mwenyewe ni jiwe kuu la pembeni. Katika yeye jengo lote linaungamanishwa vema na kukua hata liwe hekalu takatifu katika Bwana.**

## CHEMICHEMI

1. **Ni kwa nani twaipata chemichemi?**

Zaburi 36:9 - Maana kwako Wewe iko chemchemi ya uzima, Katika nuru yako tutaona nuru.

2. **Je! Elohim humjulisha nani neno lake?**

Zaburi 147:19-20 - Humhubiri Yakobo neno lake, Na Israeli amri zake na hukumu zake. Hakulitendea taifa lo lote mambo kama hayo, Wala hukumu zake hawakuzijua. Haleluya.

3. **Je! Nabii Isaya alitabiri vipi kuhusu siku za mwisho?**

Isaya 2:2-3 - Na itakuwa katika siku za mwisho, mlima wa nyumba ya Bwana utawekwa imara juu ya milima, nao utainuliwa juu ya vilima; na mataifa yote watauendea makundi makundi. Na mataifa mengi watakwenda na kusema, Njoni, twende juu mlimani kwa Bwana, nyumbani kwa Elohim wa Yakobo, naye atatufundisha njia zake, nasi tutakwenda katika mapito yake maana katika Sayuni itatoka sheria, na neno la Bwana katika Yerusalemu.

4. **Je! Masihi alisema injili itahubiriwa kutoka wapi?**

Luka 24:47 - Na kwamba mataifa yote watahubiriwa kwa jina lake habari ya toba na ondoleo la dhambi, kuanza tangu Yerusalemu.

5. **Je! Wokovu watoka wapi?**

Yohana 4:22 - Ninyi mnaabudu msichokijua; sisi tunaabudu tukijuacho; kwa kuwa wokovu watoka kwa Wayahudi.

6. **Paulo alisema vipi kuhusiana na mada hii?**

Warumi 9:4 - Ambao ni Waisraeli, wenye kule kufanywa wana, na ule utukufu, na maagano, na kupewa torati, na ibada ya Elohim, na ahadi zake.

Warumi 3:1-2 - Basi Myahudi ana ziada gani? Na kutahiriwa kwafaa nini? Kwafaa sana kwa kila njia. Kwanza kwa kuwa wamekabidhiwa mausia ya Elohim.

7. **Ni kwa sababu gani ilimpendeza Elohim injili ihubiriwe kutoka Yerusalemu?**

Zekaria 8:3 - Bwana asema hivi, Mimi nimerudi Sayuni, nami nitakaa katikati ya Yerusalemu; na Yerusalemu utaitwa, Mji wa kweli; na Mlima wa Bwana wa majeshi utaitwa, Mlima mtakatifu.

Kutoka 4:22 - Nawe umwambie Farao, Bwana asema hivi, Israeli ni mwanangu mimi, mzaliwa wa kwanza wangu.

Amosi 3:1-2 - Lisikieni neno hili alilolisema Bwana juu yenu, enyi wana wa Israeli, juu ya jamaa yote niliowapandisha kutoka nchi ya Misri, nikisema, Ni ninyi

tu niliowajua katika jamaa zote zilizo duniani; kwa sababu hiyo nitawapatiliza ninyi maovu yenu yote.

Matendo ya Mitume 10:37-39 - Jambo lile ninyi mmelijua, lililoenea katika Uyahudi wote likianzia Galilaya, baada ya ubatizo aliouhubiri Yohana; habari za Yahshuah wa Nazareti, jinsi Elohim alivyomtia mafuta kwa Roho Mtakatifu na nguvu naye akazunguka huko na huko, akitenda kazi njema na kuponya wote walioonewa na Ibilisi; kwa maana Elohim alikuwa pamoja naye.

**8. Kama ni hivyo kwa nini watu wa mataifa hawalipokei neno hili?**

Matendo ya Mitume 16:20-21 - Wakawachukua kwa makadhi, wakasema, Watu hawa wanachafua sana mji wetu, nao ni Wayahudi; tena wanatangaza habari ya desturi zisizokuwa halali kwetu kuzipokea wala kuzifuata, kwa kuwa sisi tu Warumi.

2 Wakorintho 4:3-4 - Lakini ikiwa injili yetu imesitirika, imesitirika kwa hao wanaopotea; ambao ndani yao Elohim wa dunia hii amepofusha fikira zao wasioamini, isiwazukie nuru ya injili ya utukufu wake Messiah aliye sura yake Elohim.

Yeremia 2:11 - Je! Taifa wamebadili miungu yao, ingawa siyo miungu? Lakini watu wangu wameubadili utukufu wao kwa ajili ya kitu kisichofaidia.

Maelezo - Ijapokuwa Injili ya kweli ililetwa ili kumwokoa mwanadamu, Shetani, kama baba wa uongo (Yohana 8:44), amepotosha wengi kwa kuwazuia kuona nuru ya Injili (2 Wakorintho 4:4). Hata hivyo, mpango wa Elohim hauwezi kuzuiliwa, kwani Yahshua aliahidi kuwa Injili itahubiriwa kwa mataifa yote kabla ya mwisho (Mathayo 24:14). Hili linatuthibitisha kwamba Injili ni nguvu ya Elohim na Yeye ndiye huleta wokovu wa kila mtu aaminiye (Warumi 1:16).

**9. Je! Mataifa wamepata chemichemi mahali pengine?**

Yeremia 2:13 - Kwa maana watu wangu hawa wametenda maovu mawili; wameniacha mimi, niliye chemchemi ya maji ya uzima, wamejichimbia mabirika, mabirika yavujayo, yasiyoweza kuweka maji.

Maelezo - Safari ya Injili inadhihirisha mpango mkuu wa Elohim wa ukombozi: kwanza uliwasilishwa kwa Wayahudi kama watu wake wateule, wengi waliukataa, wakitimiza unabii na kuandaa njia kwa Mataifa kuupokea kwa mioyo iliyo wazi (Yohana 1:11; Warumi 11:11). Utimilifu wa Mataifa unapofikiwa (Warumi 11:25), Biblia inatabiri kwamba watu wa mataifa mengine watazidi kukataa Injili (2

Timotheo 4:3-4), wakati Israeli watamrudia Masihi wao kwa toba na imani kama ilivyotabiriwa katika Zekaria 12:10. Safu hii ya kinabii inadhihirisha uaminifu usiobadilika wa Elohim kwa ahadi zake, kuhakikisha wokovu wa mwisho wa Israeli na kuonyesha rehema zake kwa wanadamu wote (Warumi 11:29, 33).

## UBATIZO

1. **Ni ujumbe gani unaoambatana na kuhubiriwa kwa injili ya kweli?**

Mathayo 3:1-2 - Siku zile alitokea Yohana Mbatizaji akihubiri katika nyika ya Uyahudi, akisema, Tubuni; kwa maana ufalme wa mbinguni umekaribia. Kwa sababu huyo ndiye aliyenenwa na nabii Isaya, akisema, Sauti ya mtu aliaye nyikani, Itengenezeni njia ya Bwana, Yanyosheni mapito yake.

2. **Baada ya kutubu, ni jambo gani hufuata?**

Matendo ya Mitume 2:38 - Petro akawaambia, Tubuni mkabatizwe kila mmoja kwa jina la Yahshuah Messiah, mpate ondoleo la dhambi zenu, nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu.

3. **Kwa nini ni lazima kubatizwa?**

Yohana 3:3 - Yahshuah akajibu, akamwambia, Amin, amin, nakuambia, Mtu asipozaliwa mara ya pili, hawezi kuuona ufalme wa Elohim.

4. **Kwa nini huwezi kurithi ufalme bila kubatizwa?**

1 Wakorintho 15:50 - Ndugu zangu, nisemayo ni haya, ya kuwa nyama na damu haziwezi kuurithi ufalme wa Elohim; wala uharibifu kurithi kutokuharibika.

5. **Nini itatutoa katika hali hii ya mwili na damu?**

Yohana 3:5-6 - Yahshuah akajibu, Amin, amin, nakuambia, Mtu asipozaliwa kwa maji na kwa Roho, hawezi kuuingia ufalme wa Elohim. Kilichozaliwa kwa mwili ni mwili; na kilichozaliwa kwa Roho ni roho.

6. **Ni kiasi gani cha maji kinahitajika katika ubatizo?**

Matendo ya Mitume 8:38 - Akaamuru lile gari lisimame; wakatelemka wote wawili majini, Filipo na yule towashi; naye akambatiza.

Yohana 3:23 - Yohana naye alikuwa akibatiza huko Ainoni, karibu na Salimu, kwa sababu huko kulikuwa na maji tele; na watu wakamwendea, wakabatizwa.

7. **Mbona lazima iwe maji mengi?**

Warumi 6:3-4 - Hamfahamu ya kuwa sisi sote tuliobatizwa katika Messiah Yahshuah tulibatizwa katika mauti yake? Basi tulizikwa pamoja naye kwa njia ya ubatizo katika mauti yake, kusudi kama Messiah alivyofufuka katika wafu kwa njia ya utukufu wa Baba, vivyo hivyo na sisi tuenende katika upya wa uzima.

8. **Ni agizo gani walipewa kutekeleza jambo hili?**

Mathayo 28:19 - Basi, enendeni, mkawafanye mataifa yote kuwa wanafunzi, mkiwabatiza kwa jina la Baba, na Mwana, na Roho Mtakatifu.

Maelezo: Mwokozi wetu aliwaamuru mitume wakabatize kwa jina moja tu la Yahshuah Messiah, ambalo ndilo jina la pekee la Baba, ndilo la Mwana pia na hilo hilo ndilo la Roho Mtakatifu. Jua kwamba, Messiah hakumaanisha majina matatu, ndiposa akasema kwa jina la Baba, na Mwana na Roho Mtakatifu ila sio kwa jina la Baba, na la Mwana, na la Roho.

9. **Ni kupitia jina lipi la kipekee walitimiza maagizo haya?**

Matendo ya Mitume 19:5 - Waliposikia haya wakabatizwa kwa jina la Bwana Yahshuah.

Maelezo - Jina la Yahshua linaonyesha ukuu na umuhimu wa kipekee katika mpango wa wokovu wa wanadamu. Wafilipi 2:9 inafundisha kuwa Elohim alimwadhimisha Yahshua na kumkirimia jina lililo juu ya majina yote, likiwa na mamlaka ya kipekee mbinguni na duniani. Matendo ya Mitume 4:12 inasisitiza kuwa hakuna jina lingine chini ya mbingu lililopewa wanadamu kwa ajili ya wokovu isipokuwa Yahshua. Maana ya jina hili ni Elohim anaokoa, linaonyesha jukumu lake kama Mwokozi wa ulimwengu na njia pekee ya kuwapatanisha wanadamu na Elohim. Wokovu ni neema ya Elohim kupitia Yahshua pekee, si kwa juhudi za kibinadamu. Hivyo, kila mtu anapaswa kumwamini na kulitaja jina lake kwa imani ili kupokea wokovu, amani na uzima wa milele.

10. **Wanao batizwa hivi, huwa na uhusiano gani na Elohim?**

Yohana 1:12-13 - Bali wote waliompokea aliwapa uwezo wa kufanyika watoto wa Elohim, ndio wale waliaminio jina lake; waliozaliwa, si kwa damu, wala si kwa mapenzi ya mwili, wala si kwa mapenzi ya mtu, bali kwa Elohim.

Maelezo: Wanadamu wametafuta njia tofauti za kubatiza kama vile, kunyunyuziwa maji, kuombewa na kupewa jina jipya la ubatizo, wengine hufanywa tohara kwa mara ya pili, wengine hung'olewa baadhi ya meno, wengine hulazimishwa kupita ndani ya moto, na wengine hupitishwa chini ya bendera na vinginevyo. Ila, maandiko yanatueleza waziwazi kuwa, Ubatizo wa kweli ni mmoja ambao ni wa kutumbukizwa katika maji mengi, kwa jina la Yahshuah Messiah, ambayo ndiyo njia ya pekee ya kumfanya mtu kuwa mwana wa Elohim.

## TUMAINI LA WATAKATIFU

1. **Dunia iliumbwa kwa kusudi gani?**

Isaya 45:18 - Maana Bwana, aliyeziumba mbingu, asema hivi; Yeye ni Elohim; ndiye aliyeiumba dunia na kuifanya; ndiye aliyeifanya imara; hakuiumba ukiwa, aliiumba ili ikaliwe na watu; Mimi ni Bwana, wala hapana mwingine.

2. **Masihi aliwafundisha mitume waombe nini?**

Mathayo 6:9-10 - Basi ninyi salini hivi; Baba yetu uliye mbinguni, Jina lako litukuzwe, Ufalme wako uje, Mapenzi yako yatimizwe, hapa duniani kama huko mbinguni.

3. **Watu waliokombolewa kwa damu ya mwana kondoo watamiliki wapi?**

Ufunuo wa Yohana 5:9-10 - Nao waimba wimbo mpya wakisema, Wastahili wewe kukitwaa hicho kitabu na kuzifungua muhuri zake; kwa kuwa ulichinjwa, ukamnunulia Elohim kwa damu yako watu wa kila kabila na lugha na jamaa na taifa, ukawafanya kuwa ufalme na makuhani kwa Elohim wetu; nao wanamiliki juu ya nchi.

4. **Masihi atashuka kutoka wapi, na watakatifu wake watamlaki wapi?**

1 Wathesalonike 4:16-17 - Kwa sababu Bwana mwenyewe atashuka kutoka mbinguni pamoja na mwaliko, na sauti ya malaika mkuu, na parapanda ya Elohim; nao waliokufa katika Messiah watafufuliwa kwanza. Kisha sisi tulio hai, tuliosalia, tutanyakuliwa pamoja nao katika mawingu, ili tumlaki Bwana hewani; na hivyo tutakuwa pamoja na Bwana milele.

5. **Wateule watakapo mlaki Masihi hewani watakwenda wapi?**

Isaya 35:10 - Na hao waliokombolewa na Bwana watarudi, watafika Sayuni wakiimba; na furaha ya milele itakuwa juu ya vichwa vyao; nao watapata kicheko na furaha, huzuni na kuugua zitakimbia.

6. **Sayuni iko mbuguni au iko duniani?**

2 Samueli 5:7 - Lakini Daudi aliipiga ngome ya Sayuni; huu ndio mji wa Daudi.

7. **Malaika wa saba alitoa ushahidi gani?**

Ufunuo wa Yohana 11:15 - Malaika wa saba akapiga baragumu, pakawa na sauti kuu katika mbingu, zikisema, Ufalme wa dunia umekwisha kuwa ufalme wa Bwana wetu na wa Messiah wake, naye atamiliki hata milele na milele.

8. **Masihi alisema tusifadhaike kwa sababu gani?**

Yohana 14:1-2 - Msifadhaike mioyoni mwenu; mnamwamini Elohim, niaminini na mimi. Nyumbani mwa Baba yangu mna makao mengi; kama sivyo, ningaliwaambia; maana naenda kuwaandalia mahali.

9. **Hayo makao Yohana aliyaona?**

Ufunuo wa Yohana 21:2-3 - Nami nikauona mji ule mtakatifu, Yerusalemu mpya, ukishuka kutoka mbinguni kwa Elohim, umewekwa tayari, kama bibi-arusi aliyekwisha kupambwa kwa mumewe. Nikasikia sauti kubwa kutoka katika kile kiti cha enzi ikisema, Tazama, maskani ya Elohim ni pamoja na wanadamu, naye atafanya maskani yake pamoja nao, nao watakuwa watu wake. Naye Elohim mwenyewe atakuwa pamoja nao.

10. **Kuja kwa Mwokozi kutakuwa dhahiri?**

Matendo ya Mitume 1:11 - Wakasema, Enyi watu wa Galilaya, mbona mmesimama mkitazama mbinguni? Huyu Yahshuah aliyechukuliwa kutoka kwenu kwenda juu mbinguni, atakuja jinsi iyo hiyo mlivyomwona akienda zake mbinguni.

Maelezo - Somo hili linahusu tumaini la watakatifu, likionyesha kuwa dunia iliumbwa na Elohim ili ikaliwe na wanadamu huku wakidumisha haki na amani. Ni dhahiri kuwa Mwokozi atarudi kutoka mbinguni, na watakatifu wake watamlaki hewani. Hatimaye, watakatifu watafika Sayuni, mji wa milele wa Elohim, ambapo huzuni na maumivu hayatakuwepo tena. Kwa hivyo, tunahimizwa umuhimu wa kuishi kwa imani, tukisubiri makao matakatifu ambayo Elohim ameandaa kwa watu wake.

## MLIMA WA MORIA

1. **Ni jambo lipi Elohim alifanya ili kudhihirisha Mlima huu?**

Mwanzo12:1;5. " Bwana akamwambia Abramu, Toka wewe katika nchi yako, na jamaa zako, na nyumba ya baba yako, uende mpaka nchi nitakayokuonyesha; Abramu akamchukua Sarai mkewe, na Lutu mwana wa nduguye, na vitu vyao vyote walivyokuwa wamejipatia na hao watu waliowapata huko Harani, wakatoka ili kwenda nchi ya Kanaani; nao wakaingia katika nchi ya Kanaani."

2. **Ni lipi Elohim alimuahidi alipofika nchi ya canani?**

Mwanzo 12 :7. "Bwana akamtokea Abramu, akasema, Uzao wako nitawapa nchi hii. Naye huko akamjengea madhababu Bwana aliyemtokea."

3. **Ili kuidhibitsha Imani yake Kwa Elohim ni jambo lipi aliagizwa kulitenda?**

Mwanzo 22:1-2. Ikawa baada ya mambo hayo Elohim alimjaribu Ibrahimu, akamwambia, Ee Ibrahimu! Naye akasema, Mimi hapa. Akasema, Umchukue mwanao, mwana wako wa pekee, umpendaye, Isaka, ukaende zako mpaka nchi ya Moria, ukamtoe sadaka ya kuteketezwa huko juu ya mlima mmojawapo nitakaokuambia."

Fahamu: Hapa ndipo muumba wa mbingu na nchi anajulisha Abraham kuhusu utakatifu wa mlima huu wa MORIA.

4. **Mwana huyu wake wa pekee ni nani?**

Mwanzo 22:3;11-12. Ibrahimu akaondoka alfajiri, akatandika punda wake, akachukua vijana wawili pamoja naye, na Isaka mwanawe, akachanja kuni kwa ajili ya hiyo sadaka ya kuteketezwa, akaondoka, akaenda mpaka mahali alipoambiwa na Elohim.

Ndipo malaika wa Bwana akamwita kutoka mbinguni, akasema, Ibrahimu! Ibrahimu! Naye akasema, Mimi hapa. Akasema, Usimnyoshee kijana mkono wako, wala usimtendee neno; kwa maana sasa ninajua ya kuwa unamcha Elohim, iwapo hukunizuilia mwanao, mwanao wa pekee."

Note:Isaka ndiye alikuwa mwana wa haki wa Abraham Kwa vile alizaliwa kuitimiza ahadi ya Elohim kupitia Kwa Sara mkewe(Mwanzo 17:18-19 Ibrahimu akamwambia Elohim, Lau kwamba Ishmaeli angeishi mbele yako.Elohim akasema, Sivyo, lakini Sara mkeo atakuzalia mwana wa kiume, nawe utamwita jina lake Isaka. Nami nitafanya agano langu imara kwake kuwa agano la milele kwa ajili ya uzao wake baada yake) . Elohim alikuwa amependezwa na isaka na Kwa hivyo akamtaka kuwa dhabihu kwake.

5. **Ni jambo lipi lilifanyika kudhihirisha Elohim alipendezwa na Abraham Kwa kutii na pia mahali pale palikuwa patakatifu kwake?**

Mwanzo 22:13. " Ibrahimu akainua macho yake, akaangalia, na tazama, kondoo mume yuko nyuma yake, amenaswa pembe zake katika kichaka. Basi Ibrahimu akaenda akamtwaa huyo kondoo, akamtoa awe sadaka ya kuteketezwa badala ya mwanawe."

6. **Ni ushuhuda upi twapata kuhusu mahali hapa?**

Mwanzo 22:14.(Kwa hakika kile mwanadamu alihitaji(dhabihu) ingepatika hapa.) "Ibrahimu akapaita mahali hapo Elohim-yire,kama watu wasemavyo hata leo,Katika mlima wa BWANA itapatikana."

7. **Ahadi ya Elohim ilimfuata huyu Isaka ama la?**

Mwanzo 17:19.(Agano la uridhi wa nchi ya kanani lilitimiziwa Isaka na uzao wake(Israeli) hii ni pamoja na mlima huu wa MORIA ambapo Elohim alitolewa dhabihu na Abraham na akaikubali. "Elohim akasema, Sivyo, lakini Sara mkeo atakuzalia mwana wa kiume, nawe utamwita jina lake Isaka. Nami nitafanya agano langu imara kwake kuwa agano la milele kwa ajili ya uzao wake baada yake."(Mwanzo 25:5-6).

8. **Uzao huu wa Isaka(wa Israeli) waliweza kumiliki mlima huu wa MORIA?**

2Mambo ya nyakati3:12 " Na bawa la kerubi la pili lilikuwa mikono mitano, likiufikilia ukuta wa nyumba; na bawa la pili mikono mitano, likishikana na bawa la kerubi la kwanza."

9. **Ni tukio lipi lilifanya hapa pakachaguliwa tena ili hekalu lijengwe?**

1Mambo ya nyakati 21:27-30. "Bwana naye akamwamuru malaika; naye akaurudisha upanga wake alani mwake tena. Wakati huo, Daudi alipoona ya

kwamba Bwana amemwitikia katika kiwanja cha Arauna, Myebusi, ndipo hutoa dhabihu huko. Kwa maana ile maskani ya Bwana, aliyoifanya Musa jangwani, na madhabahu ya sadaka ya kuteketezwa, vilikuwapo wakati huo mahali pa juu pa Gibeoni. Wala Daudi hakuweza kwenda mbele yake ili kumwuliza Elohim; kwa sababu aliona hofu kwa ajili ya upanga wa yule malaika wa Bwana."

**10.Daudi alitoa ushuhuda upi kuhusu mahali hapa?**

1 Mambo ya nyakati 22:1. "  Ndipo Daudi akasema, Hii ndiyo nyumba ya Bwana Elohim, na hii ndiyo madhabahu ya sadaka ya kuteketezwa kwa Israeli."

( Hapa ndipo  hekalu la kwanza na pia la pili lilinjengwa na Elohim akawa akitolewa dhabihu siku hizo zote.Juu ya mlima huu wa MORIA,ndipo Yahshua alisimama alipoingia katika hekalu na kufundisha injili ile ya kweli.(Mathayo 25:55).

**11.Ni ishara ipi ilionekana mlimani huu wakati Yahshua alikufa?**

Luka 23:44-45. "Hapo ilikuwa yapata saa sita, kukawa giza juu ya nchi yote hata saa kenda, jua limepungua nuru yake; pazia la hekalu likapasuka katikati."

(Yahshuah Messiah alitoa dhabihu iliyo kubalika akitimiza lile Elohim alikusudia alipo mwagiza Abrahamu kuchinja Isaka juu ya Mlima moria. Vivyo hivyo ndivyo Isaka alikuwa mfano wa  Yahshua akiwa mwana wapekee wa ahadi aliye pendwa sana na babake.(Mathayo 17:5,Wagalatia 3:16)

-(Warumi 4 draft a note explaining how isaacs sacrifice is similar to Yahshuah)

**12.Baada ya kifo chake Yahshua ni jambo lipi la kuhuzunisha liliufikia mlima huu?**

Mathayo 24:15. " Basi hapo mtakapoliona chukizo la uharibifu, lile lililonenwa na nabii Danieli, limesimama katika patakatifu (asomaye na afahamu)."  (Hili ni jengo la msikiti wa Al-Aqsa uliojengwa juu ya huu mlima baada ya Hekalu kubomolewa mwaka wa 70AD.)

13.**Hatima ya mlima huu ni ipi?**

Isaya 2:1-3 "Hili ni neno aliloliona Isaya mwana wa Amozi katika habari za Yuda na Yerusalemu.Na itakuwa katika siku za mwisho, mlima wa nyumba ya Bwana utawekwa imara juu ya milima, nao utainuliwa juu ya vilima; na mataifa yote watauendea makundi makundi.Na mataifa mengi watakwenda na kusema, Njoni, twende juu mlimani kwa Bwana, nyumbani kwa Elohim wa Yakobo, naye

atatufundisha njia zake, nasi tutakwenda katika mapito yake maana katika Sayuni itatoka sheria, na neno la Bwana katika Yerusalemu."

## KUFA NA KUFUFUKA KWA YAHSHUA

1. **Je, kuna ushahidi katika Agano la Kale kwamba Masihi alipaswa kufa?**

Isaya 53:5 - Bali alijeruhiwa kwa makosa yetu, alichubuliwa kwa maovu yetu; adhabu ya amani yetu ilikuwa juu yake, na kwa kupigwa kwake sisi tumepona.

Isaya 53:8-9 - Kwa kuonewa na kuhukumiwa aliondolewa; na maisha yake ni nani atakayeisimulia? Maana amekatiliwa mbali na nchi ya walio hai; alipigwa kwa sababu ya makosa ya watu wangu. Wakamfanyia kaburi pamoja na wabaya; na pamoja na matajiri katika kufa kwake; ingawa hakutenda jeuri, wala hapakuwa na hila kinywani mwake.

2. **Je, Masihi alisemaje kuhusu kufa na kufufuka kwake?**

Mathayo 16:21 - Tangu wakati huo Yahshuah alianza kuwaonya wanafunzi wake kwamba imempasa kwenda Yerusalemu, na kupata mateso mengi kwa wazee na wakuu wa makuhani, na waandishi, na kuuawa, na siku ya tatu kufufuka.

3. **Ni tukio lipi la kisheria lililokuwa likiendelea wakati wa kufa kwa Yahshua?**

Mambo ya Walawi 23:4-7 - Sikukuu za Bwana ni hizi, ni makusanyiko matakatifu, ambayo mtayapigia mbiu kwa nyakati zake. Mwezi wa kwanza, siku ya kumi na nne ya mwezi wakati wa jioni, ni Pasaka ya Bwana. Na siku ya kumi na tano ya mwezi ule ule ni sikukuu kwa Bwana ya mkate usiotiwa chachu; mtaila mikate isiyochachwa muda wa siku saba. Siku ya kwanza mtakuwa na kusanyiko takatifu msifanye kazi yo yote ya utumishi.

Mathayo 26:2 - Mnajua ya kuwa baada ya siku mbili itakuwa Pasaka, na Mwana wa Adamu atasalitiwa asulibiwe.

4. **Je, Masihi alikufa katika siku gani ya juma?**

Danieli 9:21 - Naam, nilipokuwa nikinena katika kuomba, mtu yule, Gabrieli, niliyemwona katika njozi hapo kwanza, akirushwa upesi, alinigusa panapo wakati wa dhabihu ya jioni.

Marko 15:42 - Hata ikiisha kuwa jioni, kwa sababu ni Maandalio, ndiyo siku iliyo kabla ya sabato.

5. **Katika juma alilokufa Yahshua kulikuwa na sabato ngapi?**

Luka 23:53-55 - Akaushusha, akauzinga sanda ya kitani, akauweka katika kaburi lililochongwa mwambani, ambalo hajalazwa mtu bado ndani yake. Na siku ile ilikuwa siku ya Maandalio, na sabato ikaanza kuingia. Na wale wanawake waliokuja naye toka Galilaya walifuata, wakaliona kaburi, na jinsi mwili wake ulivyowekwa.

6. **Kulingana na andiko hili Luka 23:54 tunaona kuna sabato nyingine kando na sabato ya amri, je; sabato hiyo ni ipi?**

Yohana 19:31 - Basi Wayahudi, kwa sababu ni Maandalio, miili isikae juu ya misalaba siku ya sabato, (maana sabato ile ilikuwa siku kubwa), walimwomba Pilato miguu yao ivunjwe, wakaondolewe.

7. **Masihi alikuwa akae muda wa siku ngapi kaburini?**

Mathayo 12:40 - Kwani kama vile Yona alivyokuwa siku tatu mchana na usiku katika tumbo la nyangumi, hivyo ndivyo Mwana wa Adamu atakavyokuwa siku tatu mchana na usiku katika moyo wa nchi.

8. **Je, Masihi alifufuka lini?**

Mathayo 28:1 - Hata sabato ilipokwisha, ikipambazuka siku ya kwanza ya juma, Mariamu Magdalene, na Mariamu yule wa pili, walikwenda kulitazama kaburi.

Mathayo 28:5-6 - Malaika akajibu, akawaambia wale wanawake, Msiogope ninyi; kwa maana najua ya kuwa mnamtafuta Yahshuah alibiwa. Hayupo hapa; kwani amefufuka kama alivyosema. Njoni, mpatazame mahali alipolazwa.

9. **Paulo anatoa ushuhuda upi kuhusu kufufuka kwa Masihi?**

1 Wakorintho 15:20 - Lakini sasa Messiah amefufuka katika wafu, limbuko lao waliolala.

10. **Kufa na kufufuka kwa Yahshua kuna faida gani kwetu?**

1 Timotheo 1:15 - Ni neno la kuaminiwa, tena lastahili kukubalika kabisa, ya kwamba Messiah Yahshuah alikuja ulimwenguni awaokoe wenye dhambi; ambao wa kwanza wao ni mimi.

Maelezo - Kufa na kufufuka kwa Yahshua ni kiini cha wokovu wa Elohim kwa wanadamu, na linathibitishwa na unabii wa Agano la Kale (Isaya 53:5, 8-9) na mafundisho ya Yahshua mwenyewe (Mathayo 16:21). Kifo chake kilitokea wakati wa Sikukuu ya Pasaka, na alikaa kaburini kwa siku tatu kama alivyosema (Mathayo 12:40). Alifufuka kutoka kwa wafu mapambazuko ya siku ya kwanza ya wiki (Mathayo 28:1, 5-6), na Paulo anasisitiza kuwa kupitia kufufuka kwake, Masihi alishinda kifo na alileta tumaini la uzima wa milele (1 Wakorintho 15:20, 1 Timotheo 1:15), akiwa limbuko la waliolala.

## SIKUKUU YA 'GOOD FRIDAY NA EASTER SUNDAY'

1. **Je Yahshua alikuja duniani na akafa?**

Yohana 3:16 - Kwa maana jinsi hii Elohim aliupenda ulimwengu, hata akamtoa Mwanawe pekee, ili kila mtu amwaminiye asipotee, bali awe na uzima wa milele.

2. **Alikufa siku ipi ya Juma?**

Danieli 9:27 - Naye atafanya agano thabiti na watu wengi kwa muda wa juma moja; na kwa nusu ya juma hiyo ataikomesha sadaka na dhabihu; na mahali pake litasimama chukizo la uharibifu; na hivyo, hata ukomo, na ghadhabu iliyokusudiwa imemwagwa juu yake mwenye kuharibu.

Maelezo - Yahshua ndiye alitumwa na Elohim, ili aje awe dhabihu moja ya kutosha, akazikomesha dhabihu zote ambazo zilikuwa zikitolewa kila mwaka, Waebrania 9:11-12, Lakini Messiah akiisha kuja, aliye kuhani mkuu wa mambo mema yatakayokuwapo, kwa hema iliyo kubwa na kamilifu zaidi, isiyofanyika kwa mikono, maana yake, isiyo ya ulimwengu huu, wala si kwa damu ya mbuzi na ndama, bali kwa damu yake mwenyewe aliingia mara moja tu katika Patakatifu, akiisha kupata ukombozi wa milele. Haya yalifanyika punde tu kitama cha hekalu kilikatika na akakata roho.

Luka 23:45 Jua limepungua nuru yake; pazia la hekalu likapasuka katikati.

3. **Masihi alipeana muujiza upi mkuu unaohusu kufufuka kwake? Alikaa kaburini siku ngapi?**

Mathayo 12:40 - Kwani kama vile Yona alivyokuwa siku tatu mchana na usiku katika tumbo la nyangumi, hivyo ndivyo Mwana wa Adamu atakavyokuwa siku tatu mchana na usiku katika moyo wa nchi.

Yona1:17 - Bwana akaweka tayari samaki mkubwa ili ammeze Yona, naye Yona akawa ndani ya tumbo la samaki yule muda wa siku tatu, mchana na usiku.

Maelezo. Messiah, alidhibitisha umasihi wake, na nguvu na mamlaka ya baba yake kwa kukaa kaburini siku tatu ; yaani masaa Sabini na mawili kwani siku moja, kipindi cha giza na cha meanga ni cha masaa ishirini na manne, Yohana 11:9

4. **Alifufuka wakati gani wa siku?**

Mathayo 28 :1, 5-6 - Hata sabato ilipokwisha, ikipambazuka siku ya kwanza ya juma, Mariamu Magdalene, na Mariamu yule wa pili, walikwenda kulitazama kaburi.Malaika akajibu, akawaambia wale wanawake, Msiogope ninyi; kwa maana najua ya kuwa mnamtafuta Yahshuah aliYahshuahlibiwa.Hayupo hapa; kwani amefufuka kama alivyosema. Njoni, mpatazame mahali alipolazwa.

5. **Yahshua alikufa tarehe ipi ya mwaka?**

Yohana 18:28 - Kisha wakamchukua Yahshua kutoka kwa Kayafa mpaka Praitorio, nayo ikawa alfajiri;lakini wao wenyewe hawakuingia ndani ya ile praitorio,wasije wakanajisika,bali wapate kuila Pasaka.” Kutoka 12:18 “Mwezi wa kwanza, siku ya mwezi kumi na nne, wakati wa jioni, mtakula mikate isiyochachwa, hata siku ya mwezi ishirini na moja jioni.

Maelezo - Easter, husherehekewa, siku ya Jumapili, ambayo inafuata mwezi mzima ‘full moon’ katika mwezi wa Aprili, hii anayesherehekewa, hukisiwa kuwa alikufa Friday, na kufufuka Sunday baada ya siku moja na nusu tu, ilhali Yahshua alikufa Wednesday, na kufufuka baada ya Sabato kuisha yaani Saturday evening, baada ya siku tatu. Alikufa tarehe kumi na nne mwezi wa Abib. Hii ni dhihirisho tosha ya kuwa, Sio mokozi wetu Yahshua ambaye husherehekewa Easter.

Maelezo - Easter, ni sherehe ya kipagani, ambayo ilikuwa ni ya kumwabudu Elohim wao wa kike aitwaye estero saxon goddess. Waliamini kuwa, Elohim huyu ndiye alibariki uzazi na kuleta mazao kwa watu na ardhi pia. Kumbuka kwamba, Easter haina uhusiano wowote ma Messiah, kwani, sherehe hii ya uasi na machukizo kwa Elohim, ilianza kusherehekewa muda mrefu sana hata kabla ya kuzaliwa kwa mokozi wetu Yahshua. Sherehe hii iliingizwa katika ukristiano na mfalme muovu wa Kirumi aitwaye Constantine mnamo mwaka wa 325AD.

Akazileta desturi nyingi za kipagani na za Wamisri ili kutengeneza ushirika mmoja kwa jina Ukristiano.

6. **Je Elohim amekubali uabudu wa sanamu kama vile Easter?**

Isaya 42:8 “Mimi ni Bwana; ndilo jina langu; na utukufu wangu sitampa mwingine, wala sitawapa sanamu sifa zangu.”Isaya 48:11 “Kwa ajili ya nafsi yangu, kwa ajili ya nafsi yangu, nitatenda haya; je! Litiwe unajisi jina langu? Wala sitampa mwingine utukufu wangu.”

7. **Waabudu sanamu watahukumiwa?**

Ufunuo wa Yohana 21:8 - Bali waoga, na wasioamini, na wachukizao, na wauaji, na wazinzi, na wachawi, na hao waabuduo sanamu, na waongo wote, sehemu yao ni katika lile ziwa liwakalo moto na kiberiti. Hii ndiyo mauti ya pili.

Warumi 1:32 - ambao wakijua sana hukumu ya haki ya , ya kwamba wayatendao hayo wamestahili mauti, wanatenda hayo, wala si hivyo tu, bali wanakubaliana nao wayatendao.

8. **Tunastahili kufanya nini ili kuondokea dhambi hii ya uabudu sanamu?**

Matendo ya Mitume 2:37-38

Walipoyasikia haya wakachomwa mioyo yao, wakamwambia Petro na mitume wengine, Tutendeje, ndugu zetu?Petro akawaambia, Tubuni mkabatizwe kila mmoja kwa jina lake Yahshua Messiah, mpate ondoleo la dhambi zenu, nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu.

## WATU WA MATAIFA HUPANDIKIZWA VIPI

Utangulizi - Kuna njia moja pekee Baba yetu wa Mbinguni ameiweka wazi kuhusu watu wa mataifa kuupata ufalme wa milele. Ni vizuri kusoma kwa makini kuhusu njia hii. Zaburi 119:105.

Zaburi 119:105 - Neno lako ni taa ya miguu yangu, Na mwanga wa njia yangu.

1. **Katika kitabu cha Wagalatia 3:16(sehemu ya kwanza) mtume Paulo anasema ahadi ilipeanwa kwa nani? Linganisha na Mwanzo 12:7**

Wagalatia 3:16 (a) - Basi ahadi zilinenwa kwa Ibrahimu na kwa mzao wake.

Mwanzo 12:7 - Bwana akamtokea Abramu, akasema, Uzao wako nitawapa nchi hii. Naye huko akamjengea madhabahu Bwana aliyemtokea.

2. **Ni kwa sababu gani ahadi hii ilipeanwa? Mwanzo 26:5.**

Mwanzo 26:5 - Kwa sababu Ibrahimu alisikia sauti yangu, akayahifadhi maagizo yangu, na amri zangu, na hukumu zangu, na sheria zangu.

Maelezo - Ijapokuwa wakati huu amri kumi hazikuwa zimepeanwa kwa mkono wa musa, tunaona Elohim alimhesabia Ibrahimu haki kwa kuzihifadhi amri zake.

3. **Sehemu ya mwisho ya Wagalatia 3:16, Paulo anamtaja mwokozi kuwa mzao ya Abrahamu?**

Wagalatia 3:16 (b) - Hasemi, Kwa wazao, kana kwamba ni wengi, bali kana kwamba ni mmoja, Kwa mzao wako, yaani, Kristo.

4. **Kulingana na Warumi 11:1-2, Je! Elohim aliutupilia mbali hii mzao ambayo ni wana wa Israeli? ni jukumu gani wamepatiwa? Warumi 3:1-2, Warumi 9:4-5**

Warumi 11:1-2 - Basi, nauliza, Je! Elohim aliwasukumia mbali watu wake? Hasha! Kwa kuwa mimi nami ni Mwisraeli, mmoja wa wazao wa Ibrahimu, mtu wa kabila ya Benyamini. 2 Elohim hakuwasukumia mbali watu wake aliowajua tokea awali. Au hamjui yale yaliyonenwa na maandiko juu ya Eliya? Jinsi anavyowashitaki Waisraeli mbele za Elohim,

Warumi 3:1-2 - Basi Myahudi ana ziada gani? Na kutahiriwa kwafaa nini? 2 Kwafaa sana kwa kila njia. Kwanza kwa kuwa wamekabidhiwa mausia ya Elohim.

Warumi 9:4-5 - ambao ni Waisraeli, wenye kule kufanywa wana, na ule utukufu, na maagano, na kupewa torati, na ibada ya Elohim, na ahadi zake; ambao mababu ni wao, na katika hao alitoka Kristo kwa jinsi ya mwili. Ndiye aliye juu ya mambo yote, Elohim, mwenye kuhimidiwa milele. Amina.

5. **Ni ushauri upi Paulo anawapa watu wa mataifa waliopandikizwa kwa jamii ya Israeli?**

Warumi 11:15-17,19-20 - Maana ikiwa kutupwa kwao kumeleta upatanisho kwa ulimwengu, je! Kukubaliwa kwao kutakuwa nini kama si uhai baada ya kufa? 16 Tena malimbuko yakiwa matakatifu, kadhalika na donge lote; na shina likiwa takatifu, matawi nayo kadhalika. 17 Lakini iwapo matawi mengine yamekatwa, na wewe mzeituni mwitu ulipandikizwa kati yao, ukawa mshirika wa shina la

mzeituni na unono wake, 19 Basi utasema, Matawi yale yalikatwa kusudi ili nipandikizwe mimi. 20 Vema. Yalikatwa kwa kutokuamini kwao, na wewe wasimama kwa imani yako. Usijivune, bali uogope.

Maelezo - Mataifa hupandikizwa kinyume cha asili,Warumi 11:24. Kama jinsi tawi la ndimu linapandikizwa kwa mchungwa huzaa machungwa na sio ndimu tena,vivyo hivyo mataifa wakipandikizwa kwa familia ya Abrahamu huonekana kama wayahudi. Kama jinsi tawi la ndimu haliwezi kuwa ndimu tena ama kuzaa ndimu.

6. **Kupandikizwa huku hufanyika kwa mwili ama kwa roho? Na ni kwa njia ipi?**

Warumi 2:28-29 - Maana yeye si Myahudi aliye Myahudi kwa nje tu, wala tohara siyo ile ya nje tu katika mwili; bali yeye ni Myahudi aliye Myahudi kwa ndani, na tohara ni ya moyo, katika roho, si katika andiko; ambaye sifa yake haitoki kwa wanadamu bali kwa Elohim.

7. **Tohara hii isiyo ya mwili bali ya roho hufanyika kwa njia gani? wakolosai 2:11-13 Ni kitendo kipi hufanyika katika mwili? Warumi 6:3-4**

Wakolosai 2:11-13 - Katika yeye mmetahiriwa kwa tohara isiyofanyika kwa mikono, kwa kuuvua mwili wa nyama, kwa tohara ya Kristo. Mkazikwa pamoja naye katika ubatizo; na katika huo mkafufuliwa pamoja naye, kwa kuziamini nguvu za Elohim aliyemfufua katika wafu. Na ninyi mlipokuwa mmekufa kwa sababu ya makosa yenu na kutokutahiriwa kwa mwili wenu, aliwafanya hai pamoja naye, akiisha kutusamehe makosa yote;

Warumi 6:3-4 - Hamfahamu ya kuwa sisi sote tuliobatizwa katika Kristo Yahshuah tulibatizwa katika mauti yake? Basi tulizikwa pamoja naye kwa njia ya ubatizo katika mauti yake, kusudi kama Kristo alivyofufuka katika wafu kwa njia ya utukufu wa Baba, vivyo hivyo na sisi tuenende katika upya wa uzima.

8. **Ni lazima mtu abatizwe? Yohana 3:3, Hubatizwa na nini? Yohana 3:4-5**

Yohana 3:3-5 -Yahshuah akajibu, akamwambia, Amin, amin, nakuambia, Mtu asipozaliwa mara ya pili, hawezi kuuona ufalme wa Elohim. Nikodemo akamwambia, Awezaje mtu kuzaliwa, akiwa mzee? Aweza kuingia tumboni mwa mamaye mara ya pili akazaliwa? Yahshuah akajibu, Amin, amin, nakuambia, Mtu asipozaliwa kwa maji na kwa Roho, hawezi kuuingia ufalme wa Elohim.

9. **Ni maji kiasi gani yanakubalika kubatiza katika maandiko matakatifu? Yohana 3:6,23, Matendo ya mitume 8:36**

Yohana 3:6 Kilichozaliwa kwa mwili ni mwili; na kilichozaliwa kwa Roho ni roho.

23 Yohana naye alikuwa akibatiza huko Ainoni, karibu na Salimu, kwa sababu huko kulikuwa na maji tele; na watu wakamwendea, wakabatizwa.

10. **Mtu akishapata muhuri huu wa tohara, anafaa kufanya nini ili awe na hakikisho la kurithi pamoja na Abrahamu?**

Mathayo 19:17 - Akamwambia Kwani kuniuliza habari ya wema? Aliye mwema ni mmoja. Lakini ukitaka kuingia katika uzima, zishike amri.

Yohana 14:21 - Yeye aliye na amri zangu, na kuzishika, yeye ndiye anipendaye; naye anipendaye atapendwa na Baba yangu; nami nitampenda na kujidhihirisha kwake.

1 Yohana 2:3-4 - Na katika hili twajua ya kuwa tumemjua yeye, ikiwa tunashika amri zake. Yeye asemaye, Nimemjua, wala hazishiki amri zake, ni mwongo, wala kweli haimo ndani yake.

Hitimisho - Kwa sababu ya kuwadharau wayahudi,walimu wengi hawependi kufunza kuhusu njia hii ya kipekee inayoweza kumfanya mtu wa mataifa kuwa mrithi pamoja na Abrahamu.

## BINTI ZAYUNI

1. **Katika maandiko, ni mabinti wangapi wametajwa?**




Ufunuo wa Yohana 12:1 - Na ishara kuu ilionekana mbinguni; mwanamke aliyevikwa jua, na mwezi ulikuwa chini ya miguu yake, na juu ya kichwa chake taji ya nyota kumi na mbili.

Ufunuo wa Yohana 17:1 - Akaja mmoja wa wale malaika saba, wenye vile vitasa saba, akanena nami, akisema, Njoo huku, nitakuonyesha hukumu ya yule kahaba mkuu aketiye juu ya maji mengi.

Ufunuo wa Yohana 17:4-5 - Na mwanamke yule alikuwa amevikwa nguo ya rangi ya zambarau, na nyekundu, amepambwa kwa dhahabu, na kito cha thamani, na lulu, naye alikuwa na kikombe cha dhahabu mkononi mwake, kilichojawa na machukizo, na machafu ya uasherati wake. Na katika kipaji cha uso wake alikuwa na jina limeandikwa, la siri, BABELI MKUU, MAMA WA MAKAHABA NA MACHUKIZO YA NCHI.

2. **Binti wa Ufunuo wa Yohana 12:1 amepewa jina lipi?**

Yeremia 6:2 - Binti Sayuni aliye mzuri, **mwororo** …

Tazama kiingereza (kjv)

Jeremiah 6:2 - I have likened the daughter of Zion to a comely and delicate woman. (Ni Binti anayependeza)

3. **Jina lingine lipi amepewa binti wa Ufunuo wa Yohana 17:5?**

Zaburi 137:8 - Ee binti Babeli, uliye karibu na kuangamia, heri atakayekupatiliza, ulivyotupatiliza sisi.

4. **Katika maandiko, binti amefananishwa na nini?**

Waefeso 5:22-24 - Enyi wake, watiini waume zenu kama kumtii Bwana wetu. Kwa maana mume ni kichwa cha mkewe, kama Masihi naye ni kichwa cha Kanisa; naye ni mwokozi wa mwili. Lakini kama vile Kanisa limtiivyo Masihi, vivyo hivyo wake nao wawatii waume zao katika kila jambo.

Waefeso 5:32 - Siri hiyo ni kubwa; ila mimi nanena habari ya Masihi na Kanisa.

5. **Ishara zipi za mbinguni amevikwa binti Zayuni?**

Ufunuo wa Yohana 12:1 - Na ishara kuu ilionekana mbinguni; mwanamke aliyevikwa jua, na mwezi ulikuwa chini ya miguu yake, na juu ya kichwa chake taji ya nyota kumi na mbili.

6. **Kwa nini kanisa la kweli limefananishwa na binti?**

2 Wakorintho 11:2 - Maana nawaonea wivu, wivu wa Elohim; kwa kuwa naliwaposea mume mmoja, ili nimletee Masihi bikira safi.

Waefeso 5:25-27 - Enyi waume, wapendeni wake zenu, kama Masihi naye alivyolipenda Kanisa, akajitoa kwa ajili yake; ili makusudi alitakase na kulisafisha

kwa maji katika neno; apate kujiletea Kanisa tukufu, lisilo na ila wala kunyanzi wala lo lote kama hayo; bali liwe takatifu lisilo na mawaa.

7. **Mavazi aliyovikwa binti wa Ufunuo wa Yohana 12:1 yanasimamia nini?**

Ufunuo wa Yohana 19:7-8 - Na tufurahi, tukashangilie, tukampe utukufu wake; kwa kuwa arusi ya Mwana-Kondoo imekuja, na mkewe amejiweka tayari. Naye amepewa kuvikwa kitani nzuri, ing'arayo, safi; kwa maana kitani nzuri hiyo ni matendo ya haki ya watakatifu.

8. **Haki ya watakatifu inatokana na nini?**

Zaburi 119:172 - Ulimi wangu na uiimbe ahadi yako, maana maagizo yako yote ni ya haki.

9. **Nini kinamtenganisha binti Zayuni na binti Babeli?**

Ufunuo wa Yohana 12:17 - Joka akamkasirikia yule mwanamke, akaenda zake afanye vita juu ya wazao wake waliosalia, wazishikao amri za Elohim, na kuwa na ushuhuda wa Yahshua Masihi.

10. **Mwishowe, binti Zayuni ameahidiwa nini?**

Mika 4:8 - Na wewe, Ee mnara wa kundi, kilima cha binti Sayuni, utajiliwa; naam, mamlaka ya kwanza yatakuja, ufalme wa binti Yerusalemu.

Maelezo - Mafunzo haya yanalinganisha picha ya kibiblia ya Binti Zayuni na Binti Babeli kwa kutumia vifungu kutoka kitabu cha Ufunuo na maandiko mengine. Binti Zayuni, kama inavyoonyeshwa katika Ufunuo 12:1, ni mwanamke aliyevikwa jua, akiwa na mwezi chini ya miguu yake na taji ya nyota kumi na mbili, ikionyesha usafi, haki, na kibali cha Elohim. Hii inatofautiana na Binti Babeli, aliyeelezwa katika Ufunuo 17:5 kama mwanamke aliyevaa mavazi ya kifahari lakini yenye maovu. Mafunzo haya yanasisitiza kuwa Kanisa linafananishwa na Binti Zayuni kama bibi arusi anayeangojea kurudi kwa Yahshua, na matendo ya haki ya watakatifu yanachukuliwa kama mavazi safi. Tofauti kuu kati ya Binti Zayuni na Binti Babeli ni utii kwa amri za Elohim na ushuhuda wa Yahshua Masihi. Mwishowe, Binti Zayuni ameahidiwa ushindi na ufalme wa Elohim, na Kanisa linapaswa kubaki linaaminika, likitii na kujitenga na maovu ya Binti Babeli, likingojea kurudi kwa Masihi.

## FALME NNE; MWANAUME WA CHUMA

1. **Mfalme Nebukadneza aliota ndoto gani ya ajabu?**

Danieli 2:31-32 - Wewe, Ee Mfalme, uliona, na tazama, sanamu kubwa sana. Sanamu hii, iliyokuwa kubwa sana, na mwangaza wake mwingi sana, ilisimama mbele yako; na umbo lake lilikuwa lenye kutisha. Na sanamu hii kichwa chake kilikuwa ni cha dhahabu safi; kifua chake na mikono yake ni ya fedha; tumbo lake na viuno vyake ni vya shaba.




2. **Kwa nini ndoto hii ililetwa kwa mfalme?**

Danieli 2:29 - Wewe, Ee mfalme, mawazo yako yaliingia moyoni mwako kitandani pako ya mambo yatakayokuwa halafu; na yeye afunuaye siri amekujulisha mambo yatakayokuwa.

3. **Ni nani pekee yake angeweza kufasiri ndoto?**

Danieli 1:17 - Basi, kwa habari za hao vijana wanne, Elohim aliwapa maarifa na ujuzi katika elimu na hekima; Danieli naye alikuwa na ufahamu katika maono yote, na ndoto.

Danieli 2:26-29 - Mfalme akajibu, akamwambia Danieli, aliyekuwa akiitwa Belteshaza, Je! Waweza kunijulisha ile ndoto niliyoiona, na tafsiri yake. Danieli akajibu mbele ya mfalme, akasema, Ile siri aliyoiuliza mfalme, wenye hekima hawawezi kumfunulia mfalme; wala wachawi, wala waganga, wala wanajimu; lakini yuko Elohim mbinguni afunuaye siri, naye amemjulisha mfalme Nebukadreza mambo yatakayokuwa siku za mwisho. Ndoto yako, na njozi za kichwa chako ulizoziona kitandani pako, ni hizi; Wewe, Ee mfalme, mawazo yako yaliingia moyoni mwako kitandani pako ya mambo yatakayokuwa halafu; na yeye afunuaye siri amekujulisha mambo yatakayokuwa.

4. **Kwa nini Danieli alipewa ufunuo wa ndoto?**

Danieli 2:30 - Lakini mimi, sikufunuliwa siri hii kwa sababu ya hekima iwayo yote niliyo nayo zaidi ya watu wengine walio hai, bali kusudi mfalme afunuliwe ile tafsiri, nawe upate kujua mawazo ya moyo wako.

**5. Ni nini kilitokea kwa sanamu hii kubwa ya kutisha?**

Danieli 2:34-35 - Nawe ukatazama hata jiwe likachongwa bila kazi ya mikono, nalo jiwe hilo likaipiga sanamu miguu yake, iliyokuwa ya chuma na udongo, likaivunja vipande vipande. Ndipo kile chuma, na ule udongo, na ile shaba, na ile fedha, na ile dhahabu, vilivunjwa vipande vipande pamoja vikawa kama makapi ya viwanja vya kupepetea wakati wa hari; upepo ukavipeperusha hata pasionekane mahali pake; na lile jiwe lililoipiga hiyo sanamu likawa milima mikubwa, likaijaza dunia yote.

**6. Tafsiri ilikuwa nini?**

- Danieli 2:36-43 - Hii ndiyo ile ndoto, nasi tutaihubiri tafsiri yake mbele ya mfalme. Wewe, Ee mfalme, u mfalme wa wafalme, na Elohim wa mbinguni amekupa ufalme, na uwezo, na nguvu, na utukufu; na kila mahali wakaapo wanadamu, wanyama wa kondeni na ndege wa angani amewatia mkononi mwako, naye amekumilikisha juu ya hao wote; wewe u kichwa kile cha dhahabu. Na baada ya zamani zako utainuka ufalme mwingine mdogo kuliko wewe; na ufalme mwingine wa tatu wa shaba, utakaoitawala dunia yote. Na ufalme wa nne utakuwa na nguvu mfano wa chuma; kwa maana chuma huvunja vitu vyote na kuvishinda; na kama chuma kisetavyo vitu hivi vyote, ndivyo utakavyovunja-vunja na kuseta. Na kama vile ulivyoziona hizo nyayo za miguu na vidole vyake, kuwa nusu udongo wa mfinyanzi, na nusu chuma, ufalme ule utakuwa ufalme uliogawanyika; lakini ndani yake zitakuwako nguvu za chuma, kama vile ulivyoona kile chuma kimechanganyika na udongo wa matope. Na kama vidole vya zile nyayo vilikuwa nusu chuma na nusu udongo, kadhalika ufalme ule utakuwa nusu yake una nguvu, na nusu yake umevunjika. Na kama vile ulivyokiona kile chuma kimechanganyika na udongo wa matope, watajichanganya nafsi zao kwa mbegu za wanadamu; lakini hawatashikamana, kama vile chuma kisivyoshikamana na udongo.

Kumbuka: Hizi ni falme nne ambazo zingetokea, Danieli alimwambia Nebukadneza kuwa yeye ndiye kichwa cha dhahabu wakati wa ufalme wa kwanza wa Babeli. Baada yake kulikuwa na falme tatu. Falme hizi ni; Umedi-Uajemi, Ufalme wa Ugiriki na Ufalme wa Kirumi kama ufalme wa nne. Tunaishi wakati wa Ufalme huu wa mwisho chini kabisa kwenye vidole vya miguu. Hili ndilo neno la hakika la unabii ambalo lilitabiriwa miaka mingi nyuma na kutimia, hizi zote ni falme za mataifa. Kati ya hawa ni wazi wengine walikuwa na nguvu na wengine walikuwa dhaifu kama tunavyoona katika (Danieli 2:33 - miguu yake ni ya chuma; na nyayo za miguu yake nusu ya chuma na nusu ya udongo).

**7. Jiwe lililompiga mtu wa chuma liliwakilisha nini?**

Danieli 2:44-45 - Na katika siku za wafalme hao Elohim wa mbinguni atausimamisha ufalme ambao hautaangamizwa milele, wala watu wengine hawataachiwa enzi yake; bali utavunja falme hizi zote vipande vipande na kuziharibu, nao utasimama milele na milele. Na kama vile ulivyoona ya kuwa jiwe lilichongwa mlimani bila kazi ya mikono, na ya kuwa lilivunja-vunja kile chuma, na ile shaba na ule udongo, na ile fedha, na ile dhahabu; basi Elohim aliye mkuu amemjulisha mfalme mambo yatakayokuwa baadaye; na ndoto hii ni ya hakika, na tafsiri yake ni thabiti.

**8. Mfalme Nebukadneza alielewa nini?**

Danieli 2:47 - Mfalme akajibu, akamwambia Danieli, Hakika Elohim wenu ndiye Elohim wa miungu, na Bwana wa wafalme, awezaye kufumbua siri, kwa kuwa wewe uliweza kuifumbua siri hii.

Maelezo - Mfalme alifahamu kuwa si Danieli aliyeifumbua ndoto hii bali Elohim. Na ndio maana aliweza kumsifu Elohim kama bwana wa Bwana na mfalme wa wafalme.

**9. Je, ufalme huu ambao ni wa tano utakuja kweli?**

Ufunuo wa Yohana 19:11-20 - Kisha nikaziona mbingu zimefunuka, na tazama, farasi mweupe, na yeye aliyempanda, aitwaye Mwaminifu na Wa-kweli, naye kwa haki ahukumu na kufanya vita. Na macho yake yalikuwa kama mwali wa moto, na juu ya kichwa chake vilemba vingi; naye ana jina lililoandikwa, asilolijua mtu ila yeye mwenyewe. Naye amevikwa vazi lililochovywa katika damu, na jina lake aitwa, Neno la Elohim. Na majeshi yaliyo mbinguni wakamfuata, wamepanda farasi weupe na kuvikwa kitani nzuri, nyeupe, safi. Na upanga mkali hutoka kinywani mwake ili awapige mataifa kwa huo. Naye atawachunga kwa fimbo ya chuma, naye anakanyaga shinikizo la mvinyo ya ghadhabu ya hasira ya Elohim Mwenyezi. Naye ana jina limeandikwa katika vazi lake na paja lake, MFALME WA WAFALME, NA BWANA WA MABWANA. Kisha nikaona malaika mmoja amesimama katika jua; akalia kwa sauti kuu, akiwaambia ndege wote warukao katikati ya mbingu, Njoni mkutane kwa karamu ya Elohim iliyo kuu; mpate kula nyama ya wafalme, na nyama ya majemadari, na nyama ya watu hodari, na nyama ya farasi na ya watu wawapandao, na nyama ya watu wote, waungwana kwa watumwa, wadogo kwa wakubwa. Kisha nikamwona huyo mnyama, na wafalme wa nchi, na majeshi yao, wamekutana kufanya vita na yeye aketiye juu ya farasi

yule, tena na majeshi yake. Yule mnyama akakamatwa, na yule nabii wa uongo pamoja naye, yeye aliyezifanya hizo ishara mbele yake, ambazo kwa hizo aliwadanganya watu wale walioipokea ile chapa ya huyo mnyama, nao walioisujudia sanamu yake; hao wawili wakatupwa wangali hai katika lile ziwa la moto liwakalo kwa kiberiti.

**10. Tunapaswa kusali jinsi gani?**

Mathayo 6:9-10 - Basi ninyi salini hivi; Baba yetu uliye mbinguni, Jina lako litukuzwe, Ufalme wako uje, Mapenzi yako yatimizwe, hapa duniani kama huko mbinguni.

Ufunuo wa Yohana 22:20-21 - Yeye mwenye kuyashuhudia haya asema, Naam; naja upesi. Amina; na uje, Bwana Yahshua. Neema ya Bwana Yahshua na iwe pamoja nanyi nyote. Amina.

Maelezo - Somo hili linaeleza ndoto ya Mfalme Nebukadneza kuhusu sanamu yenye sehemu za dhahabu, fedha, shaba, chuma, na mchanganyiko wa chuma na udongo (Danieli 2:31-32), ikiwakilisha falme nne kuu za Babeli, Umedi-Uajemi, Ugiriki, na Kirumi (Danieli 2:36-43). Ndoto hii ilionyesha mpango wa Elohim kwa historia ya mataifa na hitimisho lake na Ufalme wa Elohim wa milele, ulioashiriwa na jiwe lililoipiga sanamu na kuwa milima mikubwa (Danieli 2:44-45). Ndoto hii inathibitisha utawala wa Elohim na unabii wa kuja kwa Ufalme wa Masihi. Tunaitwa kujiandaa kwa imani, tukisali kwa bidii ili kushiriki utukufu wa Ufalme huo wa milele.

## MAONO YA DANIELI SURA YA SABA

1. **Baada ya kifo cha Nebukadneza ni nani alitawala Babeli?**

Danieli 5:18 - Kwa habari zako, Ee mfalme, Elohim Aliye juu alimpa Nebukadreza, baba yako, ufalme, na ukuu, na fahari, na utukufu;
- Danieli 5:22 - Na wewe, mwanawe, Ee Belshaza, hukujinyenyekeza moyo wako, ijapokuwa ulijua hayo yote.

2. **Katika mwaka wa kwanza wa utawala wa Belshaza Danieli aliona nini?**

Danieli 7:1-2 - Katika mwaka wa kwanza wa Belshaza, mfalme wa Babeli, Danieli aliona ndoto, na maono ya kichwa chake, kitandani mwake; basi akaiandika ndoto,

akatoa habari ya jumla ya mambo hayo. Danieli akanena, akisema, Naliona katika maono yangu wakati wa usiku; na tazama, hizo pepo nne za mbinguni zilivuma kwa nguvu juu ya bahari kubwa.

3. **Upepo unawakilisha nini katika unabii?**

Yeremia 23:19-20 - Tazama, tufani ya BWANA, yaani, ghadhabu yake, imetokea; ni dhoruba ya kisulisuli; itapasuka, na kuwaangukia waovu vichwani. Hasira ya BWANA haitarudi, hata atakapokwisha kuyatimiza makusudi ya moyo wake; katika siku za mwisho mtalifahamu neno hili kabisa.

Yeremia 25:32-33 - BWANA wa majeshi asema hivi, Tazama, uovu utatokea toka taifa hata taifa, na tufani kuu itainuliwa toka pande za mwisho wa dunia. Na waliouawa na BWANA siku ile watakuwapo, toka upande mmoja wa dunia hata upande wa pili; hawataliliwa, wala kukusanywa, wala kuzikwa; watakuwa samadi juu ya uso wa nchi.

4. **Upepo ulionekana ukivuma juu ya ile bahari kuu, Je! bahari inasimamia nini katika unabii?**

Ufunuo wa Yohana 17:15 - Kisha akaniambia, Yale maji uliyoyaona, hapo aketipo yule kahaba, ni jamaa na makutano na mataifa na lugha.

5. **Ni nini kilitokea baharini?**

Danieli 7:3 - Ndipo wanyama wakubwa wanne wakatoka baharini, wote wa namna mbalimbali.

6. **Mnyama anawakilisha nini katika unabii?**

Danieli 7:17 - Wanyama hao wakubwa walio wanne ni wafalme wanne watakaotokea duniani.

Maelezo - Wakati pepo nne zinapovuma juu zilionekana zikivuma juu ya bahari kuu, yaani kutoka Kaskazini hadi Kusini na kutoka mashariki hadi Magharibi, hii ina maana kwamba kulikuwa na vita kubwa, Mataifa walikuwa wakijitahidi kutawala na kukatokea falme nne zinazowakilishwa na hayawani wanne. Pepo nne zilizovuma duniani zinazowakilishwa na wanyama wanne

**7. Mfano wa mnyama wa kwanza au ufalme ilikuwa nini?**




Danieli 7:4 - Wa kwanza alikuwa kama simba, naye alikuwa na mabawa ya tai; nikatazama, hata mabawa yake yakafutuka manyoya, akainuliwa katika nchi, akasimamishwa juu kwa miguu miwili kama mwanadamu; naye akapewa moyo wa kibinadamu.

Maelezo - Simba ni mfalme wa nyika, anapoguruma wanyama wote wanaogopa, hivi ndivyo ufalme wa Babeli ulikuwa chini ya Nebukadneza. Alikuwa mfalme mkuu na mwenye nguvu akitawala Mataifa mengi.

**8. Nini kilitokea kwa mabawa ya simba?**

Danieli 7:4 sehemu ya kwanza - Wa kwanza alikuwa kama simba, naye alikuwa na mabawa ya tai; nikatazama, hata mabawa yake yakafutuka manyoya.

**9. Maana ya kufutuka manyoya ya mabawa ya Simba huyu ni nini?**

Danieli 4:25 - ya kuwa utafukuzwa mbali na wanadamu, na makao yako yatakuwa pamoja na wanyama wa kondeni, nawe utalazimishwa kula majani kama ng'ombe, nawe utatiwa maji kwa umande wa mbinguni, na nyakati saba zitapita juu yako; hata utakapojua ya kuwa Aliye juu ndiye anayemiliki katika ufalme wa wanadamu, naye humpa yeye amtakaye, awaye yote.

Danieli 4:31-33- Hata neno lile lilipokuwa katika kinywa cha mfalme, sauti ilikuja kutoka mbinguni, ikisema, Ee mfalme Nebukadreza, maneno haya unaambiwa wewe; Ufalme huu umeondoka kwako.Nawe utafukuzwa mbali na wanadamu, na makao yako yatakuwa pamoja na wanyama wa kondeni; utalishwa majani kama ng'ombe, na nyakati saba zitapita juu yako, hata utakapojua ya kuwa Aliye juu ndiye anayemiliki katika ufalme wa wanadamu, naye humpa amtakaye, awaye yote. Saa iyo hiyo jambo hilo likatimizwa, likampata Nebukadreza; alifukuzwa mbali na wanadamu, akala majani kama ng'ombe, na mwili wake ulilowa maji kwa umande wa mbinguni, hata nywele zake zikakua, zikawa kama manyoya ya tai, na kucha zake kama kucha za ndege.

**10. Katika Danieli 7:4 sehemu ya mwisho tunasoma; na akainuliwa kutoka duniani na kusimamishwa kwa miguu kama vile mwanadamu na akapewa moyo kama wa mwanaadamu, je, hii inamaanisha nini?**

Danieli 4:34-36 - Huo ulikuwa ufalme wa kwanza wa Babeli.

Danieli 4:34-36 - Hata mwisho wa siku hizo, mimi, Nebukadreza, nikainua macho yangu kuelekea mbingu, fahamu zangu zikanirudia; nikamhimidi Yeye aliye juu, nikamsifu na kumheshimu Yeye aishiye milele; kwa maana mamlaka yake ni mamlaka ya milele, na ufalme wake hudumu toka kizazi hata kizazi; watu wote wanaokaa duniani wamehesabiwa kuwa si kitu, naye hufanya kama atakavyo, katika jeshi la mbinguni, na katika hao wanaokaa duniani; wala hapana awezaye kuuzuia mkono wake, wala kumwuliza, Unafanya nini wewe? Basi wakati uo huo fahamu zangu zikanirudia, na kwa ajili ya utukufu wa ufalme wangu, enzi yangu na fahari yangu zikanirudia; na mawaziri wangu, na madiwani wangu, wakaja kunitafuta; nami nikathibitika katika ufalme wangu, nikaongezewa enzi kupita kiasi.

**11. Mwisho wa ufalme huu wa kwanza ulikuwa vipi?**

Danieli 5:30-31 - Usiku uo huo Belshaza, mfalme wa Wakaldayo, akauawa. Na Dario, Mmedi, akaupokea ufalme, naye umri wake alikuwa na miaka sitini na miwili.

Maelezo - Katika maono ya Danieli sura ya 7, pepo nne zilionekana zikivuma juu ya bahari kubwa, na wanyama wanne wakatoka baharini, kila mmoja akiwakilisha falme kubwa zitakazotawala dunia. Wanyama hawa walikuwa na maana ya falme za kihistoria, ambapo mnyama wa kwanza, kama simba, alielezea Ufalme wa Babeli, ulioongozwa na Nebukadneza, mfalme mwenye nguvu. Simba huyo alionekana akiwa na mabawa ya tai ambayo yalianguka, kielelezo cha kushuka kwa fahari ya Nebukadneza alipoonyeshwa adhabu na Elohim, alipotufukuzwa na kuwa kama mnyama kwa kipindi cha miaka saba. Hata hivyo, alikubali utawala wa Elohim na fahamu zake zikarudi, akapata utukufu tena. Mwisho wa Babeli ulijiri wakati wa Belshaza, mfalme wa pili, ambaye aliuwawa baada ya kumkhasa Elohim, na ufalme wake kupokewa na Dario, mfalme wa Mmedi. Maono haya yanaonyesha mabadiliko ya utawala duniani na kumtukuza Elohim kama mtawala wa milele juu ya falme zote.12:20

# MNYAMA WA PILI - 538 BC

1. **Baada ya Nebuchadneza ni nani alichukua mamlaka?**

Danieli 7:1 Katika mwaka wa kwanza wa Belshaza, mfalme wa Babeli, Danielii aliona ndoto, na maono ya kichwa chake, kitandani mwake; basi akaiandika ndoto, akatoa habari ya jumla ya mambo hayo.

Danieli 5:1,11,13 - Belshaza, mfalme, aliwafanyia wakuu wake elfu karamu kubwa akanywa divai mbele ya elfu hao.Yuko mtu katika ufalme wako, ambaye roho ya miungu watakatifu inakaa ndani yake; na katika siku za baba yako nuru na ufahamu na hekima zilionekana ndani yake; na mfalme Nebukadreza, baba yako, naam, mfalme, baba yako, akamfanya kuwa mkuu wa waganga, na wachawi, na Wakaldayo, na wanajimu; Ndipo Danielii akaletwa mbele ya mfalme. Na Mfalme akanena, akamwambia Danielii, Je! Wewe ndiwe Danielii yule, aliye mmoja wa wana wa Yuda waliohamishwa, ambao mfalme, baba yangu, aliwaleta huku toka Yerusalemu?

2. **Ufalme huu ulikuwa upi?**

Danieli 5:26-28 Na tafsiri ya maneno haya ni hii; MENE, Elohim ameuhesabu ufalme wako na kuukomesha. TEKELI, umepimwa katika mizani nawe umeonekana kuwa umepunguka. PERESI, ufalme wako umegawanyika, nao wamepewa Wamedi na Waajemi.

1. **Ufalme wa pili ulikuwa na mfano gani?**



Danieli 7:5 Na tazama, mnyama mwingine, wa pili, kama dubu, naye aliinuliwa upande mmoja, na mifupa mitatu ya mbavu ilikuwamo kinywani mwake katika meno yake; wakamwambia mnyama huyo hivi, Inuka, ule nyama tele.

Maelezo

Huu ni ufalme wa pili na ulichukua mamlaka baada ya vita kubwa. Ulifananishwa na myama hatari pia mla nyama ambaye ni dubu.

2. **Ufalme wa babeli uliangushwa vipi na Ufalme wa wamedi na waajemi?**

Danieli 5:1-6 Belshaza, mfalme, aliwafanyia wakuu wake elfu karamu kubwa akanywa divai mbele ya elfu hao. Belshaza, alipokuwa akionja ile divai, akaamuru wavilete vile vyombo vya dhahabu na fedha, ambavyo baba yake, Nebukadreza, alivitoa katika hekalu lililokuwako Yerusalemu; ili kwamba mfalme, na wakuu wake, na wake zake, na masuria wake, wapate kuvinywea.Basi wakavileta vile vyombo vya dhahabu, vilivyotolewa katika hekalu la nyumba ya Elohim lililokuwako Yerusalemu; na mfalme na wakuu wake, na wake zake, na masuria wake, wakavinywea. Wakanywa divai, wakaisifu miungu ya dhahabu, na ya fedha, na ya shaba, na ya chuma, na ya mti, na ya mawe. Saa iyo hiyo vikatokea vidole vya mkono wa mwanadamu, vikaandika katika chokaa ya ukuta wa nyumba ya enzi ya mfalme, mahali palipokikabili kinara; naye mfalme akakiona kitanga cha ule mkono ulioandika.Ndipo uso wa mfalme ukambadilika; fikira zake zikamfadhaisha; viungo vya viuno vyake vikalegea; magoti yake yakagongana.

3. **Jinsi walovyokunywa divai na kulewa, Yeremia alikuwa ametabiri jinsi ufalme wa babeli ungeangushwa?**

Yeremia 51:39,57-58 Wakiingiwa na ukali, nitawafanyizia karamu yao, nami nitawalevya, wapate kufurahi, na kulala usingizi wa milele, wasiamke tena, asema Bwana. Nami nitawalevya wakuu wake, na watu wake wenye hekima, maliwali wake, na maakida wake, na mashujaa wake; nao watalala usingizi wa milele, wasiamke, asema Mfalme, Bwana wa majeshi, ambaye jina lake ni Bwana.Bwana wa majeshi asema hivi, Kuta pana za Babeli zitabomolewa kabisa, na malango yake marefu yatateketezwa; nao watu watajitaabisha kwa ubatili, na mataifa kwa moto; nao watachoka.

4. **Makosa makubwa ya babeli yalikuwa ni yepi?**

Danieli 5:22-23 Na wewe, mwanawe, Ee Belshaza, hukujinyenyekeza moyo wako, ijapokuwa ulijua hayo yote.Bali umejiinua juu ya Bwana wa mbingu; nao wamevileta vyombo vya nyumba yake mbele yako; na wewe, na wakuu wako, na wake zako, na masuria wako, mmevinywea; nawe umeisifu miungu ya fedha na ya dhahabu na ya shaba, na ya chuma, na ya mti, na ya mawe; wasioona, wala kusikia, wala kujua neno lo lote; na Elohim yule, ambaye pumzi yako i mkononi mwake, na njia zako zote ni zake, hukumtukuza.

5. **Kitanga cha mkono kiliandika nini na tafsiri yake ilikuwa ipi?**

Danieli 5:24-28 - Ndipo kile kitanga cha ule mkono kikaletwa kutoka mbele zake, na maandiko haya yameandikwa.Na maandiko yaliyoandikwa ni haya; MENE,

MENE, TEKELI, NA PERESI.Na tafsiri ya maneno haya ni hii; MENE, Elohim ameuhesabu ufalme wako na kuukomesha.TEKELI, umepimwa katika mizani nawe umeonekana kuwa umepunguka.PERESI, ufalme wako umegawanyika, nao wamepewa Wamedi na Waajemi. Isaya 13:17 Tazama, nitawaamsha Wamedi juu yao, ambao hawaoni fedha kuwa kitu, wala hawafurahii dhahabu.

6. **Usiku huo ni nini kilitendeka?**

Danieli 5:30-31 - Usiku uo huo Belshaza, mfalme wa Wakaldayo, akauawa.Na Dario, Mmedi, akaupokea ufalme, naye umri wake alikuwa na miaka sitini na miwili.

Maelezo - Ufalme huu wa wamedi na waajemi ulipiga wilaya tatu za babeli yaani babeli, libya na misri hii ndiyo maana ya mifupa ya mbavu tatu ambazo zilikuwa zimeumwa na dubu. Walikuwa wafalme wawili Kurusu na Dario. Tazama Ezra 1:1Ezra 1:1 Ikawa katika mwaka wa kwanza wa Koreshi, mfalme wa Uajemi, ili kwamba neno la Bwana alilolisema kwa kinywa cha Yeremia lipate kutimizwa, Bwana akamwamsha roho yake Koreshi, mfalme wa Uajemi, hata akapiga mbiu katika ufalme wake wote, akaiandika pia, akisema,Ezra 1:1 Ikawa katika mwaka wa kwanza wa Koreshi, mfalme wa Uajemi, ili kwamba neno la Bwana alilolisema kwa kinywa cha Yeremia lipate kutimizwa, Bwana akamwamsha roho yake Koreshi, mfalme wa Uajemi, hata akapiga mbiu katika ufalme wake wote, akaiandika pia, akisema,

Historia husema ya kwamba aligeuza njia ya mto farati uliokuwa umepitia katikati ya babeli na wakapata njia ya kuingia maana kuta za babeli zilikuwa kuu sana. Majeshi yote yalikuwa yamelewa kwa hivyo neno lote likatimia na ufalme wa pili ukasimama.

# MNYAMA WA TATU 333BC




**1. Mnyama wa tatu alikuwa na mfano upi?**

Danieli 7:6 - Kisha nikatazama, na kumbe! Mnyama mwingine, kama chui, naye juu ya mgongo wake alikuwa na mabawa manne kama ya ndege; mnyama huyo alikuwa na vichwa vinne; akapewa mamlaka

**2. Chui huyu aliyekuwa na vichwa vinne na mabawa manne alisimamia ufalme upi?**

Danieli 8:20-21 - "Yule kondoo mume uliyemwona, mwenye pembe mbili, hizo ndizo wafalme wa Umedi na Uajemi.Na yule beberu, mwenye manyoya mengi, ni mfalme wa Uyunani; na ile pembe kubwa iliyo kati ya macho yake ni mfalme wa kwanza."

Danieli 10:20 - " Ndipo akasema, Je! Unajua sababu hata nikakujia? Na sasa nitarudi ili nipigane na mkuu wa Uajemi; nami nitakapotoka huku, tazama, mkuu wa Uyunani atakuja"

Maelezo

Huu ni ufalme wa Uyunani ama Grecian Empire, ulianza utawala wake mwaka wa 333 BC na Alexander mkuu ndiye aliyekuwa mfalme wake wa kwanza.

3. **Chui huyu alikuwa na mabawa manne na vichwa vinne, Je! vilisimamia nini?**

Danieli 7:6 - Kisha nikatazama, na kumbe! Mnyama mwingine, kama chui, naye juu ya mgongo wake alikuwa na mabawa manne kama ya ndege; mnyama huyo alikuwa na vichwa vinne; akapewa mamlaka."

Maelezo:

Alexander alikuwa kijana wa miaka 32 alipokuwa ameipiga dunia na kuiongoza. Historia husema alilia sana alipokosa mahali au ufalme wa kupigana nao, na jeshi lake lilitumia ndovu na mikuki mirefu ambao kwa haraka sana walipiga kila ufalme. Hii ndiyo maana ya chui na mabawa yake.

Alexander alikufa wa miaka 33 kuzaliwa ni Julai 356BC na kufa ni juni 323 BC. Alifia babeli kutokana na typhoid au malaria, wengine husema alikuwa na shida ya maini kutokana na vinywaji vikali. Alipokufa ufalme wake ulichukuliwa na majemedari wanne ambao walivisimamia vile vichwa vinne. Wafalme hawa ni - Lysimachus, Seleucus, Ptolemy na Cassandar. Ufalme huu uliondolewa na ufalme wa kirumi mnano 31BC.

## MNYAMA WA NNE




1. **Katika njozi, Danieli alimwona mnyama wa nne akiwa na sura gani?**

Danieli 7:7-8 - Baadaye nikaona katika njozi ya usiku, na tazama, mnyama wa nne, mwenye kutisha, mwenye nguvu, mwenye uwezo mwingi, naye alikuwa na meno ya chuma, makubwa sana; alikula na kuvunja vipande vipande, na kuyakanyaga mabaki kwa miguu yake; na umbo lake lilikuwa mbali kabisa na wale wa kwanza, naye alikuwa na pembe kumi. Nikaziangalia sana pembe zake, na tazama, pembe nyingine ikazuka kati yao, nayo ilikuwa ndogo, ambayo mbele yake pembe tatu katika zile za kwanza zikang'olewa kabisa; na tazama, katika pembe hiyo mlikuwa na macho kama macho ya mwanadamu, na kinywa kilichokuwa kikinena maneno makuu.

2. **Mnyama huyu hatari alitawala kwa muda gani?**

Danieli 7:9 - Nikatazama hata viti vya enzi vikawekwa, na mmoja aliye mzee wa siku ameketi; mavazi yake yalikuwa meupe kama theluji, na nywele za kichwa chake kama sufu safi; kiti chake cha enzi kilikuwa miali ya moto, na gurudumu zake moto uwakao.

3. **Hatima ya mnyama huyu wa nne itakuwa nini?**

Danieli 7:11 - Nikatazama wakati huo; kwa sababu ya sauti ya yale maneno makubwa iliyoyasema ile pembe; nalitazama hata mnyama yule akauawa, mwili wake ukaharibiwa, akatolewa ateketezwe kwa moto.

4. **Mnyama huyu atakapouawa na kuteketezwa, ni nani alichukua mamlaka, utukufu, na ufalme?**

Danieli 7:13-14 - Nikaona katika njozi za usiku, na tazama, mmoja aliye mfano wa mwanadamu akaja pamoja na mawingu ya mbingu akamkaribia huyo mzee wa siku, wakamleta karibu naye. Naye akapewa mamlaka, na utukufu, na ufalme, ili watu wa kabila zote, na taifa zote, na lugha zote, wamtumikie; mamlaka yake ni mamlaka ya milele, ambayo hayatapita kamwe, na ufalme wake ni ufalme usioweza kuangamizwa.

5. **Danieli alihuzunishwa sana na njozi ya mnyama huyu wa nne. Ni nani aliyemtafsiria maana yake?**

Danieli 7:15-16 - Basi, mimi Danieli, roho yangu ilihuzunika mwilini mwangu, na hayo maono ya kichwa changu yakanifadhaisha. Nikamkaribia mmoja wa hao waliosimama karibu, nikamwuliza maana ya kweli ya hayo yote. Basi akaniambia, akanijulisha tafsiri ya mambo hayo.

6. **Kwa nini Danieli alitaka tafsiri ya mnyama huyu wa nne hasa?**

Danieli 7:19-21 - Kisha nalitaka kujua maana ya yule mnyama wa nne, aliyekuwa mbali na wenziwe wote, mwenye kutisha sana, ambaye meno yake yalikuwa ya chuma, na makucha yake ya shaba; aliyekula, na kuvunja vipande vipande, na kuyakanyaga mabaki kwa miguu yake; na habari za zile pembe kumi zilizokuwa kichwani mwake, na ile pembe nyingine iliyozuka, ambayo mbele yake zilianguka pembe tatu; yaani, pembe ile yenye macho, na kanwa lililonena makuu, ambayo kuonekana kwake kulikuwa hodari kuliko wenzake. Nikatazama, na pembe iyo hiyo ilifanya vita na watakatifu, ikawashinda.

7. **Tafsiri yake ilikuwa nini?**

Danieli 7:23 - Akanena hivi, Huyo mnyama wa nne atakuwa ni ufalme wa nne juu ya dunia, utakaokuwa mbali na falme zile zote, nao utakula dunia yote, na kuikanyaga, na kuivunja vipande vipande.

8. **Na pembe zile kumi zilisimamia nini?**

- Danieli 7:24 - Na habari za zile pembe kumi, katika ufalme huo wataondoka wafalme kumi; na mwingine ataondoka baada ya hao; naye atakuwa mbali na hao wa kwanza; naye atawashusha wafalme watatu.

9. **Kazi ya pembe hii ndogo iliyong'oa pembe tatu ilikuwa nini?**

- Danieli 7:25 - Naye atanena maneno kinyume chake Aliye juu, naye atawadhoofisha watakatifu wake Aliye juu; naye ataazimu kubadili majira na sheria; nao watatiwa mikononi mwake kwa wakati, na nyakati mbili, na nusu wakati.

Maelezo: Ni kweli kwamba mnyama wa nne ni ufalme wa nne ambao ni wa Rumi. Ulianza mwaka wa 31 KK ambapo falme kumi za Ulaya zilishikana na kutengeneza ufalme mmoja wa Kirumi. Kama Danieli alivyoambiwa, pembe kumi ni wafalme kumi. Falme hizo ni:

i. Anglo-Saxon – England
ii. Burgundians – Switzerland
iii. Franks – France
iv. Visigoths – Spain
v. Lombards – Italy
vi. Alemanni – Germany
vii. Suevi – German – Czech Republic Region
viii. Vandals
ix. Ostrogoths
x. Heruli

## PEMBE NDOGO




**1. Mfano wa hii pembe ndogo ni upi?**

Danieli 7:8 - Nikaziangalia sana pembe zake, na tazama, pembe nyingine ikazuka kati yao, nayo ilikuwa ndogo, ambayo mbele yake pembe tatu katika zile za kwanza zikang'olewa kabisa; na tazama, katika pembe hiyo mlikuwa na macho kama macho ya mwanadamu, na kinywa kilichokuwa kikinena maneno makuu.

Danieli 7:20 - na habari za zile pembe kumi zilizokuwa kichwani mwake, na ile pembe nyingine iliyozuka, ambayo mbele yake zilianguka pembe tatu; yaani, pembe ile yenye macho, na kanwa lililonena makuu, ambayo kuonekana kwake kulikuwa hodari kuliko wenzake.

**2. Kazi ya hii pembe ndogo ni gani?**

Danieli 7:21 - Nikatazama, na pembe iyo hiyo ilifanya vita na watakatifu, ikawashinda;

Danieli 7:25 - Naye atanena maneno kinyume chake Aliye juu, naye atawadhoofisha watakatifu wake Aliye juu; naye ataazimu kubadili majira na sheria; nao watatiwa mikononi mwake kwa wakati, na nyakati mbili, na nusu wakati.

**3. Baada ya utawala wake, nani alipewa mamlaka?**

Danieli 7:22 - hata akaja huyo mzee wa siku, nao watakatifu wake Aliye juu wakapewa hukumu; na majira yakawadia watakatifu waumiliki ufalme.

Danieli 7:27 - Na ufalme, na mamlaka, na ukuu wa ufalme, chini ya mbingu zote, watapewa watu wa watakatifu wake Aliye juu; ufalme wake ni ufalme wa milele, na wote wenye mamlaka watamtumikia na kumtii.

**4. Je, Danieli alipewa tafsiri ya pembe hii? Tafsiri yake ni gani?**

Danieli 7:24 - Na habari za zile pembe kumi, katika ufalme huo wataondoka wafalme kumi; na mwingine ataondoka baada ya hao; naye atakuwa mbali na hao wa kwanza; naye atawashusha wafalme watatu.

Maelezo: Baada ya wafalme hawa kumi kuitawala dunia kwa muda mrefu, waliona vyema kumpa kiongozi wa dini ya Kirumi mamlaka yao, yaani 'Pope' aliyekuwa askofu wa Roma wakati huo. Hata hivyo, wafalme wa nchi zile tatu; Vandals, Ostrogoths na Heruli, walikataa. Pope alipewa jeshi na akaanza vita na nchi hizo. Mnamo mwaka wa 538 AD ndipo aling'oa kabisa nchi ya tatu, na hapo ndipo dini na ufalme vikaungana na ufalme huu ukaanza. Ufalme huu uliitwa 'Holy Roman Empire' ama 'Papacy Kingdom'.

5. **Je, Yohana aliyeandika kitabu cha Ufunuo alionyeshwa jambo hilo?**

Ufunuo wa Yohana 17:17 - Maana Elohim ametia mioyoni mwao kufanya shauri lake, na kufanya shauri moja, na kumpa yule mnyama ufalme wao hata maneno ya Elohim yatimizwe.

6. **Katika maono yake, Yohana aliona nini?**

Ufunuo wa Yohana 17:1-3 - Akaja mmoja wa wale malaika saba, wenye vile vitasa saba, akanena nami, akisema, Njoo huku, nitakuonyesha hukumu ya yule kahaba mkuu aketiye juu ya maji mengi; ambaye wafalme wa nchi wamezini naye, nao wakaao katika nchi wamelevywa kwa mvinyo ya uasherati wake. Akanichukua katika Roho hata jangwani, nikaona mwanamke, ameketi juu ya mnyama mwekundu sana, mwenye kujaa majina ya makufuru, mwenye vichwa saba na pembe kumi.

7. **Mwanamke huyu aliyekalia mnyama huyu wa ajabu amevikwa nini?**

Ufunuo wa Yohana 17:4 - Na mwanamke yule alikuwa amevikwa nguo ya rangi ya zambarau, na nyekundu, amepambwa kwa dhahabu, na kito cha thamani, na lulu, naye alikuwa na kikombe cha dhahabu mkononi mwake, kilichojawa na machukizo, na machafu ya uasherati wake.

8. **Jina la siri lililoandikwa kwenye kipaji cha uso wake ni lipi?**

Ufunuo wa Yohana 17:5 - Na katika kipaji cha uso wake alikuwa na jina limeandikwa, la siri, BABELI MKUU, MAMA WA MAKAHABA NA MACHUKIZO YA NCHI.

Maelezo: Mwanamke huyu alisimamia kanisa hili la Kirumi, katika kipindi cha giza kuu kilichoifunika dunia nzima. Kipindi hiki kilianza mwaka wa 538 AD mpaka 1798 AD, jumla ya miaka 1260. Mwanamke huyu aliyevikwa mambo ya dunia ya thamani kuu ambaye wafalme wa dunia walizini naye. Alikuwa na kikombe cha dhahabu kilichojaa machukizo na machafu ya uasherati wake. Haya ni mafundisho potovu yaliyofanya dunia nzima kulewa na kuanguka. Baadhi ya mafundisho haya ni kama: kubadilisha na kuondolewa kwa Amri za Elohim, kubadilishwa kwa sabato takatifu kutoka siku ya saba ya juma hadi siku ya kwanza ambayo ni Jumapili, sherehe za kipagani kama Krismasi, Easter Sunday na Good Friday, kubadilisha saa, mwezi, sherehe za mwaka mpya (1 Januari) na mengine mengi ambayo yamefanya dunia yote kulewa kiroho ambayo ni divai ya mafundisho ya uongo. Huyu ndiye Babeli mama wa makahaba, yaani ndiye aliyezaa makanisa yote ya kiprotestanti na ndiyo maana ya jina hilo la siri

Yeremia 51:7.- Babeli umekuwa kikombe cha dhahabu mkononi mwa Elohim; kilicholevya dunia yote; mataifa wamekunywa mvinyo wake; kwa sababu hiyo mataifa wameingiwa na wazimu.

9. **Mwanamke huyu alikuwa mlevi. Je! alikuwa amelewa na nini?**

Ufunuo wa Yohana 17:6 - Nikamwona yule mwanamke amelewa kwa damu ya watakatifu, na kwa damu ya mashahidi wa Yahshua. Nami nilipomwona nikastaajabu ajabu kuu.

Ufunuo wa Yohana 13:5-7 - Naye akapewa kinywa cha kunena maneno makuu, ya makufuru. Akapewa uwezo wa kufanya kazi yake miezi arobaini na miwili. Akafunua kinywa chake amtukane Elohim, na kulitukana jina lake, na maskani yake, nao wakaao mbinguni. Tena akapewa kufanya vita na watakatifu na kuwashinda, akapewa uwezo juu ya kila kabila na jamaa na lugha na taifa.

Maelezo: Ni katika kipindi hiki cha miaka 1260 (au miezi 42) ambapo watakatifu waliuawa, na damu ya watakatifu wengi ikamwagwa. Historia husema kati ya watu milioni 50 na 100 waliuawa katika kipindi hiki. Kweli mwanamke huyu alikuwa amelewa damu ya wateule. Soma (Ufunuo wa Yohana 18:24 - Na ndani yake ilionekana damu ya manabii, na ya watakatifu, na ya wale wote waliouawa juu ya nchi.)

10. **Watu wa ulimwengu walifanya nini?**

Ufunuo wa Yohana 13:4 - Wakamsujudu yule joka kwa sababu alimpa huyo mnyama uwezo wake; nao wakamsujudu yule mnyama, wakisema, Ni nani afananaye na mnyama huyu? Tena ni nani awezaye kufanya vita naye?

Ufunuo wa Yohana 13:8-9 - Na watu wote wakaao juu ya nchi watamsujudu, kila ambaye jina lake halikuandikwa katika kitabu cha uzima cha Mwana-Kondoo, aliyechinjwa tangu kuwekwa misingi ya dunia. Mtu akiwa na sikio na asikie.

**11.Kichwa kimoja cha mnyama huyu kilifanya nini?**

- Ufunuo wa Yohana 13:3 - Nikaona kimoja cha vichwa vyake kana kwamba kimetiwa jeraha la mauti, na pigo lake la mauti likapona. Dunia yote ikamstaajabia mnyama yule.

Maelezo: Jeraha hili la mauti ni wakati Napoleon mfalme wa Ufaransa alimtuma jenerali Bathier mjini Roma. Alimpiga Pope na kumnyang'anya mamlaka aliyokuwa nayo ya kuitawala serikali na kanisa ambapo alimshika Pope mwaka wa 1798 AD/CE akampeleka katika kisiwa kimoja cha Mediterranean Sea. Pope huyu alikufa baada ya miezi mitatu. Hivyo kanisa na serikali zikaachana.

**12.Malaika aliyeshuka kutoka juu alipaza sauti akasemaje?**

Ufunuo wa Yohana 18:1-3 - Baada ya hayo naliona malaika mwingine, akishuka kutoka mbinguni, mwenye mamlaka kuu; na nchi ikaangazwa kwa utukufu wake. Akalia kwa sauti kuu, akisema, Umeanguka, umeanguka Babeli ule mkuu; umekuwa maskani ya mashetani, na ngome ya kila roho mchafu, na ngome ya kila ndege mchafu mwenye kuchukiza; kwa kuwa mataifa yote wamekunywa mvinyo ya ghadhabu ya uasherati wake, na wafalme wa nchi wamezini naye, na wafanya biashara wa nchi wamepata mali kwa nguvu za kiburi chake.

**13.Ni onyo gani tunalopokea kutoka kwa malaika mwingine wa tatu?**

Ufunuo wa Yohana 14:9-11 - Na mwingine, malaika wa tatu, akawafuata, akisema kwa sauti kuu, Mtu awaye yote akimsujudu huyo mnyama na sanamu yake, na kuipokea chapa katika kipaji cha uso wake, au katika mkono wake, yeye naye atakunywa katika mvinyo ya ghadhabu ya Elohim iliyotengenezwa, pasipo kuchanganywa na maji, katika kikombe cha hasira yake; naye atateswa kwa moto na kiberiti mbele ya malaika watakatifu, na mbele za Mwana-Kondoo. Na moshi wa maumivu yao hupanda juu hata milele na milele, wala hawana raha mchana wala usiku, hao wamsujuduo huyo mnyama na sanamu yake, na kila aipokeaye chapa ya jina lake.

**14.Tunapaswa kuchukua hatua gani basi?**

- Ufunuo wa Yohana 18:4-5 - Kisha nikasikia sauti nyingine kutoka mbinguni, ikisema, Tokeni kwake, enyi watu wangu, msishiriki dhambi zake, wala msipokee mapigo yake. Kwa maana dhambi zake zimefika hata mbinguni, na Elohim amekumbuka maovu yake.

## JERAHA LA MAUTI LILILOPONA

1. **Katika Ufunuo wa Yohana 13:1-2 tunajifunza nini?**




Ufunuo wa Yohana 13:1-2 - Kisha nikaona mnyama akitoka katika bahari, mwenye pembe kumi, na vichwa saba, na juu ya pembe zake ana vilemba kumi, na juu ya vichwa vyake majina ya makufuru. Na yule mnyama niliyemwona alikuwa mfano wa chui, na miguu yake ilikuwa kama miguu ya dubu, na kinywa chake kama kinywa cha simba, yule joka akampa nguvu zake na kiti chake cha enzi na uwezo mwingi.

2. **Kichwa kimoja cha mnyama huyu kilitiwa nini?**

Ufunuo wa Yohana 13:3 - Nikaona kimoja cha vichwa vyake kana kwamba kimetiwa jeraha la mauti, na pigo lake la mauti likapona. Dunia yote ikamstaajabia mnyama yule.

3. **Dunia yote ilifanya nini?**

Ufunuo wa Yohana 13:4 - Wakamsujudu yule joka kwa sababu alimpa huyo mnyama uwezo wake; nao wakamsujudu yule mnyama, wakisema, Ni nani afananaye na mnyama huyu? Tena ni nani awezaye kufanya vita naye?

Maelezo - Mnyama huyu ni ufalme huo huo wa Kirumi, kakita kipindi cha papa. Nguvu zake ni mchanganyiko wa wanyama wote wa Danieli saba. Ndiposa tunaona mfano wa chui, kinywa kama cha Simba, miguu mfano wa dubu, pembe kumi na vichwa saba. Jeraha la mauti katika kichwa kimoja ni wakati Napoleon alimpiga papa na kumnyang'anya mamlaka ya kuitawala serikali ya Kirumi mnamo 1798 AD. Jeraha hilo la mauti lilionekana kuwa limepona.

4. **Je! Jeraha hilo llilionekana limepona vipi?**

Ufunuo wa Yohana 17:8 - Yule mnyama uliyemwona alikuwako, naye hayuko, naye yu tayari kupanda kutoka kuzimu na kwenda kwenye uharibifu. Na hao wakaao juu ya nchi, wasioandikwa majina yao katika kitabu cha uzima tangu kuwekwa misingi ya ulimwengu, watastaajabu wamwonapo yule mnyama, ya kwamba alikuwako, naye hayuko, naye atakuwako.

5. **Ni nguvu zipi za kifalme ziliweza kuusimamisha Upapa tena uweze kusikika?**

Ufunuo wa Yohana 13:11-12 - Kisha nikaona mnyama mwingine, akipanda juu kutoka katika nchi; naye alikuwa na pembe mbili mfano wa Mwana-Kondoo, akanena kama joka. Naye atumia uwezo wote wa mnyama yule wa kwanza mbele yake. Naye aifanya dunia na wote wakaao nda ni yake wamsujudie mnyama wa kwanza, ambaye jeraha lake la mauti lilipona.

6. **Ni ishara zipi za kuupotosha ulimwengu ziliweza kuonekana kwa mnyama huyo?**

Ufunuo wa Yohana 13:13-15 - Naye afanya ishara kubwa, hata kufanya moto kushuka kutoka mbinguni uje juu ya nchi mbele ya wanadamu. Naye awakosesha wale wakaao juu ya nchi, kwa ishara zile alizopewa kuzifanya mbele ya huyo mnyama, akiwaambia wakaao juu ya nchi kumfanyia sanamu yule mnyama, aliyekuwa na jeraha la upanga naye akaishi. Akapewa kutia pumzi katika ile sanamu ya mnyama, hata ile sanamu ya mnyama inene, na kuwafanya hao wote wasioisujudu sanamu ya mnyama wauawe.

Maelezo - Huu ni ufalme wa Marekani ambao Yohana aliuona kama mnyama mpole mfano mwana kondoo lakini anena kama Joka. Pembe mbili zikisimamia vyama viwili vya utawala yaani Republican na Democratic parties. Utawala wote wa Marekani ni wa mnyama aliyekuwa na jeraha la mauti na kisha akapona. Uweza ulio na Marekani ni wa kuifanya Dunia nzima imsujudie mnyama wa kwanza na hata utaleta mauaji kwa wote watakao kataa kumsujudia mnyama huyo.




7. **Ni ushawishi upi Marekani imekuwa nao katika ulimwengu wa kibiashara?**

Ufunuo wa Yohana 13:16-17 - Naye awafanya wote, wadogo kwa wakubwa, na matajiri kwa maskini, na

walio huru kwa watumwa, watiwe chapa katika mkono wao wa kuume, au katika vipaji vya nyuso zao; tena kwamba mtu awaye yote asiweze kununua wala kuuza, isipokuwa ana chapa ile, yaani, jina la mnyama yule, au hesabu ya jina lake.

**8. Nambari ya huyo mnyama ni ipi?**

Ufunuo wa Yohana 13:18 - Hapa ndipo penye hekima. Yeye aliye na akili, na aihesabu hesabu ya mnyama huyo; maana ni hesabu ya kibinadamu. Na hesabu yake ni mia sita, sitini na sita.

Maelezo - Sasa dunia nzima imeweza kuletwa pamoja chini ya mpango wa New World Order. Ambao kwa hakika unaweza kuitawala dunia kwa kila hali. Elimu ya teknolojia imeweza kutawala dunia nzima kiuchumi, biashara zote na hata kisiasa.12:20

Hivi karibuni hakuna mtu atakaye weza kuuza wala kununua pasipo na nambari itakayo wekwa mwilini kupitia njia ya chip ili uweze kuuza na kununua. Nambari ya 666 hupatikana hata katika krauni ya utawala ya papa ambayo imeandikwa jina hili Vicarius Filii Dei. Mwenye hekima akihesabu jina hilo kwa kuipa kila herufi dhamana ya Kirumi itakupa 666.

**9. Malaika wa tatu anatoa onyo ipi?**

Ufunuo wa Yohana 14:9-10 - Na mwingine, malaika wa tatu, akawafuata, akisema kwa sauti kuu, Mtu awaye yote akimsujudu huyo mnyama na sanamu yake, na kuipokea chapa katika kipaji cha uso wake, au katika mkono wake, yeye naye atakunywa katika mvinyo ya ghadhabu ya Elohim iliyotengenezwa, pasipo kuchanganywa na maji, katika kikombe cha hasira yake; naye atateswa kwa moto na kiberiti mbele ya malaika watakatifu, na mbele za Mwana-Kondoo.

**10.Kikombe hiki cha hasira ya mvinyo wa Elohim kinasimamia nini?**

Ufunuo wa Yohana 15:1 - Kisha nikaona ishara nyingine katika mbingu, iliyo kubwa, na ya ajabu; malaika saba wenye mapigo saba ya mwisho; maana katika hayo ghadhabu ya Elohim imetimia.

Maelezo - Haya ni mapigo saba ya mwisho, ambayo Elohim ameyaweka tayari chini ya malaika saba, ambayo yatatimiza hasira za Elohim duniani.

**11.Mapigo haya ni yepi?**

Muhtasari wa Ufunuo Sura ya 16:1-21 - Vitasa Saba vya Hasira za Elohim

Katika Ufunuo 16:1-21, Yohana anaonyeshwa kumiminwa kwa hukumu ya ghadhabu ya Elohim juu ya dunia kupitia vitasa saba vya hasira. Hizi ni adhabu kali zinazokuja kama jibu la dhambi za wanadamu, zikimalizia kwa uharibifu wa waovu.

a. **Kitasa cha Kwanza (Mistari 1-2)** - Vidonda vya maumivu vinapata wale wenye alama ya mnyama na wanaoabudu picha yake. Hii ni hukumu dhidi ya ibada ya sanamu na uasi wa wanadamu.
b. **Kitasa cha Pili (Mstari 3)** - Bahari inageuka kuwa damu na viumbe vyote vya baharini vinakufa. Hii ni hukumu kwa wale waliomwaga damu ya watakatifu na manabii.
c. **Kitasa cha Tatu (Mistari 4-7)** - Mito na chemchemi zinageuka kuwa damu, na malaika anatangaza kuwa adhabu hii ni haki kwa sababu waovu wameimwaga damu ya watu wa Elohim. Haki ya Elohim inadhihirishwa.
d. **Kitasa cha Nne (Mistari 8-9)** - Jua linapewa nguvu ya kuwasha moto mkali na kuwasababisha watu kupigwa na joto kali. Licha ya mateso, watu wanakataa kutubu na wanalaani Elohim.
e. **Kitasa cha Tano (Mistari 10-11)** - Ufalme wa mnyama unazama katika giza, na watu wanateseka kwa maumivu makali. Hata hivyo, wanakataa kutubu na kubaki katika uasi wao.
f. **Kitasa cha Sita (Mistari 12-16)** - Mto Eufrate unakauka kuandaa njia kwa wafalme wa Mashariki. Roho tatu za uovu zinatoka katika vinywa vya joka, mnyama, na nabii wa uongo, zikifanya miujiza ili kuwakusanya wafalme wa dunia kwa vita la mwisho huko Harmagedoni.
g. **Kitasa cha Saba (Mistari 17-21)** - Kitasa la saba linamiminwa angani, na sauti kutoka katika kiti cha enzi inasema, Imekwisha! Tetemeko kubwa linatokea, likitikisa dunia na kusababisha miji, visiwa, na milima kutoweka. Hailstones kubwa, kila moja ikiwa na uzito wa kilo 45, zinashuka kutoka angani, lakini watu wanalaani Elohim na wanakataa kutubu.

Hitimisho - Sura hii inaonyesha ukali wa hukumu ya Elohim dhidi ya dhambi, ugumu wa mioyo ya waovu, na ushindi wa mwisho wa mapenzi ya Elohim juu ya uovu. Hizi ni adhabu kwa uasi na mwito wa mwisho wa kutubu, ingawa wengi wanakataa kutubu.
Ufunuo wa Yohana 8,9 - Muhtasari wa Ufunuo wa Yohana Sura ya 8 na 9

Sura ya 8:1-13 – Kufungua Muhuri wa Saba na Mapigo ya Pipa la Thabiti

Kufunguliwa kwa Muhuri wa Saba (Mstari 1-5)

Wakati muhuri wa saba unafunguliwa, kuna kimya cha nusu saa mbinguni. Malaika mmoja anachukua thabiti ya dhahabu na anatoa moshi wa thabiti mbele ya Elohim, ambao unachanganywa na sala za watakatifu. Hii inaonyesha maombi ya watu wa Elohim kuwa na nguvu mbele ya Elohim. Kisha, malaika anatoa thabiti hiyo duniani, na mapigo makali yanatokea.

Mapigo (Mstari 6-13) - Malaika saba wanapokea macheteto saba, na kila moja linatoa pigo kwa dunia. Wakati wa kupiga, vipengele mbalimbali vya dunia vinapata madhara makubwa. Hii ni maandalizi ya mapigo makali zaidi, ambayo yatakuja baadaye, kama vile dhoruba, mvua ya mawe, na mapigo makali ya moto.

**Sura ya 9:1-21 – Mapigo ya Tatu ya Pipa na Uharibifu wa Dunia**

a. **Kufungua Kisanduku cha Tatu (Mstari 1-12)** –

Malaika wa tano anapofungua kisanduku chake, nyota inashuka kutoka angani, na ufungua kisima cha kuzimu. Kutoka humo, mende wa ajabu wanatoka na kuwasumbua watu kwa maumivu makali. Walakini, watu hawawezi kufa kutokana na maumivu haya, lakini wanateseka sana.

b. **Kufungua Kisanduku cha Nne (Mstari 13-19)** –

Malaika wa sita anapopiga baragumu lake, wanatokea majitu manne kutoka mto Eufrate, na wanaletewa majeshi ya watu milioni mia mbili ili kuleta uharibifu mkubwa. Hii ni sehemu ya vita vya mwisho vinavyofanyika duniani, ambapo watu wanapigwa na maafa makubwa.

**c. Madhara na Kifo cha Mwandamu (Mstari 20-21)**

Wakati wa mapigo haya, wengi wanakataa kutubu dhambi zao. Ingawa wanapata mateso makali, wanendelea na uasi wao dhidi ya Elohim, wakilaumu na kutotubu. Hii inaonyesha hali ya ugumu wa mioyo ya wanadamu na upinzani wao kwa Elohim.

Hitimisho - Katika sura hizi tatu, Yohana anaona picha ya maafa makubwa yanayokuja kama adhabu ya dhambi za wanadamu. Mapigo haya ni hukumu ya Elohim dhidi ya uovu, lakini licha ya mateso, wengi wanakataa kutubu na kumtukana Elohim. Hii inadhihirisha ugumu wa mioyo ya waovu na hatua za mwisho za haki ya Elohim duniani.
Haya ni maelezo mafupi sana ya sura hizi tatu msomaji anahimizwa achukue muda wake aweze kupitia sura hizi kikamilifu ili kupata picha yote kwa ukamilifu.

**12. Baada ya mapigo haya ni nini kitatokea?**

Ufunuo wa Yohana 11:15 - Malaika wa saba akapiga baragumu, pakawa na sauti kuu katika mbingu, zikisema, Ufalme wa dunia umekwisha kuwa ufalme wa Bwana wetu na wa Masihi wake, naye atamiliki hata milele na milele.

**13. Tunahimizwa kufanya nini ili tukoe nafsi zetu kutoka kwa mapigo haya?**

Ufunuo wa Yohana 18:4-8 - Kisha nikasikia sauti nyingine kutoka mbinguni, ikisema, Tokeni kwake, enyi watu wangu, msishiriki dhambi zake, wala msipokee mapigo yake. Kwa maana dhambi zake zimefika hata mbinguni, na Elohim amekumbuka maovu yake. Mlipeni kama yeye alivyolipa, mkamlipe mara mbili kwa kadiri ya matendo yake. Katika kikombe kile alichokichanganyisha, mchanganyishieni maradufu. Kwa kadiri alivyojitukuza na kufanya anasa, mpeni maumivu na huzuni kadiri iyo hiyo. Kwa kuwa husema moyoni mwake, Nimeketi malkia, wala si mjane, wala sitaona huzuni kamwe. Kwa sababu hiyo mapigo yake yatakuja katika siku moja, mauti, na huzuni, na njaa, naye atateketezwa kabisa kwa moto. Kwa maana Bwana Elohim aliyemhukumu ni mwenye nguvu.

Yeremia 51:6-7 - Kimbieni kutoka kati ya Babeli, kila mtu na ajiokoe nafsi yake; msikatiliwe mbali katika uovu wake; maana ni wakati wa kisasi cha BWANA, atamlipa malipo. Babeli umekuwa kikombe cha dhahabu mkononi mwa BWANA; kilicholevya dunia yote; mataifa wamekunywa mvinyo wake; kwa sababu hiyo mataifa wameingiwa na wazimu.

Maelezo - Funzo hili linajadili tafsiri ya kinabii ya mnyama katika Ufunuo 13, akiwakilisha Ufalme wa Kirumi na upapa, na kurudi kwa nguvu zake baada ya jeraha la mauti kupona. Kuinuka kwa mnyama wa pili (unaowakilisha Marekani) kunahusishwa na kulazimisha utiifu kwa mnyama wa kwanza kupitia udhibiti na ushawishi wa kiuchumi, na hatimaye alama ya mnyama (666). Tunasisitiziwa madhara ya kumwabudu mnyama, ikijumuishwa hasira ya Elohim na hukumu ya mwisho. Waumini tunahimizwa kujitenga na dhambi na mifumo iliyooza ya dunia ili kuepuka adhabu hizi zinazokuja, ikisisitiza ushindi wa mwisho wa ufalme wa Elohim.

# SEHEMU YA TATU

# MWONGOZO WA BIBLIA KATIKA MAISHA

## UTANGULIZI WA SEHEMU YA TATU

Sehemu hii ya tatu nay a mwisho ina umuhimu mkubwa katika kufanya mtu wa Elohim awe mkamilifu kabisa. Mafunzo yaliyo katika sehemu hii yansaidia msomaji kuwa na maisha bora na yenye furaha na amani hapa duniani huku akimpendeza Muumba wetu. Tumeagizwa kutunza miili yetu ambayo ni Hekalu la Roho Mtakatifu. Katika sehemu hii, utapata maagizo yanayohusu maisha ya mteule ya kila siku. Ni vizuri kuiga mifano bora ya waliotutangulia katika masuala ya Kuomba, kula, kunywa, kuvaa, kusema, kufanya kazi na hata kulea watoto. Paulo anahimiza kuishi maisha yanayompendeza aliyetuumba katika mambo yote. 1 Wakorintho 10:31 -**Basi, mlapo, au mnywapo, au mtendapo neno lo lote, fanyeni yote kwa utukufu wa Elohim.**

## MAOMBI

1. **Ni ushauri gani wa maana tunapewa na mtume Paulo?**

1 Timotheo 2:1-3 - Basi, kabla ya mambo yote, nataka dua, sala, maombezi, na shukrani zifanyike kwa ajili ya watu wote; kwa ajili ya wafalme na wote wenye mamlaka, ili tuishi maisha ya utulivu na amani, katika utauwa wote na ustahivu. Hili ni zuri, nalo lakubalika mbele za Elohim Mwokozi wetu.

2. **Je, Biblia imeeleza kuwa maombi ni nini?**

Zaburi 142:1-2 - Kwa sauti yangu nitamlilia Bwana, kwa sauti yangu nitamwomba Bwana dua. Nitafunua mbele zake malalamiko yangu, shida yangu nitaitangaza mbele zake.

3. **Biblia imempa Elohim sifa gani kuhusiana na maombi?**

Zaburi 65:2 “Wewe usikiaye kuomba, wote wenye mwili watakujia.

4. **Kama ni hivyo basi, tunafaa kumwomba Elohim aje?**

Mathayo 6:5-6 - Tena msalipo, msiwe kama wanafiki; kwa maana wao hupenda kusali hali wamesimama katika masinagogi na katika pembe za njia, ili waonekane na watu. Amin, nawaambia, wamekwisha kupata thawabu yao. Bali wewe usalipo, ingia katika chumba chako cha ndani, na ukiisha kufunga mlango wako, usali mbele za Baba yako aliye sirini; na Baba yako aonaye sirini atakujazi.

5. **Je, tunafaa kupayuka-payuka tunapomwomba Elohim ama tumepewa taratibu gani nzuri?**

Mathayo 6:7 - Nanyi mkiwa katika kusali, msipayuke-payuke, kama watu wa mataifa; maana wao hudhani ya kuwa watasikiwa kwa sababu ya maneno yao kuwa mengi.

6. **Ni lazima sauti yako isikike unapoomba?**

1 Samweli 1:12-13 - Ikawa, hapo alipodumu kuomba mbele za Bwana, Eli akamwangalia kinywa chake. Basi Hana alikuwa akinena moyoni mwake; midomo yake tu ilionekana kama anena, sauti yake isisikiwe; kwa hiyo Eli alimdhania kuwa amelewa.

Maelezo - Ingawa Hana alikuwa na uchungu sana kwa sababu ya kukosa mtoto na hivyo akawa akipata kejeli kutoka kwa Penina, alipokuwa akiomba hakupayuka-payuka ili asikiwe mbali, aliomba kwa utulivu sana hata maneno yake yasisikiwe.

7. **Ni nani huombwa kwa kupayuka-payuka na kupiga makelele kwa sauti kuu?**

1 Wafalme 18:26-29 - Wakamtwaa yule ng'ombe waliyepewa, wakamtengeneza, wakaliitia jina la Baali tangu asubuhi hata adhuhuri, wakisema, Ee Baali, utusikie. Lakini hapakuwa na sauti, wala aliyejibu. Nao wakaruka-ruka juu ya madhabahu waliyoifanya. Ikawa, wakati wa adhuhuri, Eliya akawafanyia dhihaka, akasema, Mwiteni kwa sauti kuu; maana ni Elohim huyo; labda anazungumza, au ana shughuli, au anasafiri, au labda amelala, sharti aamshwe. Wakapiga kelele, wakajikata-kata kwa visu na vyembe kama ilivyo desturi yao, hata damu ikawachuruzika. Ikawa, wakati wa adhuhuri ulipopita, walitabiri hata wakati wa kutoa dhabihu ya jioni; lakini hapakuwa na sauti, wala aliyejibu, wala aliyeangalia.

8. **Ni mfano upi mzuri tunaonyeshwa na Nabii Eliya jinsi tunavyopaswa kumwendea Elohim kwa njia ya maombi?**

1 Wafalme 18:36 - Ikawa, wakati wa kutoa dhabihu ya jioni, Eliya nabii akakaribia, akasema, Ee Bwana, Elohim wa Ibrahimu, na wa Isaka, na wa Israeli, na ijulikane leo ya kuwa wewe ndiwe Elohim katika Israeli, na ya kuwa mimi ni mtumishi wako, na ya kuwa nimefanya mambo haya yote kwa neno lako.

Maelezo - Eliya aliuchukua muda wake akaiandaa dhabihu ya kuteketezwa, akayakaribia madhabahu na kumnenea Elohim kwa maneno machache yenye utulivu.

**9. Ni nani anafaa kuongoza maombi?**

1 Timotheo 2:8 - Basi, nataka wanaume wasalishe kila mahali, huku wakiinua mikono iliyotakata pasipo hasira wala majadiliano.

Maelezo - Somo hili linatufundisha umuhimu wa maombi na jinsi tunavyopaswa kuomba kwa njia inayokubalika mbele za Elohim. Mtume Paulo anashauri maombi ya shukrani na maombezi kwa ajili ya watu wote, ili tuishi maisha ya utulivu na amani. Biblia inafundisha kwamba maombi ni kutoa shukrani na shida zetu mbele za Elohim kwa unyenyekevu. Tunapaswa kuomba kwa utulivu, bila kupayuka-payuka au kutafuta umakini wa watu. Eliya anatuonyesha mfano wa kuomba kwa imani, kwa kutoa maombi ya utulivu na kwa kutumia maneno machache, bila kujaribu kujionyesha. Elohim anasikia maombi yetu, na tunapaswa kumwendea kwa heshima na unyenyekevu.

## CHAKULA

1. **Hapo mwanzo Elohim alimpa mwanadamu (Adamu na Hawa) nini kama chakula?**

Mwanzo1:29 - Elohim akasema, Tazama, nimewapa kila mche utoao mbegu, ulio juu ya uso wa nchi yote pia, na kila mti, ambao matunda yake yana mbegu; vitakuwa ndivyo chakula chenu;

Danieli 1:8, 12,15 - Lakini Danieli aliazimu moyoni mwake ya kuwa hatajitia unajisi kwa chakula cha mfalme, wala kwa divai aliyokunywa; basi akamwomba yule mkuu wa matowashi ampe ruhusa asijitie unajisi.

12 Tafadhali utujaribu sisi watumishi wako muda wa siku kumi; na watupe mtama tule, na maji tunywe.

15 Hata mwisho wa zile siku kumi nyuso zao zilikuwa nzuri zaidi, na miili yao ilikuwa imenenepa zaidi, kuliko wale vijana wote waliokula chakula cha mfalme.

2. **Kulikuwa na wanyama najisi na walio safi nyakati za Nuhu? Mwanzo 7:2,3 na wakati wa Petro? Matendo ya Mitume 10:14**

Mwanzo 7:2-3 - Katika wanyama wote walio safi ujitwalie saba saba, mume na mke; na katika wanyama wasio safi wawili wawili, mume na mke. [3]Tena katika

ndege wa angani saba saba, mume na mke; ili kuhifadhi hai mbegu juu ya uso wa nchi yote.

Matendo ya Mitume 10:14 - Lakini Petro akasema, Hasha, Bwana, kwa maana sijakula kamwe kitu kilicho kichafu au najisi.

3. **Mbali na matumizi ya wanyama walio safi kama chakula, kwa nini Nuhu aliagizwa aweke wengi kwenye Safina? Mwanzo 4:2-4; Mwanzo 8:20,21**

Mwanzo 4:4 - Habili naye akaleta wazao wa kwanza wa wanyama wake na sehemu zilizonona za wanyama. BWANA akamtakabali Habili na sadaka yake;

Mwanzo 8:20-21 - Nuhu akamjengea BWANA madhabahu; akatwaa katika kila mnyama aliye safi, na katika kila ndege aliye safi, akavitoa sadaka za kuteketezwa juu ya madhabahu. [21] BWANA akasikia harufu ya kumridhisha; BWANA akasema moyoni, Sitailaani nchi tena baada ya hayo kwa sababu ya wanadamu, maana mawazo ya moyo wa mwanadamu ni mabaya tangu ujana wake; wala sitapiga tena baada ya hayo kila kilicho hai kama nilivyofanya.

Maelezo: Habili alitoa mazao ya kwanza ya zizi lake, kuna uwezekano mkubwa kwamba aliwatumia kama chakula pia.

4. **Abrahamu walitumia vyakula safi au najisi? Mwanzo 18:7,8; Ezekieli 4:14**

Mwanzo 18:7-8 - Ibrahimu akapiga mbio kwenda kundini, akaleta ndama wa ng’ombe aliye laini, mzuri, akampa mtumishi, naye akahimiza kuiandaa. [8]Akatwaa siagi na maziwa, na ndama aliyoiandaa, akawaandikia mbele yao, akasimama karibu nao chini ya mti, nao wakala.

Ezekieli 4:14

14 Ndipo nikasema, Ee Bwana ELOHIM, tazama, roho yangu haikutiwa unajisi; maana tangu ujana wangu hata sasa sijala nyamafu, wala iliyoraruliwa na hayawani; wala nyama ichukizayo haikuingia kinywani mwangu.

5. **Unawezaje kutambua wanyama wa ardhi kavu walio safi na walio najisi? Mambo ya nyakati 11:2,3; 4-7**

Mambo ya Walawi 11:2-3 - Neneni na wana wa Israeli, mkiwaambia, Wanyama hawa ndio wanyama wenye uhai mtakaowala, katika hayawani wote walio juu ya

nchi. [3]Kila mnyama mwenye kwato katika miguu yake, mwenye miguu ya kupasuka kati, mwenye kucheua, katika hayawani, hao ndio mtakaowala.

Mambo ya Walawi 11:2-4,6-7 - Neneni na wana wa Israeli, mkiwaambia, Wanyama hawa ndio wanyama wenye uhai mtakaowala, katika hayawani wote walio juu ya nchi. [3]Kila mnyama mwenye kwato katika miguu yake, mwenye miguu ya kupasuka kati, mwenye kucheua, katika hayawani, hao ndio mtakaowala. [4]Pamoja na hayo, wanyama hawa hamtawala katika wale wenye kucheua, na katika wale walio na kwato; ngamia, kwa sababu yuacheua lakini hana kwato, yeye ni najisi kwenu. [6]Na sungura, kwa sababu hucheua, lakini hana kwato, yeye ni najisi kwenu. [7]Na nguruwe, kwa sababu yeye anazo kwato, ni mwenye miguu iliyopasuka kati, lakini hacheui, yeye ni najisi kwenu.

6. **Je, wanyama wanaoishi majini na kupaa angani wote ni safi? Mambo ya walawi 11:9-12; 13-19; Mathayo 15:36**

Mambo ya Walawi 11:9-19 - Katika hao wote walio ndani ya maji mtakula hawa; kila aliye na mapezi na magamba, ndani ya hayo maji, na ndani ya bahari, na ndani ya mito, mtakula hao. [10]Na hao wote wasio na mapezi na magamba, ndani ya bahari, na ndani ya mito, katika hao waendao majini, na katika wote wenye uhai, waliomo majini, hao ni machukizo kwenu, [11]watakuwa machukizo kwenu; msiile nyama yao, na mizoga yao itakuwa machukizo kwenu. [12]Kila asiye na mapezi wala magamba aliye ndani ya maji ni machukizo kwenu. [13]Kisha katika ndege hawa watakuwa ni machukizo kwenu; hawataliwa, ndio machukizo; tai, na furukombe, na kipungu; [14]na mwewe, na kozi kwa aina zake, [15]na kila kunguru kwa aina zake; [16]na mbuni, na kirukanjia, na dudumizi, na kipanga kwa aina zake; [17]na bundi, na mnandi, na bundi mkubwa; [18]na mumbi, na mwari, na mderi; [19]na korongo, na koikoi kwa aina zake, na hudihudi, na popo.

Mathayo 15:36 - akaitwaa ile mikate saba na vile visamaki, akashukuru akavimega, akawapa wanafunzi wake, nao wanafunzi wakawapa makutano.

7. **Twaweza kula wadudu warukao au wanyama wadogo wanaotembea kwa miguu minne kama vile panya?**

Mambo ya Walawi 11:20-23 - Tena vyote vitambaavyo vyenye mabawa viendavyo kwa miguu minne, hivi ni machukizo kwenu. [21]Pamoja na hayo, hivi vitambaavyo vyenye mabawa viendavyo kwa miguu minne ni halali kula, hao walio na miguu mirefu, ya kurukia juu ya nchi; [22]katika hao mna ruhusa kuwala; nzige kwa aina zake, na nzige kuu kwa aina zake, na panzi kwa aina zake, na

parare kwa aina zake. [23]Lakini vyote vitambaavyo vyenye mabawa, vilivyo na miguu minne, ni machukizo kwenu.

Mambo ya Walawi 11:29-30 - Tena katika vitu vile vitambaavyo, vitambaavyo juu ya nchi, hivi ni najisi kwenu; kicheche, na panya, na mjombakaka, kwa aina zake, [30]na guruguru na kenge, na mjusi na goromoe, na lumbwi.

8. **Tuna ruhusa kutumia damu kama chakula? Mambo ya Walawi 7:26; Matendo ya Mitume 15:29**

Mambo ya Walawi 7:26-27 -Tena msiile damu yo yote, ama ya ndege, ama ya mnyama, katika nyumba zenu zote. [27]Mtu ye yote alaye damu, mtu huyo atakatiliwa mbali na watu wake.

Matendo ya Mitume 15:29 - yaani, mjiepushe na vitu vilivyotolewa sadaka kwa sanamu, na damu, na nyama zilizosongolewa, na uasherati. Mkijizuia na hayo, mtafanya vema. Wasalamu.

9. **Je, kula nyama zilizosongolewa (wanyama waliokufa bila kuchinjwa) ni halali? Walawi 11:39,40; Matendo ya Mitume 15:29**

Mambo ya Walawi 11:39-40 - Kama akifa mnyama awaye yote, ambaye mna ruhusa kumla, yeye anayeugusa mzoga wake atakuwa najisi hata jioni. [40]Na yeye atakayekula nyama ya mzoga wake atafua nguo zake, naye atakuwa najisi hata jioni; yeye atakayeuchukua mzoga wake atafua nguo zake, naye atakuwa ni najisi hata jioni.

Matendo ya Mitume 15:29 - yaani, mjiepushe na vitu vilivyotolewa sadaka kwa sanamu, na damu, na nyama zilizosongolewa, na uasherati. Mkijizuia na hayo, mtafanya vema. Wasalamu.

10. **Masihi alisafisha vyakula vyote wakati wake au wa mitume? Mathayo 15:11,19-20; Matendo ya Mitume 10:14**

Mathayo 15:11,17,19-20 - Sikilizeni, mfahamu; Sicho kiingiacho kinywani kimtiacho mtu unajisi; bali kitokacho kinywani ndicho kimtiacho mtu unajisi. [17]Hamjafahamu bado ya kuwa kila kiingiacho kinywani hupita tumboni, kikatupwa chooni? [19]Kwa maana moyoni hutoka mawazo mabaya, uuaji, uzinzi, uasherati; wivi, ushuhuda wa uongo, na matukano; [20]hayo ndiyo yamtiayo mtu unajisi; lakini kula kabla hajanawa mikono hakumtii mtu unajisi.

Matendo ya Mitume 10:14 - Lakini Petro akasema, Hasha, Bwana, kwa maana sijakula kamwe kitu kilicho kichafu au najisi.

**11. Ni kweli ya kwamba vyakula vyote ni safi na hakuna cha kukataliwa? 1 Timotheo 4:4-5**

1 Timotheo 4:4-5 - Kwa maana kila kiumbe cha Elohim ni kizuri, wala hakuna cha kukataliwa, kama kikipokewa kwa shukrani; [5]kwa kuwa kimetakaswa kwa neno la Elohim na kwa kuomba.

Maelezo: Ni kweli vyote vilivyotakaswa kwa neno na kuomba ni safi. Elohim alinena na wana wa Israeli kuhusu Wanyama halali na najisi. Alichotakasa katika neno lake ndicho tunafaa kusafisha kwa maombi. Tuna kielelezo bora zaidi katika Mathayo 14:19

Mathayo 14:19 - Akawaagiza makutano waketi katika majani; akaitwaa ile mikate mitano na wale samaki wawili, akatazama juu mbinguni, akabariki, akaimega ile mikate, akawapa wanafunzi, wanafunzi wakawapa makutano.

**12. Tunastahili kuwa makini vipi kutojinajisi kwa chakula? Walawi 11:35 kwa nini tunafaa kujihadhari hivi? 1 Wakorintho 6:12,13(a),20**

Mambo ya Walawi 11:35 - Na kila kitu kitakachoangukiwa na kipande cho chote cha mizoga yao kitakuwa najisi; kwamba ni tanuru, au meko ya vyungu, kitavunjwa vipande vipande; ni najisi vitu hivyo, navyo vitakuwa najisi kwenu.

1 Wakorintho 6:12-13,19-20 - Vitu vyote ni halali kwangu, lakini si vyote vifaavyo; vitu vyote ni halali kwangu, lakini mimi sitatiwa chini ya uwezo wa kitu cho chote. [13]Vyakula ni kwa tumbo, na tumbo ni kwa vyakula; lakini Elohim atavitowesha vyote viwili, tumbo na vyakula. Lakini mwili si kwa zinaa, bali ni kwa Bwana, naye Bwana ni kwa mwili. [19]Au hamjui ya kuwa mwili wenu ni hekalu la Roho Mtakatifu aliye ndani yenu, mliyepewa na Elohim? Wala ninyi si mali yenu wenyewe; [20]maana mlinunuliwa kwa thamani. Sasa basi, mtukuzeni Elohim katika miili yenu

Maelezo: Vyombo vilivyoguzwa na nyama au damu ya wanyama najisi vilikuwa najisi katika Israeli. Hata leo, tunapaswa kutahadhari sana tunapopata chakula hata katika hoteli.

**13. Elohim huwachukia wanaojinajisi kwa chakula kiasi gani? Isaya 65:2-4; 66:17**

Isaya 65:2-4 -Nitazameni, nitazameni. Mchana kutwa nimewanyoshea mikono yangu watu walioasi, watu waendao katika njia isiyo njema, wakifuata mawazo yao wenyewe; [3]watu wanikasirishao mbele za uso wangu daima, wakitoa dhabihu katika bustani zao, na kufukiza uvumba juu ya matofali; [4]waketio kati ya makaburi, na kulala katika mahali pao pa siri; walao nyama ya nguruwe, na mchuzi wa vitu vinichukizavyo u katika vyombo vyao;

Isaya 66:17 - Watu wale wajitakasao, na kujisafisha katika bustani, nyuma yake aliye katikati; wakila nyama ya nguruwe, na machukizo, na panya; watakoma pamoja, asema BWANA.

Maelezo: Kulingana na maandiko tuliyosoma hapo juu. Ni wazi ya kwamba Wateule wote kwanzia Adamu, Nuhu, Abraham, Ezekieli, Danieli, Masihi, Petro na Paulo hawakujinajisi kwa chakula kisicho safi. Nasi iwapo tungependa kuiga mfano wao wa Imani ya kweli. Itabidi tujizuie chakula najisi pia. Waefeso 2:19-20

Waefeso 2:19-20

19 Basi tangu sasa ninyi si wageni wala wapitaji, bali ninyi ni wenyeji pamoja na watakatifu, watu wa nyumbani mwake Elohim.

20 Mmejengwa juu ya msingi wa mitume na manabii, naye Kristo Yahshuah mwenyewe ni jiwe kuu la pembeni.

## ULEVI

1. **Je, ni jukumu la wahubiri kufundisha kinachoadhiri jamii?**

1 Timotheo 4:13 - Hata nitakapokuja, ufanye bidii katika kusoma na kuonya na kufundisha.

2 Timotheo 4:1-2 - Nakutahadharisha mbele za Elohim, na mbele za Masihi Yahshua, atakayewahukumu walio hai na waliokufa; kwa kufunuliwa kwake na kwa ufalme wake; lihubiri neno, uwe tayari, wakati ufaao na wakati usiokufaa, karipia, kemea, na kuonya kwa uvumilivu wote na mafundisho.

2. **Tunaonywa vipi kuhusu walevi?**

Mithali 23:20 - Usiwe miongoni mwao wanywao mvinyo; miongoni mwao walao nyama kwa pupa.

3. **Ni majanga gani huwapata walevi?**

Methali 23:21, 29-35 - Kwa maana mlevi na mlafi huingia umaskini, na utepetevu humvika mtu nguo mbovu. Ni nani apigaye yowe? Ni nani aliaye ole? Ni nani mwenye ugomvi? Ni nani mwenye mguno? Ni nani aliye na jeraha zisizo na sababu? Ni nani aliye na macho mekundu? Ni wale wakaao sana kwenye mvinyo; waendao kutafuta divai iliyochanganyika. Usiitazame mvinyo iwapo ni nyekundu; iitiapo bilauri rangi yake, ishukapo taratibu; mwisho wake huuma kama nyoka; huchoma kama fira. Macho yako yataona mambo mageni; na moyo wako utatoa yaliyopotoka. Naam, utakuwa kama alalaye katikati ya bahari; au kama yeye asinziaye juu ya mlingoti. Utasema, wamenichapa wala sikuumia; wamenipiga wala sina habari; nitaamka lini, nitazidi kuitafuta tena.

4. **Ulevi huleta maangamizi?**

Nahum 1:10 - Kwa maana wangawa kama miiba iliyotatana, na kunyweshwa kana kwamba ni katika kunywa kwao, wataliwa kabisa kama mabua makavu.

5. **Mtu wa kwanza kujihusisha na ulevi alileta madhara gani?**

Mwanzo 9:21-22, 24-25 - Akanwa divai, akalewa; akawa uchi katika hema yake. Hamu, baba wa Kanaani, akauona uchi wa baba yake, akawaeleza ndugu zake wawili waliokuwa nje. Nuhu akalevuka katika ulevi wake, akajua mwana wake mdogo alivyomtendea. Akasema, Na alaaniwe Kanaani; atakuwa mtumwa kabisa kwa ndugu zake.

6. **Ni dhambi zipi hujumulishwa pamoja na ulevi?**

1 Wakorintho 5:11 - Lakini, mambo yalivyo, naliwaandikia kwamba msichangamane na mtu aitwaye ndugu, akiwa ni mzinzi au mwenye kutamani au mwenye kuabudu sanamu au mtukanaji au mlevi au mnyang'anyi; mtu wa namna hii msikubali hata kula naye.

Waefeso 5:18 - Tena msilewe kwa mvinyo, ambamo mna ufisadi; bali mjazwe Roho.

7. **Je, ulevi hupelekea mtu kufanya dhambi?**

Mwanzo 19:32-35 - Haya, na tumnyweshe baba yetu mvinyo, tukalale naye, ili tumhifadhie baba yetu uzao. Wakamnywesha baba yao mvinyo usiku ule,

akaondoka huyo mkubwa akalala naye, wala yeye hana habari alipolala wala alipoondoka. Ikawa siku ya pili, mkubwa akamwambia mdogo, 'Tazama, nimelala jana na baba yangu, tumnyweshe mvinyo tena usiku huu, ukaingie ukalale naye.' Wakamnywesha tena baba yao mvinyo usiku ule, akaondoka mdogo akalala naye, wala yeye hana habari alipolala wala alipoondoka.

**8. Ni kitu gani muhimu huondolewa na ulevi?**

Hosea 4:11 - Uzinzi na divai na divai mpya huondoa fahamu za wanadamu.

**9. Je, ulevi huonyesha kutokuwa na tumaini?**

Methali 31:6 - Mpe kileo yeye aliye karibu na kupotea; kampe divai yeye aliye na uchungu nafsini.

Isaya 22:13 - Na kumbe! Furaha, na kuchekelea, na kuchinja ng'ombe, na kuchinja kondoo, na kula nyama, na kunywa mvinyo; tule, tunywe, kwa maana kesho tutakufa.

**10.Kosa hili hunasa pia wahubiri?**

Isaya 28:7 - Lakini hawa nao wamekosa kwa divai, wamepotea kwa kileo; kuhani na nabii wamekosa kwa kileo, wamemezwa kwa divai, wamepotea kwa kileo; hukosa katika maono, hujikwaa katika hukumu.

**11.Ushauri wa maandiko katika jambo hili ni upi?**

1 Petro 4:3 - Maana wakati wa maisha yetu uliopita watosha kwa kutenda mapenzi ya Mataifa; kuenenda katika ufisadi, na tamaa, na ulevi, na karamu za ulafi, na vileo, na ibada ya sanamu isiyo halali.

Methali 23:31 - Usiitazame mvinyo iwapo ni nyekundu; iitiapo bilauri rangi yake, ishukapo taratibu.

**12.Wenye kutengeneza au kuuza pombe huonekana vipi?**

Habakuki 2:15 - Ole wake yeye ampaye jirani yake kileo, wewe utiaye sumu yako, na kumlevya pia, ili kuutazama uchi wao.

Isaya 5:22-24 - Ole wao walio hodari kunywa kileo chenye nguvu, watu waume wenye nguvu kuchanganya vileo; wampao haki mwenye uovu, ili wapewe ijara, na kumwondolea mwenye haki haki yake! Kwa hiyo kama vile mwali wa moto uteketezavyo mabua makavu, na kama manyasi makavu yaangukavyo katika mwali wa moto; kadhalika shina lao litakuwa kama ubovu, na ua lao

litapeperushwa juu kama mavumbi; kwa sababu wameikataa sheria ya Bwana wa majeshi, na kulidharau neno lake aliye Mtakatifu wa Israeli.

**13.Wamekaribishwa wapi?**

Isaya 5:14 - Kwa hiyo kuzimu kumeongeza tamaa yake, kumefunua kinywa chake bila kiasi; na utukufu wao, na wingi wao, na ghasia yao, naye pia afurahiye miongoni mwao, hushuka na kuingia humo.

Maelezo - Funzo hili linatuhamasisha kuhusu dhambi ya ulevi na madhara yake. Biblia inatoa onyo kali dhidi ya walevi, ikionyesha kuwa ulevi huleta umaskini, ugomvi, na majeraha, na huondoa fahamu. Ulevi pia hufanya watu kutenda dhambi, kama vile usherati na uasi, na huathiri jamii nzima. Hata wahubiri wanapaswa kuwa waangalifu, kwani ulevi unawaathiri pia katika kazi zao za kiroho. Maandiko yanatufundisha kuwa tunapaswa kuepuka ulevi na kila aina ya ufisadi, na kuishi kwa heshima mbele za Elohim, tukitafuta nguvu ya Roho Mtakatifu badala ya kileo. Onyo kali limetolewa kwa wale wanaotengeneza au kuuza pombe, ikisemekana kuwa watakutana na hukumu kali. Hivyo basi, tunahimizwa kuishi maisha ya utakatifu, tukiepuka ulevi na matendo ya uovu ambayo yanaathiri si tu sisi wenyewe, bali pia jamii nzima.

## MAVAZI

1. **Baada ya wanadamu wa kwanza kumuasi Elohim, ni nini kilichofanyika kudhihirisha upendo kwao?**

Mwanzo 3:21 - Bwana Elohim akawafanyia Adamu na mkewe mavazi ya ngozi, akawavika.

Isaya 61:10 - Nitafurahi sana katika Bwana, nafsi yangu itashangilia katika Elohim wangu; maana amenivika mavazi ya wokovu, amenifunika vazi la haki, kama bwana arusi ajipambavyo kwa kilemba cha maua, na kama bibi arusi ajipambavyo kwa vyombo vya dhahabu.

2. **Je, ni sheria ipi Elohim alisisitiza kuhusu mavazi?**

Kumbukumbu la Torati 22:5 - Mwanamke asivae mavazi yampasayo mwanamume, wala mwanamume asivae mavazi ya mwanamke; kwa maana kila afanyaye mambo hayo ni machukizo kwa Bwana, Elohim wako.

3. **Inasemwaje kuhusu kufunikwa kichwa kwa wanaume?**

1 Wakorintho 11:4,7 - Kila mwanamume, asalipo, au anapohutubu, naye amefunikwa kichwa, yuaaibisha kichwa chake.

7 Kwa maana kweli haimpasi mwanamume kufunikwa kichwa, kwa sababu yeye ni mfano na utukufu wa Elohim. Lakini mwanamke ni utukufu wa mwanamume.

4. **Inasemwaje kuhusu kufunikwa kichwa kwa wanawake?**

1 Wakorintho 11:5-6 - Bali kila mwanamke asalipo, au anapohutubu, bila kufunika kichwa, yuaaibisha kichwa chake; kwa maana ni sawa na yule aliyenyolewa. Maana mwanamke asipofunikwa na akatwe nywele. Au ikiwa ni aibu mwanamke kukatwa nywele zake au kunyolewa, na afunikwe.

1 Wakorintho 11:10 - Kwa hiyo imempasa mwanamke awe na dalili ya kumilikiwa kichwani, kwa ajili ya malaika.

5. **Nini hasa imetiliwa mkazo kuhusu mavazi ya wanawake wote?**

1 Timotheo 2:9-10 - Vivyo hivyo wanawake na wajipambe kwa mavazi ya kujisitiri, pamoja na adabu nzuri, na moyo wa kiasi; si kwa kusuka nywele, wala kwa dhahabu na lulu, wala kwa nguo za thamani; bali kwa matendo mema, kama iwapasavyo wanawake wanaoukiri uchaji wa Elohim.

1 Petro 3:3-4 - Kujipamba kwenu, kusiwe kujipamba kwa nje, yaani, kusuka nywele; na kujitia dhahabu, na kuvalia mavazi, bali kuwe utu wa moyoni usioonekana, katika mapambo yasiyoharibika; yaani, roho ya upole na utulivu, iliyo ya thamani kuu mbele za Elohim.

6. **Je, ni kwa nini Baba wa Mbinguni alitia mkazo katika hali ya mavazi katika miili yetu?**

1 Wakorintho 3:16-17 - Hamjui ya kuwa ninyi mmekuwa hekalu la Elohim, na ya kuwa Roho wa Elohim anakaa ndani yenu? Kama mtu akiliharibu hekalu la Elohim, Elohim atamharibu mtu huyo. Kwa maana hekalu la Elohim ni takatifu, ambalo ndilo ninyi.

1 Wakorintho 6:19-20 - Au hamjui ya kuwa mwili wenu ni hekalu la Roho Mtakatifu aliye ndani yenu, mliyepewa na Elohim? Wala ninyi si mali yenu wenyewe; maana mlinunuliwa kwa thamani. Sasa basi, mtukuzeni Elohim katika miili yenu.

7. **Tusipojali tahadhari hii kuna uwezekano wa kuvutia wanadamu kuivunja amri ipi?**

Kutoka 20:14 - Usizini.

8. **Ni onyo gani imepeanwa katika makanisa yote ya Elohim?**

1 Wakorintho 11:16 - Lakini mtu yeyote akitaka kuleta fitina, sisi hatuna desturi kama hiyo, wala makanisa ya Elohim.

Maelezo - Biblia inafundisha kwamba Elohim anathamini kuvaa vizuri na kujipamba vizuri kama maonyesho ya hadhi, staha, na kujitoa Kwake. Katika Agano la Kale, alimpa Musa maagizo ya kina kwa mavazi ya ukuhani, akisisitiza jukumu lao katika kuakisi utakatifu wake na kuleta heshima kwa huduma yake (Kutoka 28:2-4). Paulo, katika Agano Jipya, aliwaita waumini kuvaa kwa kiasi na kwa adabu, wakipatanisha sura yao ya nje na imani ya ndani na uchaji kwa Elohim (1 Timotheo 2:9-10). Zaidi ya hayo, sheria na mafundisho ya Elohim (kama yale yaliyo katika Mambo ya Walawi 19:27-28 na Kumbukumbu la Torati 22:5), yanaonyesha umuhimu wa mavazi tofauti, ya utaratibu, na ya heshima ambayo yanaheshimu tabia yake ya utakatifu. Hatimaye, kuvaa vizuri na kujipamba huashiria utayari wa kiroho na heshima kwa Elohim, kama inavyoonekana katika Maandiko yote, kutoka kwa mavazi ya makuhani hadi mifano kama karamu ya harusi (Mathayo 22:11-14).

## JUKUMU LA MZAZI

1. **Mzazi ameshauriwa awalee watoto wake vipi?**

Waefeso 6:4 - Nanyi, akina baba, msiwachokoze watoto wenu; bali waleeni katika adabu na maonyo ya Bwana.

2. **Kwa nini ni muhimu mzazi kumhusisha Elohim katika kuwalea watoto?**

Zaburi 127:3 -Tazama, wana ndio urithi wa Bwana, uzao wa tumbo ni thawabu.

Matendo ya Mitume 2:39 - Kwa kuwa ahadi hii ni kwa ajili yenu, na kwa watoto wenu, na kwa watu wote walio mbali, na kwa wote watakaoitwa na Bwana Elohim wetu wamjie.

3. **Ahadi ya Elohim kwa wazazi wanaomhusisha katika ulezi ni ipi?**

Isaya 54:13 - Na watoto wako wote watafundishwa na Bwana; na amani ya watoto wako itakuwa nyingi.

4. **Ni bidii ya aina gani inahitajika katika kuwafundisha watoto?**

Kumbukumbu la Torati 6:6-7 - Na maneno haya ninayokuamuru leo, yatakuwa katika moyo wako; nawe uwafundishe watoto wako kwa bidii, na kuyanena uketipo nyumbani kwako, na utembeapo njiani, na ulalapo, na uondokapo.

5. **Kwa nini mzazi lazima atie bidii kuwafundisha watoto wake?**

Methali 22:6 - Mlee mtoto katika njia impasayo, naye hataiacha, hata atakapokuwa mzee.

Methali 29:17 - Mrudi mwanao naye atakustarehesha; naam, atakufurahisha nafsi yako.

Maelezo - Ni jambo linalofahamika kwamba mtoto akifundishwa miaka saba ya kwanza huyashika hayo maishani mwake yote.

6. **Ni sababu ipi ya kuwafundisha na kuwarekebisha watoto mapema?**

Methali 19:18 - Mrudi mwanao, kwa maana liko tumaini; wala usiikaze nafsi yako kwa kuangamia kwake.

7. **Kuwarekebisha mapema kunadhihirisha chuki ama upendo?**

Methali 13:24 - Yeye asiyetumia fimbo yake humchukia mwanawe; bali yeye ampendaye humrudi mapema.

8. **Kuwarudi watoto kunawafanya wapende na kuwaheshimu wazazi wao?**

Waebrania 12:8-10 - Basi kama mkiwa hamna kurudiwa, ambako ni fungu la wote, ndipo mmekuwa wana wa haramu ninyi, wala si wana wa halali. Na pamoja na hayo tulikuwa na baba zetu wa mwili walioturudi, nasi tukawastahi; basi si afadhali sana kujitia chini ya Baba wa roho zetu na kuishi? Maana ni hakika, hao kwa siku chache walituridi kama walivyoona vema wenyewe; bali yeye kwa faida yetu, ili tuushiriki utakatifu wake.

9. **Ni katika jinsi gani mzazi lazima awe kielelezo chema kwa wana wake?**

Tito 2:7 - Katika mambo yote ukijionyesha wewe mwenyewe kuwa kielelezo cha matendo mema, na katika mafundisho yako ukionyesha usahihi na ustahivu.

**10. Je, kuna umuhimu wa ushirikiano kati ya wazazi katika malezi ya watoto wao?**

Mwanzo 25:27-28 - Watoto wakakua, Esau alikuwa mtu stadi wa kuwinda wanyama, mtu wa nyikani, na Yakobo alikuwa mtu mtulivu, mwenye kukaa hemani. Isaka akampenda Esau kwa sababu alikula mawindo yake, na Rebeka akampenda Yakobo.

**11. Madhara ya wazazi kugawanyika katika malezi ni yapi?**

Mathayo 12:25 - Basi Yahshuah akijua mawazo yao, akawaambia, Kila ufalme ukifitinika juu ya nafsi yake, hufanyika ukiwa; tena mji au nyumba yoyote ikifitinika juu ya nafsi yake, haitasimama.

**12. Ni furaha iliyoje kwa mzazi kuona kizazi chake kikienda kwa njia za haki?**

Methali 17:6 - Wana wa wana ndio taji ya wazee, na utukufu wa watoto ni baba zao.

3 Yohana 1:4 - Sina furaha iliyo kuu kuliko hii, kusikia ya kwamba watoto wangu wanakwenda katika kweli.

Maelezo - Kwa ujumla, somo hili linasisitiza kuwa malezi ya watoto ni jukumu takatifu linalohitaji hekima, upendo, na ushirikiano na Elohim. Wazazi wanapaswa kuwafundisha watoto katika njia za haki mapema ili kujenga misingi imara ya kiadili, ambayo itaathiri maisha yao ya baadaye. Kumhusisha Elohim ni muhimu kwa sababu watoto ni zawadi kutoka kwake, na ahadi yake ni kwamba wale wanaofundishwa katika njia zake watapata amani na baraka. Pia, wazazi wanapaswa kuwa mfano bora, kuwarudi kwa upendo, na kushirikiana ili kuepuka migawanyiko katika familia. Furaha ya mzazi hutokana na kuona watoto wao wakifuata haki, jambo linaloleta amani na fahari kwa vizazi vyote, kama inavyosisitizwa na Methali 23:24.



**Uombeeni Yerusalem amani,**

**Na wafanikiwe wakupendao**

**Amani na ikae ndani ya kuta zako**

**Na kufanikiwa ndani ya majumba zako**

**Zaburi 122: 16 - 17**

**Knessiah Print Media**

Publishing Press of Knessiah Church of Elohim

Nairobi – Kenya

Contacts For Correspondence - Simu:

0721 218 834 / 0722 982 979 / 0702 028 465

Find Our Affiliate Video lessons Media, KTV

Kaloleni Church of Elohim